

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 4 Februari, 2021**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, leo ni Kikao chetu cha Tatu cha Mkutano wetu wa Pili. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

Kama tulivyoambiana ni maswali ya sera na mafupi. Kama hupo basi, swali lako ndiyo itakuwa bahati mbaya tena. Tuanze na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 24 Oktoba, 2019 Mheshimiwa Rais alitoa agizo kwa Halmashauri za vijijini ambazo zilikuwa zinakaa mjini kwamba ndani ya siku 30 ziweze kurudi kwenye maeneo husika ili kutoa huduma karibu

na wananchi. Baada ya siku 30 Halmashauri nyingi zilitekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na shida, inaonekana kama kuna kukaidi agizo la Mheshimiwa Rais, kwani wamehamisha ofisi lakini makazi bado wanarudi kulala mjini, hata kama kule walikohamia kuna nyumba na inapelekea Halmashauri kuzipa mzigo wa kugharamia mafuta kila siku ya kurudisha watumishi kwenda kulala mjini.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwenye Halmashauri hizo ambazo zimerudi vijijini na watumishi wanarudishwa kulala mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua tuliyofikia leo ambapo tuko kwenye Kikao cha Tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa King Musukuma, Mbunge wa Nzela, Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais alitoa maagizo kwa Halmashauri za Wilaya zote ambazo zilikuwa na Makao Makuu yake kwenye Makao Makuu ya Halmashauri za Miji kuhama mara moja na kwenda kwenye Makao Makuu huko ambako wananchi wa Halmashauri waliko, waweze kuwahudumia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, agizo hili Halmashauri nyingi zimeteketeleza na mimi nimepata bahati ya kupita kwenye baadhi ya Halmashauri, kwa wafanyakazi wenyewe kwa kuhamisha ofisi zao na kuhamishia kwenye maeneo hayo mapya, lakini na wao wenyewe kuishi huko.

Mheshimiwa Spika, tunatambua yapo maeneo yenye changamoto; hatuna nyumba za kutosha kwa ajili ya makazi yao, lakini kuna Halmashauri ambazo zina nyumba za watumishi na wananchi wanazo nyumba ambazo zinaweza kupangishwa na hili lilikuwa agizo la Mheshimiwa Rais; na agizo la Mheshimiwa Rais ni agizo ambalo linatakiwa litekelezwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge Musukuma alivyosema kwamba huko kuna makazi, kutokwenda ni kuvunja amri, kukataa amri ya Mheshimiwa Rais. Ni kosa kubwa sana kwenye utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaagize Wakuu wa Mikoa akiwemo na Mkuu wa Mkoa wa eneo ambako Halmashauri iliyotakiwa kuhama ilipo, Katibu Tawala wa Mkoa ambaye pia ni Mtendaji Mkuu kwenye Mkoa huo, ambapo kwenye Halmashauri zenye mazingira hayo ambayo watumishi wametakiwa waondoke kwenda kwenye makao mapya hawajaenda, waondoke mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kipindi cha kuondoka kilishatamkwa na Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, hatuna sababu ya kuwapa muda tena. Ni kuondoka mara moja baada ya tamko hili. Endapo hawatafanya hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Mkoa husika achukue hatua mara moja dhidi ya watumishi hao na hasa wale wote ambao hawataki kwenda kwenye maeneo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumeagiza haya, naagiza pia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo pia inasimamia Halmashauri hizi, kufuatilia kila Halmashauri iliyotakiwa kuhama kwenye maeneo ya zamani, kuhamia kwenye maeneo mapya ili watumishi wote waweze kuhamia na nitahitaji taarifa hizo keshokutwa Jumamosi, ofisini kwangu saa 4.00 asubuhi ili nijue ni Halmashauri gani ambayo bado watumishi hawajahama, ili tuchukue hatua nyingine za kinidhamu kwa watumishi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge, na ninyi hamieni majimboni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, umenipa nafasi nami niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali imetoa waraka kwamba mazao aina ya choroko, dengu na kadhalika kwa msimu huu yatanunuliwa na *AMCOS* kwa mkopo bila bei elekezi na watapeleka kwenye minada ya *TMX* na hatujui lini minada itatokea; na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kwimba ni wakulima wadogo wadogo ambao wamezoea kuuza sokoni kwa kilo tano, kilo kumi mpaka kilo 20 na wakishauza wanapata fedha *cash* wanakwenda kununua mahitaji yao kama chakula na kupeleka kwenye familia zao; hawa watu wanateseka kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa wafanyabiashara wapo sasa hivi ambao kila mwaka walikuwa wananunua mazao hayo kwa *cash*, kwa bei ya soko na wakulima walikuwa wanapata fedha taslimu (*cash*), kwa nini wasiruhusiwe kuendelea kununua mazao hayo wakati *AMCOS* wanajiandaa kuwa na fedha taslimu ya kulipa kwa wakulima ili tupate ushindani? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Umeshaeleweka. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mansoor, Mbunge wa Kwimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba upo waraka unaoelekeza kununua mazao ya choroko kwa mkopo. Sina uhakika kama kweli Wizara iliagiza inunue kwa mkopo, ila ninachojua ambacho pia nimekipatia

taarifa na tumeagiza pia Wizara ya Kilimo ifanyie kazi, ni pale ambapo Wizara ya Kilimo imeagiza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia kuwepo kwa ushirika kwa wakulima, iwe ni mahali ambapo wanaweza kuuza mazao yao kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ambao maeneo kadhaa ambayo wananchi wake hawajapata elimu kwa ule Mfumo wa Stakabadhi Ghalani inaonekana kama vile ni mkopo.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unawataka wakulima kukusana mazao, kuyaweka pamoja halafu kusubiri siku moja kutangaza soko. Kwa hiyo, kitendo kile cha wakulima kukusanya mazao na kuyaweka pamoja kusubiri soko, zile siku ndiyo inapotafsiriwa kwamba tayari wamekwenda kuuza na wamekopwa, kumbe mauzo bado, ndiyo mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Sasa mgogo huu nimeusikia pia Mkoani Mwanza, Simiyu, Mara kwenye mazao haya na Shinyanga kwenye zao hili la choroko.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, kama waraka ulitoka kwenda kuwaagiza Wakuu wa Mikoa wasimamie hili, mfumo huu kabla haujatekelezwa ni lazima wakulima wapate elimu ili waweze kuelewa mfumo huu unakuwaje? Kama hakuna elimu, kunatokea malalamiko haya, kwa sababu uzoefu pia, hata kwenye mazao kama korosho, mfumo ulipoanza kulikuwa na migongano mingi ambayo ilipelekea kutoelewana na wananchi, wakaanza kuilalamikia Serikali kwa kauli hiyo hiyo kwamba wanakopwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naagiza sasa mikoa yote ambayo inanunua mazao haya ya choroko na dengi, zao ambalo wazalishaji wengi wanazalisha kama alivyosema kilo tano, sita, saba; ili ukusanye dengi iweze kupata mzigo mkubwa na utangaze mnada, lazima itachukua siku nyingi. Kwa hiyo, kwa zao hili ni tatizo kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema Wakuu wa Mikoa waridhie kwanza eneo hili la choroko na dengi ambalo uzalishaji wake ni mdogo mdogo, ni muhimu tukaufikiria upya kuanza kwake tofauti na mazao yanayopatikana kwa wingi

kama vile korosho, chai, pamba, kahawa na mazao yale yanayozalishwa kwa wingi, yale inawezekana ukakusanya siku mbili ukapata mzigo mkubwa na kuuza kwenye mnada na kuwa na siku chache sana kufikia siku ya mauzo na mwananchi hawezi kulalamika. Ila fiwi, choroko na denguni zao ambalo linalimwa kwenye ekari moja, mtu anavuna kilo mbili. Sasa ukimpeleka kwenye mnada mpaka akae upate mzigo wa kutangaza mnada, lazima atalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye eneo hili, naiagiza Wizara ya Kilimo ifanye mapitio tena ya waraka huo na ione mazingira ambako wananchi wanaona kama wanakopwa, lakini kumbe ni subira ya kusubiri siku ya mnada kwa uchache wa zao lenyewe ili Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, tuanze na mazao yale ambayo yanapatikana kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna maeneo wameshaanza, wao waendeleo kwa sababu mfumo huu umekuja kututhibitishia kwamba unaleta bei nzuri sana ya zao siku ya mnada kwa sababu mnada ule unashindanisha wanunuzi. Kila mmoja anakuja na bei yake na wakulima watakuwa na uhuru wa kumchagua mnunuzi aliyeweka bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zetu zinaonesha, zao hilo hilo limewahi kuuzwa mpaka shilingi 600/= mpaka shilingi 700/=, lakini baada ya mnada lilienda mpaka shilingi 900/=, shilingi 1,200/= na zaidi, hasa pale Mkoani Shinyanga ambako walishaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara ya Kilimo ifanye mapitio tena kwenye eneo hili halafu tuwape mrejesho Waheshimiwa Wabunge na wananchi wajue ni nini kinatakiwa kifanyike kwenye mazao haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkansi Kaskazini, kutoka CHADEMA.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, dhana ya Serikali ya kutenga maeneo na kusimamia hifadhi zilizopo nchini kwetu ilikuwa ni kulinda rasilimali za nchi yetu. Sote tunajua wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi mbalimbali ni wahifadhi namba moja, jambo ambalo kwa sasa limebadilika kulingana na watendaji aidha ni wachache, kulingana na mambo yanayofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, natambua kumekuwa na kelele nyingi na malalamiko mengi kutoka kwa sisi Wabunge kwa wananchi wetu. Leo wananchi wanaozunguka hifadhi, wanaoshughulika na shughuli za kawaida ikiwemo kilimo, ufugaji na uvuvi, imekuwa changamoto ya kupigwa, kunyanyaswa, kunyang'anywa mifugo, jambo ambalo linakwenda kuondoa ile dhana ya wao kuwa wasimamizi wa hizi hifadhi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, miongoni mwa changamoto zinazopelekea vurugu hizo ni mipaka inayobadilishwa kila siku na mipaka mingine ambayo haieleweki, kwa maana ya kwamba havijawekwa vitu ambavyo vinaonesha alama kwamba hapa ni mpaka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujua Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kwenda kupitia upya maeneo hayo ambayo yanasababisha migogoro kwa wananchi wetu ili mipaka hiyo ieleweke; na pia wanapokwenda kutengeneza au kupima hiyo mipaka, iwe shirikishi. Napenda kujua Serikali ina mpango gani wa haraka?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto ya uwepo wa migogoro kati ya wananchi waliopo pembezoni mwa Hifadhi zetu za Taifa, mapori tengefu ambayo yameweka ukomo wa wananchi hao kuingia kwenda huko. Migogoro hii mara nyingi imetokana na kutoeleweka kwa uwepo wa mipaka kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili Serikali imefanya jitihada kubwa; moja, ni kutoa elimu ya wananchi walioko kwenye vijiji vilivyo karibu na mipaka hii; kwanza kutambua ukomo wa mipaka ya Hifadhi hizo za Taifa na maeneo ambayo wananchi wanaishi huku wakiendelea kupata huduma za kijamii kwenye suala la uchumi na mambo mengine, kwa mfano kilimo, mifugo na shughuli nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa migogoro kwenye maeneo haya ni pale ambapo kama Mbunge alivyosema, mipaka haieleweki. Jukumu hili tumeshawapa Wizara ya Maliasili kuhakikisha kwamba wanapitia ramani zilizopo na kwenda kila mahali palipo na migogoro ili kuondoa migogoro hii ili wananchi waweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameonesha kwenye Jimbo lake pia kuna migogoro ya hiyo, ndiyo sababu amekuja na swali hili. Kwa hiyo, nimuagize sasa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kufika Nkasi Kaskazini kuona mgogoro huo ili kutatua tatizo hilo kwa kubainisha vizuri mipaka na kuweka alama zinazoonekana zitakazomwezesha mwananchi kutokuingia kwenye eneo hilo ili kuepusha migogoro ambayo ipo. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo haya ya hifadhi, lakini pia mapori tengefu yanaendelezwa kwa malengo yaliyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunatamani kuona wananchi walipo pembezoni wakiendelea na maisha yao, shughuli zao za kijamii, kilimo, mifugo na indelezwe lakini pia kwa kuzingatia mipaka ile. Kwa hiyo, kama ni tatizo la mipaka, tayari Mheshimiwa Waziri atakuwa amepokea kauli yangu na agizo langu, aende Nkasi. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, siyo Nkasi tu, na popote pale ambako kuna migongano kati ya wananchi na mipaka ili tubainishe kwa uwazi kabisa na sasa zoezi hilo liwe shirikishi; wananchi walioko jirani washirikishwe na maafisa walikuwepo pale washirikishwe, wafanye kazi kwa pamoja na kila mmoja afanye kazi yake kwa amani na watu wajipange, waongeze uchumi wao kupitia fursa zilizopo kwenye maeneo yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini, uliza swali lako tafadhali.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kutokana na muitikio mkubwa wa wananchi wa Tanzania kulima mazao ya kimkakati ili kukuza uchumi wa nchi yetu, upo uwezekano baada ya miaka michache tukaongeza sana uzalishaji kwenye mazao haya. Kwa sasa sehemu kubwa ya mazao haya ya kimkakati soko lake ni nje ya nchi yetu, jambo ambalo linaminya kidogo fursa za ajira, lakini pia soko likiyumba kule, inaleta shida kwa wakulima wetu na kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujua, ni upi sasa mkakati maalum na mahususi wa Serikali kuhakikisha kwamba inawezesha uwekezaji kwenye viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa kwa mazao haya ya kimkakati kama zao la mkonge ili kuwasaidia wananchi wapate uhakika wa masoko na pia kuendelea kutengeneza ajira kwa wananchi wetu wa Tanzania? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa nae kwenye kampeni za kufufua zao la mkonge Mkoani Tanga kwenye kikao cha wadau na tulifanya ziara kwa pamoja kwa siku tatu mfululizo kupitia mashamba, viwanda, vinavyochakata zao la mkonge. Zao la mkonge ni miongoni mwa mazao yale ya kimkakati, tulianza na matano, tumeongeza mazao mawili kuwa saba na mazao hayo ni mkonge yenyewe pamoja na mchikichi ambao unalimwa sana Mkoani Kigoma na maeneo ya Ukanda wa Pwani. Tunapohamasisha kilimo cha mazao haya na kuyapa hadhi ya mkakati, mazao haya ni mazao yanayolimwa na jamii pana kwenye maeneo yake na mazao haya ndiyo yanayoleta uchumi wa mtu mmoja mmoja kwenye maeneo yanayolimwa, lakini pia hata uchumi wa kitaifa kwa kupata fedha nyingi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, lakini bado mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tunahamasisha kilimo si tu cha mazao haya ya kimkakati pamoja na mazao mengine ya chakula na biashara tunataka pia usalama wa chakula nchini uwepo, watu wapate chakula cha kutosha, lakini pia na mazao haya ya kibiashara yakiwemo haya ya kimkakati na mazao mengine ambayo hatukuyaingiza kwenye mkakati lakini tunatamani mazao haya yalimwe ili wananchi waweze kuuza, wapate uchumi wa kutosha na sisi pia tuwe na uwezo wa kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mkakati wa kutafuta masoko. Ni kweli mkakati tunao, kila zao tunajua maeneo ambako soko lipo, lakini tunapoupeleka kwenye masoko haya jambo la kwanza ambalo tunalizingatia ni kuongeza thamani ili wakulima wapate faida kubwa na mazao haya tunaposema kuongeza thamani tunakwenda sasa kwenye wito wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wa ujenzi wa viwanda ndani ya nchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, moja kati ya mkakati ambao tunao ni kuhakikisha kwamba tunakaribisha uwekezaji kwa Watanzania na walioko nje ya nchi kuja kuwekeza kwenye

viwanda kwa sababu tuna uhakika tuna ardhi ya kutosha, lakini pia malighafi ya mazao hayo tunaweza pia na tuna *labour* ya kutosha nchini kwa maana ya kwamba tunaweza kutengeneza ajira nyingi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Spika, sasa mkakati huu nilipokuwa ziara ya siku tatu mkoani Tanga tumepita kwenye viwanda na tumeona na kumesikia, sehemu kubwa ya viwanda vingi vinafanya kazi, lakini pia vingine havifanyi kazi kwa sababu ya uchakavu. Tunahitaji kubadilisha teknolojia ili tuwe na teknolojia ambayo sasa inaendelea vizuri.

Pili, viko viwanda ambavyo wawekezaji wamejenga vinakwama kupata masoko mazuri kwa sababu kuna bidhaa zisizokuwa na sifa zinazolingia nchini. Ili kuendeleza uwekezaji huo, moja kati ya jambo kubwa tunalolifanya ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti bidhaa za kutoka nje ili kuwezesha uwekezaji wa ndani kukua na kuuletea manufaa makubwa kwa kupata fedha za kutosha na ajira. Hayo yote tunayazingatia ili tuweze kuhakikisha kwamba uwekezaji unakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aliyetaka kujua Serikali ina mpango gani, mpango wetu ni kuhakikisha kwamba tunaongeza hamasa ya ujenzi wa viwanda, lakini pia tunavilinda viwanda vya ndani. Kwa mfano tuliouona kwenye zao la mkonge, tunacho kiwanda kinazalisha nyuzi nchini kupitia zao la mkonge, na kiwanda hiki inazalisha bidhaa mbalimbali za nyuzi zenye ukubwa tofauti lakini pia tunazo bidhaa za plastiki zinaingia nchini huku Tanzania tukiwa tumeshazuia kuingiza plastiki. Kwa hiyo, nimeagiza Wizara ya Kilimo kufanya mapitio kwenye viwanda vyote vinavyozalisha nyuzi za plastiki huwa tukiwa na viwanda vinavyozalisha nyuzi za mkonge tunaoulima hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulishapiga marufuku matumizi ya plastiki lakini tulisema tutaenda kwa awamu. Tulianza na plastiki za kubebea mizigo na zile za viroba. Sasa tutaenda

mbali zaidi tunaingia kwenye nyuzi kwa lengo la kumlinda mwekezaji wetu aliyejengwa kiwanda nchini, lakini pia anayetumia zao letu la mkonge kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwemo na nyuzi lazima tumlinde ilia pate faida na sisi tunufaike kwa kupata soko zuri, kupata ajira kwa watu wetu lakini pia kuhakikisha kwamba wakulima sasa wanahamasika kulima kwa sababu ya uhakika wa soko. Huo ndiyo mpango wetu wa Serikali kwenye eneo hili. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, CHADEMA.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia na mimi nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu nchi yetu imepata uhuru, Watanzania zaidi ya asilimia 75 ni wakulima kutokana na Serikali kutangaza kilimo ni uti wa mgongo lakini wakulima wetu hawa ambao ni Watanzania wameendelea kulima kilimo cha kutegemea mvua ya Mwenyezi Mungu ambacho kimekuwa hakina tija kwao wala tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini mkakati wa Serikali wa kuwatoa Watanzania wakulima kwenye kilimo hiki kisichokuwa na tija kwao na kwa Taifa letu kuwapeleka kwenye kilimo ambacho kitaweza kutuondoa Watanzania kwenye wimbi la umaskini na kwenda kufikia sasa kwenye uchumi wa kati ambao utakaokwenda kukidhi mahitaji ya muonekano kwa Watanzania wetu? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuntiy Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba Serikali yetu sasa hivi inasisitiza kilimo ili kiweze kutoa manufaa au tija kwa

wale wanaolima na wito huu wa kulima mazao haya ya biashara na chakula ni mkakati ule ule wa kuongeza tija kwa kilimo chetu. Ni kweli kwamba tukitegemea kilimo kinachotegemea hali ya hewa kama mvua pekee hatuwezi kupata tija. Nini tumekifanya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina taasisi au Kurugenzi ya Umwagiliaji ambayo yenyewe tumeipa bajeti ya kuhakikisha kwamba wanahakikisha tunafufua kilimo cha umwagiliaji nchini kitakachomwezesha mkulima kulima wakati wote masika, lakini wakati wa kiangazi ili uzalishaji uwe mkubwa na mkulima anapolima apate mazao ya kutosha, akiamua kuyauza kama atapata ziada, atapata uchumi lakini pia kumhakikishia usalama wa chakula pale anapozalisha, lakini kama ni zao tu la biashara kuendelea kumtafutia masoko. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali katika hili ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na kilimo cha aina zote mbili cha kutegemea hali ya hewa ya mvua lakini pia na umwagiliaji ambao pia tumeimarisha na tunaendelea pia kubaini maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji na kuanzisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, Mheshimiwa Kunti yeye anatoka Chemba, Chemba ni eneo ambalo limepitwa na mto mkubwa sana ambao unatiririsha maji mpaka maeneo ya Bahi. Mto ule unapitisha maji masika pamoja na kiangazi. Mkakati ambao tunao maeneo yote yanayopita maji yale kwenye mto pembezoni tunaona wakulima wapo ambao wanalima. Sasa tunawaanzishia miradi ya umwagiliaji ili wakulima hao waweze kulima kilimo ambacho kitawapatia fursa ya kutosha ili waweze kunufaika na kilimo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo yetu kilimo chetu nchini kiwe na tija kwa wakulima, kituletee mazao ya chakula ya kutosha, pale ambapo wanalima mazao ya kibiashara basi wapate mazao ya kibiashara ya kutosha. Kwa ujumla wake tutaanza kuleta tija kwa wakulima, lakini pia kwa nchi na kuifanya nchi yetu kuwa na usalama wa chakula cha kutosha kwa kulima chakula cha kutosha na ziada. Huo ndiyo mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba Serikali na wananchi wake wanalima kilimo hiki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mbunge wa Mwanga, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo uliza swali lako.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali imetumia nguvu nyingi sana katika kupambana na uvuvi haramu na kulinda hifadhi zetu na kama sehemu ya mafanikio ya juhudi hizi idadi ya wanyamapori imeongezeka na katika maeneo mengine wanyamapori hawa wamesambaa na kuingia katika makazi ya watu na hivyo kuathiri sana maisha ya watu na shughuli za uzalishaji. Kwa kuwa tatizo hili sasa limeonekana kuwa la kudumu, Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suluhisho la kudumu la tatizo hili? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tadayo, Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana sana na swali ambalo mwanzo nimetoa ufafanuzi wake kwamba yako maeneo yana migogoro kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi. Swali la awali lilikuwa linazungumzia ule mgongano wao na hili linazungumzia wanyamapori walioko.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo haya tuliyoyahifadhi yana hawa wanyamapori na maeneo haya ya wanyamapori pia tumeendelea kuwahifadhi na kutoa tahadhari kwa wananchi walioko jirani na maeneo haya. Mkakati wa kuzuia wanyamapori hawa kuja kwenye makazi ya wananchi upo na unaendelea pale ambapo kwanza tumetoa elimu kwa wananchi wanaokaa karibu na maeneo haya ya wanyamapori kuwa na tahadhari. Wanapofanya shughuli zao wasiingie kwenye eneo la wanyamapori, pia tumewawekea *buffer* ya mita kama 500 ambazo wao wananchi walioko huko hata wanapoingia eneo hili lazima

wawe na tahadhari ya kutosha. Tunaamini wanyama walioko kwenye lile pori wanaweza kuja mpaka kwenye mpaka wa kijitanua kidogo wanaingia kwenye hili eneo la mita hizi 500, wanaweza wakazunguka hapo na kurudi. Inapotokea wakija huku sasa Idara ya Maliasili kupitia kikosi chao cha wanyamapori tumekiweka maeneo yale ambayo wanyamapori huwa wana tabia ya kutoka na kurudi huku kwa ajili ya kuwazuia kurudi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tunalifanya kwa kushirikisha pia vijiji vyenyewe, tunawapa elimu tunaanzisha ulinzi wa kijiji ambako pia ikitokea hilo nao wanasaidia kuwarudisha. Bado tunao wanyama wanatoka wanakuja lakini bado tumeendelea kuimarisha vikosi vyetu kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yana wanyamapori wanaotoka sana kuweka kambi dogo la kuhakikisha kwamba wanarudishwa kwenye maeneo hayo na makambi hayo tumeamua tuyaweke katika maeneo yote ambayo tunaona wanyama kama tembo ambao wameongezeka sana kwa sasa waweze kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, nimeliona hili pia nilipokuwa nafanya ziara wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, nimeona pia nikiwa Bariadi Mkoani Simiyu, nimeenda pia hata Tarime na maeneo mengine ambayo nimepita, nimepata malalamiko haya na tumeshawasiliana na Wizara ya Maliasili kujiandaa vizuri kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, tumeshaanza kusambaza vikosi vyetu, kulinda maeneo hayo ili pia wananchi wasiweze kusumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, wito kwa wananchi walioko kwenye vijiji ambavyo viko karibu na maeneo ya hifadhi, wasiingie sana kwenye mapito ya mara kwa mara ya wanyama. Tunao wanyama kama tembo ambao wao wana mapito yao miaka yote. Kwa hiyo, maeneo hayo kwa sababu tunaishi kwenye vijiji hivyo, tunayafahamu. Ni muhimu kuwa na tahadhari kwenye maeneo haya ya mapito ili tusije tukawa tunaingiliana na hawa wanyama, lakini bado mkakati wetu ni ule ule. Kwa hiyo, tushirikiane pamoja kuhakikisha kwamba tunawahifadhi wanyama wetu na

madhara ambayo yanajitokeza pia tunaendelea kuyadhibiti ili yasiweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wa kudhibiti hatari hii unaendelea chini ya maliasili kwa kuweka makamanda kwenye maeneo hayo na kila wilaya iliyoko kwenye mpaka tuna kitengo hicho ambacho pia kinafanya kazi hiyo kubaini kwenye mipaka yake kwamba wakati wote tunakuwa salama. Lengo ni kuwalinda wananchi wanaoendelea na shughuli zao, lakini pia kuwalinda wanyamapori ambao pia na wao watatupatia tija kwa shughuli za kitalii na uhifadhi wa wanyama wetu kwa ajili ya sasa na vizazi vijavyo. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa.

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa ziarani Mwanza katika ziara yake ya kikazi alitoa tamko kwa nchi kuhakikisha wanafunzi wote wanakwenda darasani mwisho tarehe 28 mwezi wa pili. Tamko hilo liliungwa mkono na wananchi nchi nzima na wakuu wa mikoa wakalisimamia, wakuu wa wilaya wamelisimamia tunamshukuru Mwenyezi Mungu. Majengo yamejengwa, kuna maboma mengi katika nchi hii yamekamilika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nini tamko la Serikali kuhusiana na pesa za kumalizia haya majengo kwa nchi nzima ili watoto wote waingie kutokana na idadi ya siku uliyokuwa umetoa tarehe 28 Februari? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.



**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasamu, Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uko ukweli kwamba Halmashauri zetu zimekuwa zikifanya kazi za ukamilishaji wa maboma haya kama jambo la dharura kila mwaka, lakini sasa tumefika tumeziagiza Halmashauri hizi kuhakikisha kuwa wana mpango wa muda mrefu wa kudumu unaosimamia ujenzi wa miundombinu hii ikiwemo madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu kwenye shule zetu ili jambo hili lisiwe la zima moto kila mwaka. Kwa kutumia pia takwimu tulizonazo Halmashauri zote zinajua kila mwaka zina wanafunzi wangapi wa darasa la saba wanaotaka kumaliza mwaka huo na ambao wanaweza kufaulu.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu walimu wanautumia kujua wangapi wanaweza kufaulisha. Kutokana na takwimu hiyo inaweza kuifanya Halmashauri ikajiandaa kujenga vyumba vya madarasa na miundombinu nyingine. Lakini pia hata kwa sekondari wanapomaliza kidato cha nne wanaweza kutabiri tutakuwa na idadi ya wanafunzi wangapi ambao wanaenda kidato cha tano. Halmashauri ikamudu kujipanga vizuri kujenga miundombinu ya kuwapokea kidato cha tano. Jambo hili sasa limeenda sambamba na agizo ambalo nimelitoa.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ulivyosema tumekuta maboma mengi yamejengwa na wananchi hajakamilishwa na umetaka kujua mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunakamilisha majengo hayo. Bado kwanza tumetoa wito kwa Halmashauri zenyewe kupitia mapato yao ya ndani na kupitia mipango yao kukamilisha maboma yaliyojengwa na wananchi ili tuwe na miundombinu ya kutosha kila mwaka tuweze kupata nafasi ya kuingiza wanafunzi. Lakini kupitia pia bajeti inayoandaliwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo haitoshi kumaliza maboma yote huwa tunaunga mkono juhudi za wananchi na Halmashauri kwa kukamilisha maboma yaliyopo kwa ajili ya kutoa nafasi ya wanafunzi wanaojiunga upya kwenye maeneo haya ili kila

mwanafunzi ambaye anapata nafasi ya kuendelea na masomo aende kwa wakati bila ya kuwa na awamu ya kwanza na ya pili na kuendelea huko mwishoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba pale ambapo uwezo wa Serikali unaendelea, tutaendelea ku-*support*, kuunga mkono jitihada za Halmashauri na wananchi katika kukamilisha maboma, lakini awali kabisa Halmashauri zenyewe zijiwekee mpango endelevu wa kuhakikisha kwamba unapata miundombinu ya kutosha ili wanafunzi hawa waweze kuingia kwenye majengo haya ili kusiwe tena na maagizo, maagizo. Kwa sababu itakuwa kila mwaka Waziri Mkuu au Makamu wa Rais au Mheshimiwa Raisa toe maagizo ya kila mwaka, jambo hili halikubaliki na sasa tumewaambia wajipange vizuri ili tuwe na miundombinu endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Tabasamu, Halmashauri zote zimesikia na kila Halmashauri imeagizwa iwe na mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba miundombinu inajengwa kila mwaka na kila wanafunzi wanapofaulu wanaingia moja kwa moja bila ya maagizo. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umeisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha mkubwa. Wabunge waliokuwa wameomba kuuliza maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu walikuwa 11. Tumebahatika kupata saba, wakati mwingine tutawachukua na hawa wengine waliobaki.

Katibu tuendeleee.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo. Mheshimiwa Anna, uliza swali lako sasa.

Na. 31

**Barabara za Kata ya Katumba**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara za Kata ya Katumba?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Na hili swali Waheshimiwa Wabunge mnaliona lilivyokaa? Haya ndiyo maswali ya Kibunge haya, *straight!* Ni lini Serikali itatengeneza barabara ya Kata ya Katumba? Sio unazungukaa

Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dugange majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 420.97 ambazo tayari zimeingizwa katika mfumo wa barabara za Wilaya (*DROMAS*). Aidha, Kata ya Katumba ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 185.88 ambazo ni sawa na asilimia 44 ya mtandao wote.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Nsimbo umetumia kiasi cha shilingi milioni 246.08 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Msaginya – Kanoge na Ikondamoyo – Kalungu. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 81.2 imetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Msaginya – Kanoge na barabara ya Kituo cha Afya Katumba – Mto Kalungu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara kote nchini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kata nyingine, hii kata ina barabara za urefu wa kilometa 185. Mheshimiwa Anna, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika mimi nasikitika sana, kata hii ina vijiji 16 hakuna mawasiliano kati ya kijiji hiki na kijiji kingine. Madaraja yote yamekwenda na maji, mito na barabara zote zimeunganika. Wananchi wa Kata ya Katumba wanapata shida sana. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara za wananchi wa Kata ya Katumba? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Naibu Waziri yuko tayari kwenda na mimi tukimaliza tu Bunge tukatembelee Kata ya Katumba yenye vijiji 16 ili aone uhalisia wake? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe ziara hiyo lazima mpate ruhusa ya Spika. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya

Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna changamoto ya barabara katika Halmashauri ya Nsimbo na katika kata hii husika, lakini Serikali katika bajeti ya Wilaya ya Nsimbo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ya shilingi milioni 556 tayari shilingi milioni 148 sawa na asilimia 27 zimekwishapelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa ajili ya kutekeleza miundombinu ya barabara ambazo zinaunganisha vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza Serikali inatambua changamoto hiyo na ndio maana imepeleka fedha kiasi hiki kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo na madaraja hayo na nimhakikishie kwamba utaratibu wa kuendelea kupeleka fedha nyingine kwa ajili ya kuimarisha miundombinu katika Halmashauri ya Nsimbo na katika vijiji hivi vya kata hiyo unakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba, niko tayari baada ya shughuli za Bunge kwenda naye katika Halmashauri hiyo kupitia vijiji hivyo ambavyo vinahitaji matengenezo ili tuweze kuongeza nguvu pamoja na kuondoa changamoto za wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, lakini kumsaidia Mheshimiwa Anna Lupembe japo sijawahi kufika huko, TAMISEMI, vijiji 16 kata moja! Nusu za barabara ya Wilaya hii ya Nsimbo, ukiangalia mtandao kwa kilometa, nusu ya barabara ziko kwenye kata moja kilometa 185. Hii kata ni kubwa mno, kwa vyovyote vile inatakiwa igawanywe kidogo watawalike, huyo Mtendaji wa Kata anafanyaje kazi vijiji 16 na wenzake wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

Na. 32

## Hitaji la Walimu wa Kike Shule ya Msingi Birise na Donsee

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kike katika Shule za Msingi Birise na Donsee ambazo hazina walimu wa kike?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, asante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya ukosefu wa walimu wa kike katika Shule ya Msingi Birise na Donsee zilizopo katika Halmashauri ya Chemba, Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imempeleka mwalimu mmoja wa kike katika Shule ya Msingi Donsee wakati ikiendelea na utaratibu wa kukamilisha kumpeleka mwalimu mwingine wa kike katika Shule ya Msingi Birise.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikijiandaa na mpango wa ajira na mgawanyo wa walimu wapya kwa Halmashauri zote nchini, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inazielekeza Halmashauri zote nchini kufanya msawazo wa walimu wa shule za msingi na sekondari kwa kuzingatia jinsia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi tena ya kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya ya Chemba tuna upungufu wa walimu wa kike chini ya asilimia 50. Huyu mwalimu ambaye amepeleka Shule ya Msingi Donsee ametolewa kwenye shule nyingine, wamemhamisha kutoka shule hiyo wamempeleka shule nyingine, lakini nataka kwenye mpango wa Serikali nimeambiwa hapa Serikali iko kwenye mpango.

Ni lini Serikali itatuletea walimu wa kike kwa ajili ya kunusuru maisha ya watoto wetu wa kike?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, changamoto zinazosababisha walimu wetu wa kike wasikae kwenye shule zetu hizo ni ukosefu wa nyumba za walimu, miundombinu ya barabara, ukosefu wa umeme, kuna changamoto nyingi kadha wa kadha. Walimu wakifika kule kwa mfano Shule ya Msingi Birise iko umbali wa zaidi ya kilometa 160, bodaboda ni shilingi 45,000 mwalimu wa kike unampeleka pale, hawezi kukaa mazingira ni magumu. Hata zahanati tu hawana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali, ni lini itakwenda kujenga nyumba za walimu, kuboresha miundombinu ya barabara, lakini pia suala zima la umeme ili tunapopeleka walimu wetu wa kike waende wakakutane na mazingira rafiki wapate kuishi kule na hatimaye watoto wetu wa kike waweze kupata na wao fursa ya kuhudumiwa na walimu hawa wa kike? Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mboni nilikuona. Endelea Mheshimiwa Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana, naomba nitumie fursa hii kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameuliza lini Serikali itapeleka walimu wa kike katika Halmashauri ya Chemba? Kama ambavyo nilijibu katika swali langu la msingi, Serikali bado imeendelea na utaratibu wake wa kawaida wa kuajiri walimu mara kwa mara na bahati nzuri sasa hivi tuko katika mpango wa mwisho wa kutoa ajira mpya kwa walimu kwa hiyo, hilo suala lake tualizingatia na tutaangalia zaidi jinsia, ili kuhakikisha kwamba, tunawasaidia watoto wa kike katika shule zote nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, alikuwa anauliza moja ya changamoto kubwa ni ukosefu wa miundombinu, hususan nyumba za walimu, na ndio sababu ambayo imesababisha walimu wengi kutokufika katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inatambua kwamba changamoto hiyo ipo na katika moja ya mkakati wa Serikali ambao umekuwepo sasa hivi, Serikali ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, imekuwa ikijenga miradi mingi kwa maana ya miundombinu katika sekta ya elimu. Tumekuwa tukijenga mabweni, madarasa, mabwalo, miundombinu ya vyoo pamoja na nyumba za walimu za *two in one*.

Mheshimiwa Spika, sasa lini tutajenga, mimi niseme tu kwamba, kwa sababu tuna mpango mwingine wa tatu ambao tutaueleza katika bajeti na kwa sababu umeelezeka huko ndani kulingana na bajeti, tutapeleka hizo nyumba za walimu katika yale maeneo ambayo yana shida zaidi ili kuhakikisha kwamba walimu wa kike wanafika maeneo hayo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge.



Na. 33

**Kiasi cha Fedha Tanzania imepata kutoka katika Mfuko wa Fedha za Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, ni fedha kiasi gani Tanzania imeomba na kupatiwa kutoka katika mfuko wa fedha za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi wa Umoja wa Mataifa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa, ndio mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako tukufu naomba kwa kibali chako niruhusu niseme angalau maneno mawili kabla ya kwenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, la kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima, lakini la pili nashukuru sana Chama Cha Mapinduzi, chama changu kuendelea kunianimi na kunipa dhamana hata kuniruhusu kwenda kugombea kwenye Jimbo la Tarime Vijijini, lakini pia nawashukuru sana wapiga kura wa Tarime Vijijini, Kanda Maalum kule Tarime Mara kwa kunipa ridhaa hii na hatimaye ahadi yangu ambayo nilitoa mbele yako imetimia. Lakini mwisho lakini sio kwa umuhimu namshukuru sana Mheshimiwa Rais kuendelea kuniamini kuiteua kama Naibu Waziri. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya maelezo hayo mafupi ninaomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, nijibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeomba na kupokea fedha kiasi cha dola za Marekani 8,488,564 kutoka katika Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Fedha kutoka Mfuko huo huombwa kwa kuandaa miradi inayokidhi vigezo vilivyokubalika. Fedha huombwa kupitia taasisi ya utekelezaji ya kitaifa au kimataifa, fedha hizo husajiliwa na Bodi ya Mfuko huo. Kwa Tanzania taasisi ya kitaifa iliyosajiliwa na Mfuko huo ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ambao walipata ithibati ya Mfuko huo Oktoba, 2017.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa miradi ifuatayo imeomba na kupata fedha kutoka mfuko huo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa ajili ya utekelezaji hapa nchini.

Mradi wa kwanza ni Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoa wa Dar es Salaam. Gharama za mradi huo ni dola za Marekani 5,008,564. Mradi ulitekelezwa mwaka 2013 hadi 2019 na Fedha zilizotolewa kupitia *UNEP*. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa ukuta wa kuinga maji ya bahari Kigamboni na Barabara ya Barrack Obama na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua llala na Temeke na kupanda mikoko maeneo ya Mweni na Kigamboni, Dar es Salaam.

Mradi wa pili ni Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za pwani ya Zanzibar. Gharama za mradi huo ni dola za Kimarekani 1,000,000. Mradi uliidhinishwa na Bodi ya AF na kiasi cha dola za Marekani 30,000 kilitolewa kwa ajili ya kuandika andiko la mradi. Fedha zitatolewa kupitia *NEMC* ambayo iliwasilisha kwa mtekelezaji wa mradi huo ambaye ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar. Aidha, andiko la mradi liliidhinishwa na sasa taratibu za kusaini mkataba kati ya *NEMC* na Mfuko wa *Adaption Fund* zinaendelea chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mradi wa tatu ni Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Wakulima na Wafugaji

Wilaya ya Kongwa. Gharama za mradi ni dola za Marekani 1,200,000. Mradi umeidhinishwa na Bodi ya AF na kiasi cha dola za Marekani 30,000 kimetolewa kwa ajili ya kuandika andiko la mradi. Fedha zitatolewa NEMC na kuwasilishwa kwa mtekelezaji ambaye ni NGO ya *Foundation for Energy Climate and Environment*.

Mradi wa nne ni Mradi wa Kimkakati wa Teknolojia ya Kuvuna Maji Kuimarisha Uwezo wa Jamii za Vijijini katika Maeneo Kame ya Mikoa ya Singida, Tabora na Dodoma. Gharama za mradi ni dola za Marekani 1,280,000. Mradi umeidhinishwa na Bodi ya AF na kiasi cha dola za Marekani 30,000 kimetolewa kwa ajili ya kuandika andiko la mradi.

Mradi wa mwisho na wa tano ni Mradi wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi wilaya ya Bunda. Gharama za mradi ni dola za Marekani 1,400,000. Mradi huu bado haujaidhinishwa na Bodi ya EF, lakini kiasi cha dola za Marekani 30,000 kimetolewa kwa ajili ya kuandika andiko la mradi. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba mifuko hii ya *Adaptation Fund* pamoja ile ya *LDCF* yaani *Least Developed Country Fund* hutengewa fedha maalum na Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi kupitia hii mifuko na fedha hizi hutakiwa zitumike katika muda maalum na ni fungu maalum, na kutokana na utaratibu ambao unaendelea katika Serikali au katika Wizara zetu imekuwa ikichukua muda mrefu sana kutayarisha maandiko na kuweza kuyawasilisha na mpaka kupata hizi fedha.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba, fedha hizi ambazo zinakuwa zinatengwa kwa ajili ya Tanzania zinaombwa kwa haraka na kuweza kupatikana katika muda

muafaka ili kupunguza hatari ya kuweza kuja kuzikosa hizi fedha au kuzipoteza?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, je, kuna utaratibu gani wa uwiano wa fedha hizi kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, uwiano wa fedha hizi kati ya pande zote mbili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kumekuwa na, kwa namna moja au nyingine ucheleweshaji wa fedha hizi, lakini tunaendelea kuimarisha utaratibu wa mawasiliano. Fedha hizi kwanza lazima mradi uandikwe, lakini vilevile tunashiriki na wenzetu wa Wizara ya Fedha ambao wana taratibu zao, tunahitaji *tax exemption* katika jambo hili. Kwa hiyo, lazima wataalam wetu wapitie kwanza halafu kisha wamshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha namna bora ya kuweza kuruhusu mradi uweze kuendelea. Wakati mwingine unalazimika kwenda *site*, hiyo ndio inasababisha muda unakuwa mrefu kidogo, lakini tunaahidi mbele ya Bunge lako tukufu kwamba tutachukua hatua za haraka na miradi hii itakuwa haichukui muda mwingi sana kutekelezwa, ili tuweze kupata fedha hizo ambazo ni manufaa makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ambacho Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni kwamba kuna uwiano. Hii miradi kama nilivyotaja katika miradi mitano mradi ukiibuliwa kule upande wa Zanzibar kiasi hicho cha fedha mradi utatekelezwa fedha zinapelekwa bila kuwa na mgawo, kwa hiyo, hapa kazi kubwa ni kujiimarisha, kuandaa watu wetu, wataalam wetu, waandae maandiko ya kutosha fedha

zinapatikana. Sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais ni ku-*facilitate* na kuratibu mambo haya yaweze kufanyika kwa haraka zaidi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu haya. Hizi fedha za Kongwa zilishafika siku nyingi na sasa karibu zinarudishwa zilikutoka kwa sababu, fedha zilishafika Wizara ya Fedha zinakwama hapo. Nafikiri haina hata wiki zitarudi zilikutoka, kwa hiyo, vitu vingine hebu sukumeni huko, hii Ofisi ya Makamu wa Rais bwana, lazima ipate hadhi yake pale.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Hassan Selamani Mtenga, Mbunge wa Mtwara mjini, uliza swali lako Mheshimiwa Hassan.

Na. 34

### **Matumizi ya Bandari ya Mtwara**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni sababu kwa sasa kutumia Bandari ya Mtwara kusafirisha korosho zinazolimwa Kusini badala ya kutumia njia ya magari ambayo yanasababisha uharibifu mkubwa wa barabara kwenda Bandari ya Dar es Salaam?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, wafanyabiashara wamekuwa wakitumia bandari ya Mtwara kusafirisha korosho zinazolimwa kusini mwa nchi kwa kuzingatia ushawishi wa Serikali wa kutumia zaidi bandari

hiyo badala ya kutumia njia ya magari ambayo ni kweli inachangia uharibifu wa barabara na wakati mwingine ajali za mara kwa mara. Katika kufanikisha nia hii, Serikali imeendelea kufanya vikao na wadau mbalimbali ili waweze kutumia Bandari ya Mtwara na hasa baada ya kufanya maboresho makubwa katika bandari hiyo kwa kujenga gati jipya na kuongeza kina cha maji ili meli kubwa zaidi ziweze kutia nanga katika bandari hiyo ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, changamoto za Bandari ya Mtwara ni utegemezi wa shehena ya aina moja tu ya korosho inayotoka Mtwara na hakuna shehena nyingine inayoingia katika Bandari hiyo. Hali hiyo inasababisha gharama za usafirishaji kuwa juu kutokana na meli kuja zikiwa tupu bila mzigo ili kufuata shehena ya korosho Mtwara tofauti na Dar es Salaam.

Kufuatia kuwepo kwa changamoto hiyo Serikali inaendelea kuwashawishi wenye meli kupunguza gharama za usafirishaji ili kufidia gharama za kusafirisha korosho kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa njia ya barabara. Aidha, Serikali kupitia TPA (Mamlaka ya Bandari) inaendelea kuitangaza bandari ya Mtwara ili zipatikane shehena zinazoingia katika bandari hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seleman swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka niulize swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo inawezekana nikayapokea au nisiyapokee.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Mtwara ambayo tulipokea takribani bilioni 153 kwa ajili ya matengenezo makubwa sana. Lakini cha kushangaza bandari hii kwa nini isitumike kwa meli kubwa ambazo zinaweza zikabeba mizigo? Kwa sasa hivi kuna kampuni moja ya meli ambayo kampuni hii inaitwa Sibatanza hawa watu ndiyo ambao wanaleta meli pale peke yao na kuja kufanya kazi ya uchukuzi.

Swali la pili kwa kuwa tumepoteza rasilimali nguvu kazi za watu takribani wachukuzi 6200 wamepoteza ajira kwenye Bandari ya Mtwara ni lini Naibu Waziri tutaongozana kwenda kuzungumza na wale wachukuzi ili waelewe hatma yao ya kazi zao za kila siku walizokuwa wanazifanya kwenye bandari ya Mtwara? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Msongwe wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imewekeza shilingi bilioni si 153 lakini bilioni 157 kuboresha Bandari ya Mtwara kwa kujenga gati na kuwekeza fedha nyingi hizi ni ili kuhakikisha kwamba Bandari ya Mtwara inatumika kwa meli kubwa.

Sasa juhudi zinazofanyika mpaka sasa hivi kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, moja ni kwamba Serikali tayari imeshafanya usanifu kujenga chelezo kwa ajili ya kujenga meli yetu chini ya *MSCL* ambayo itakuwa na uwezo wa kufanya biashara kati ya bandari ya Mtwara na bandari zingine. Lakini tayari Serikali imeshamshawishi mfanyabiashara Dangote aweze kutumia Bandari ya Mtwara kuleta bidhaa zake lakini pia na kusafirisha bidhaa zake.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ushoroba wa Mtwara kuanzia Mtwara, Tunduru, Songea, Mbinga mpaka Mbambabay barabara hii imekamilika tayari Serikali imeshafanya mazungumzo na upande wa wafanyabiashara wa Malawi kwamba waweze kutumia Bandari hii ya Mtwara, lakini pia mazungumzo yapo na upande wa Msumbiji Kaskazini Magharibi ili waweze kutumia bandari hiyo. Kwa maana hiyo tuna uhakika kwamba bandari hii itaendelea kufanyakazi kama ilivyokuwa imekusudiwa ndiyo maana Serikali imewekeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongozana na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga kwenda Mtwara mimi nasema hili halina shida naomba baada ya hapa tukubaliane lini tunakwenda lakini pia tunampongeza Mheshimiwa Mtenga kwa kuhakikisha kwamba bandari hii inafanyakazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana nilikuona Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE.ZUBERI M.KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye Bandari ya Mtwara, lakini *commitment* ya Serikali katika matumizi ya bandari ile bado haijaonekana. Mfano leo hii kule kuna kitengo cha mafuta (kuna *pump* ya mafuta ambayo inatakiwa wananchi wa Kanda ya Kusini wote wachukulie mafuta kwenye bandari ya Mtwara lakini ukienda kwa wafanyabiashara bado wanalalamika kwamba mafuta ya Mtwara yako bei juu kuliko Dar es Salaam, matokeo yake watu wanatoka Songea, wanatoka Lindi, wanatoka Tunduru wanafuata mafuta Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali namna bandari hii inaweza kutumika *efficiently* na sisi watu wa Kanda ya Kusini tukanufaika kwa kuwepo kwa bandari hii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Msongwe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nini *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Serikali ni kutengeneza miundombinu na tayari *commitment* ya Serikali imeonekana kuiboresha Bandari ya Mtwara ili iweze



kufanyakazi kama ilivyopangwa na ndiyo maana katika jibu langu la msingi sasa tunatangaza na kuitangaza Bandari ya Mtwara ili iweze kutumika kwa sababu sasa inauwezo wa kupokea meli zote kubwa na tungeshauri wafanyabiashara wote waweze kutumia bandari ya Mtwara na hasa wale wa Ukanda wa Kusini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye ulisimama.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba matumizi ya bandari ya Dar es Salaam yalisababisha uharibifu wa barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi kwenda Mtwara na hali ya barabara hiyo kwa sasa kwa kweli ni mbaya pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais aliagiza ikarabatiwe, lakini hali ni mbaya tunasafiri mpaka masaa saba badala ya masaa manne.

Je, Serikali iko tayari sasa kutenga fedha ya kutosha kuikarabati barabara hii kwa kiwango kinachotakiwa ili turudie hali yetu ya zamani?

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Msongwe tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la msingi ilikuwa ni bandari lakini ilikuwa linahusianisha na uharibifu wa barabara kwa sababu magari mengi yanaendelea kutumika. Naomba tu niseme baada ya hapa kwa sababu halikuwa swali la msingi, nitaomba nionane na Mheshimiwa Nape ili niweze kuona namna ambavyo Serikali imetenga fedha kwa sababu ni utaratibu wa Serikali kutenga fedha kufanya matengenezo kwenye barabara zote na hasa barabara muhimu kama hizo.

Lakini *figure* kamili sina, ila fedha inatengwa kwa kila barabara kuhakikisha kwamba hiyo barabara inatumika. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Nashon Bidyanguze Mbunge wa Kigoma Kusini tafadhali uliza swali lako

Na. 35

### **Ujenzi wa Daraja la Mto Maragalasi Ilagala**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliluliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu kujenga daraja katika Mto Maragalasi Ilagala?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, daraja katika Mto Maragalasi katika eneo la Ilagala liko katika barabara ya Mkoa wa Kigoma (Simbo – Ilagala – Kalya) yenye urefu wa kilometa 235. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 345 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa kutambua umuhimu wa daraja husika kwa wananchi, hususan wa Mkoa wa Kigoma na maeneo ya jirani, baada ya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, Serikali imejipanga kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza na kukamilisha ujenzi wa daraja hilo.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Bidyanguze tafadhali.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niishukuru Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini pia naomba nimuulize swali kwamba

eneo lile ni eneo ambalo lina watu wengi kwa maana kata sita katika ukanda ya maji na wakati mwingine kivuko kilichopo huwa kinasombwa na maji kupelekea wananchi wale wanaathirika kwa muda mrefu zaidi na eneo lile lina vituo viwili vya afya ambavyo vina *ambulance* mbili.

Kwa hiyo, naomba Serikali ione namna ya kufanya haraka katika kuhakikisha kwamba wananchi wale wa Jimbo la Kigoma Kusini katika maeneo yale ya kata sita wanapata ufumbuzi wa jambo hili. Ahsante.

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Msongwe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Nashon kwa kufuatilia jambo hili la barabara hii ya Ilagala. Niseme tu mimi Mkoa wa Kigoma nimefanyakazi na barabara hii naifahamu sana, ni kweli anachosema na ndiyo maana Serikali imeamua kutengeneza hili daraja ili kuondokana na adha hii.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea tayari Serikali iko kwenye hatua ya manunuzi ya kufuata Mhandisi Mshauri ambayo inasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusombwa na vivuko ni kweli kwamba kwenye daraja hili huu mto Maragalasi ni mto wenye zaidi ya kilometa 300 kwahiyo inawezekana kivuko hiki kinapata changamoto kwasababu ya magogo ambayo yanasombwa na mito na ndiyo maana usiku kivuko hiki huwa hakifanyakazi ila tu kinafanyakazi kunapotokea *emergency*.

Kwa hiyo tutaendelea na utaratibu huo huo lakini tutahakikisha kwamba hiyo barabara hilo daraja linakamilika mara mara fedha itakapopatikana. Ahsante.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Maji swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kyela Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila.

Na.36

### **Matatizo ya Maji Wilaya ya Kyela**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. ALLY A. MLAGHILA** aliuliza: -

Suluhisho la tatizo la maji katika Wilaya ya Kyela ni kutumia chanzo cha Ziwa Nyasa kama ilivyoielezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

Je, ni lini sasa mradi huo utaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masache Kasaka kwa kumuulizia swali hilo. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer* Maryprisca Wilfred Mahundi. Majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la huduma ya maji linaloikabili Wilaya ya Kyela. Katika kuhakikisha wananchi wa Wilaya hiyo wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosha, Serikali ina mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa muda mfupi Serikali imeendelea na ukarabati wa miradi

ambapo baadhi ya miradi iliyokarabatiwa tayari inatoa huduma ya maji ukiwemo mradi wa maji wa *Makwale Group* ambao unahudumia vijiji viwili vya Ibale na Makwale, Mradi wa maji wa Matema unaohudumia kijiji cha Matema (kitongoji cha Ibungu) na Kijiji cha Ikombe (Kitongoji cha Lyulilo) na mradi wa maji wa Lubaga ulioharibika muda mrefu umekarabatiwa na wananchi wanapata maji kwenye vituo 15 vya kuchotea maji. Aidha, kupitia bajeti ya mwaka 2020/2021 Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Mababu, Kisyosyo, Katumbasongwe, mradi wa Kapapa kwenda kijiji cha Mwaigoga na mradi wa *Sinyanga Group*.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za muda mrefu, Serikali imepangakutumia Ziwa Nyasa kama chanzo cha kudumu cha kusambaza maji kwa wananchi waliopo Wilayani Kyela pamoja na maeneo ya jirani. Hadi sasa timu ya kitaifa ya wataalam imefanya upembuzi wa awali kwa kufika Kyela na kubaini eneo la kijiji cha Ikombe kilichopo katika mwambao wa Ziwa Nyasa kuwa linafaa kujengwa chanzo cha maji. Mradi huu unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa kuwa mpango huu wa kutumia maji ya Ziwa Nyasa ni wa muda mrefu na Serikali imekuwa inatoa ahadi hii mara kwa mara na hata kwenye ziara yako Mheshimiwa Naibu Waziri ulipofika na ulituhidi mradi huu utaanza.

Je, ni lini mradi huu utaanza ili walau kata za Kajunjumele, Ipinda, Kasumulu pamoja na Kyela Mjini waweze kunufaika?

Swali la pili kwa Wilaya yangu Wilaya ya Chunya kwa mwaka huu wa fedha zilitengwa fedha kwa ajili ya kuhudumia miradi ya maji kwa vijiji vinane lakini mpaka sasa hivi fedha hizo hazijaweza kutoka.

Je, ni lini fedha hizo zinaweza zikatoka ili sasa watu wangu wa vijiji vya Sangambi, Shoga, Kambikatoto, Lualaje, Nkung'ungu, Soweto na Itumbi waweze kunufaika nahii miradi ya maji? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer* Maryprisca Mahundi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally, Mbunge wa Kyela nipende kusema kwamba upembuzi yakinifu unaendelea na muda wa kufika mwezi Mei utakamilika na tunatarajia mwaka mpya wa fedha 2021/2022 Serikali itakwenda kutekeleza mradi huo.

Kuhusiana na swali lake la nyongeza kwa Wilaya ya Chunya nipende kusema kwamba Serikali imeweka jicho la kipekee kabisa kwa Wilaya ya Chunya na Chunya ni moja ya ile miji 28 ambayo tunaitarajia kuja kutekeleza kwa fedha ambazo tumezipata za mkopo kutoka Serikali ya India kupitia benki ya Exim. Kwa hiyo kuanzia mwezi huu Machi shughuli ya kazi katika vijiji vya Sangambi na vile vijiji vya jirani pia vinakuja kutekelezwa, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana naona Mheshimiwa Masache, Mbunge wa Chunya hivi Jimbo la Lupa liliendaga wapi? Tunaendelea Waheshimiwa swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge bado tuko Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kyombo uliza swali lako tafadhali.

Na. 37

### **Maji ya Ziwa Victoria Kufikishwa Katika Kata za Jimbo la Nkenge**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Kata za Gera, Ishozi, Ishunju, Kanyigo, Kashenye, Bwanjai, Bugandika, Kitobo, Buyango na Ruzinga katika jimbo

la Nkenge zina shida kubwa ya maji licha ya kwamba zipo kwenye mwambao wa Ziwa Victoria.

Je, ni lini Serikali itawafikishia wananchi wa kata hizo maji kutoka Ziwa Victoria kama inavyofanya kwa mikoa mingine inayopata maji kutoka katika ziwa hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya maji katika vijiji 32 ambapo imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.084 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Misenyi.

Aidha, Wilaya ya Misenyi inatarajiwa kunufaika na Mradi wa Maji wa Maziwa Makuu kupitia Ziwa Victoria ambapo Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina unaotarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2021 na ujenzi wa mradi kuanza mwaka wa fedha 2021/2022. Vijiji 11 vitanufaika ambavyo ni Ishunju, Luhano, Katolerwa, Kyelima, Kashenye, Bushango, Kigarama, Bweyunge, Bukwali, Kikukwe na Bugombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali naomba kuongeza maswali ya nongeza mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kupitia Mheshimiwa Dkt. Magufuli, lakini pia na Waziri wa Wizara ya Maji pamoja na Naibu Waziri kwa usimamizi mzuri wa mradi

unaoendelea katika Jimbo la Nkenge wa Kyaka Bunazi wa bilioni 15.1 na Mheshimiwa Naibu Waziri nikushukuru sana juzi ulitoka kule kuangalia maendeleo ya mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi huo unahudumia vijiji saba katika Kata za Kyaka na Kasambia lakini kata zingine na vijiji ambavyo vimezunguka mradi huo. Je, ni lini Serikali itaongeza thamani ya mradi ya huo ambao una tenki lenye zaidi ya lita milioni mbili kuzunguka Kata za Nsunga, Mutukula, Bugorora, Bushasha ili thamani ya mradi iweze kuongezwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili Wilaya ya Misenye ambayo ni ndani ya Jimbo la Nkenge, ina vyanzo vingi vya maji na vyanzo hivi ni pamoja na Mto Kagera, lakini tuna Mto wa Ngono. Je, ni lini Serikali itaona ni vizuri kutumia vyanzo hivyo vya maji kuweza kupeleka maji katika vijiji ambavyo vinazunguka vyanzo hivyo vya Kata za Kakunyu, Kilimile, Mabale pamoja na Miziro? Nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, maji toka Mto Ngono.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nipende kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge na niseme kwamba mradi huu mkubwa ambao umeutambua na Mheshimiwa Waziri alifika pale na nikupongeze wewe binafsi kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano katika Wizara yetu na nikuhakikishie tu kwamba mradi huu kuongezwa thamani tayari michakato imeanza na wataalam wetu wanafika huko hivi karibuni na kila kitu kitakwenda sawa kama ambavyo uliweza kuongea na Mheshimiwa Waziri alipokuwa ziarani katika jimbo lako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia vyanzo vingine vya maji ili kukidhi na kuondoa shida ya maji katika vijiji vile vingine Mheshimiwa Mbunge nikuahidi tu kwamba tunatarajia kufikia mwezi Juni, tutakuwa tumekamilisha hatua mbalimbali za kuona namna gani tunaibua vyanzo vipya lakini vyanzo vile vilivyoko tunaviboresha na kuona mtandao wa maji



unaendelea kutawanyika katika jimbo lako vijiji vyote ambavyo havina maji kwa sasa viweze kupata maji. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa sababu ya muda tuendeleo na Wizara Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati.

Na. 38

### **Mahitaji ya *Ct-Scan* Hospitali ya Mkoa wa Iringa**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Hospitali ya Mkoa wa Iringa mashine ya *CT-Scan*?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uwepo wa huduma za kibingwa za vipimo vya mionzi kwa kutumia *CT-Scan*. Katika kuzingatia umuhimu huu tayari ilishakamilisha kufunga mashine hizi kwenye Hospitali za Kibingwa Taifa, kanda na Hospitali mbili za Rufaa za Mikoa zilipata mashine hizi mnamo Desemba, 2020 ambazo ni Mwananyamala na Sekou Toure.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi hili ni endelevu, Serikali inaendelea kuziwezesha hospitali zingine zote za Rufaa za Mikoa ikiwemo Iringa kufunga mashine hizi kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha za utekelezaji wa mpango huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta.

Waheshimiwa wenye kikao kule nyuma nitalazimika kuwatajeni majina na itakuwa haipendezi, naomba mkae kwenye viti vyenu. Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, kabla sijauliza kwanza nikushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri nimekuwa nikikusumbua sana kwa masuala ya afya, Mkoa wetu wa Iringa na wakati wote upo tayari. Naomba sasa nikuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa kipimo hiki katika hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa kumefanya wagonjwa wetu kupata matatizo makubwa na mateso makubwa kwa sababu ni lazima kwanza waje wafanye kipimo Hospitali ya Mkapa au Hospitali ya Muhimbili Dar es Salaam. Kwa wagonjwa wasio na uwezo wamekuwa wakipata mateso na kusababisha vifo vingi sana katika mkoa wetu wa Iringa.

Je, Serikali sasa iko tayari kuhamasisha sekta binafsi kwa kutumia miradi ya *PPP* ili iweze kufunga katika hospitali zetu kwa sehemu ambazo hakuna mashine hizo?

Mheshimiwa Spika, swali letu la pili, kwa kuwa kumekuwa na mfumo usio mzuri kati ya *MSD*, hospitali na vituo vyetu vya afya kuletewa madawa yasiyooombwa na kuacha yale ambayo wanayaomba. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akalizungumziaje suala hili la madawa katika hospitali zetu na vituo vya afya? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu si tu

amekuwa akieleza matatizo ya afya yaliyoko kwenye Mkoa wa Iringa, lakini vilevile amekuwa akiyazungumzia matatizo ya watumishi wa Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunaenda kwenye utaratibu wa bima ya afya kwa wote, lakini Serikali ina utaratibu wa PPP. Sasa kwa kuunganisha hayo kwa sababu utaratibu wa PPP unahitaji umakini wake kutekeleza tushiriki wakati tutaona jinsi ya kufanya namna tuweze kuona namna gani ya kushirikiana na *private sector* ili kufunga mashine hizo kwenye hospitali zetu, lakini ieleweke tu kwamba Serikali bado ina mpango huo wa kufunga kwenye hospitali zote, na sasa hapa tulipo kuna mashine mbili ziko njia kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba ameluliza kuhusu MSD, nalichukua wazo lake, ni wazo nzuri ambalo sasa Meneja wa MSD ataenda kulifanyia kazi kuhakikisha mawazo yake haya mazuri yanafanywa kazi kuhakikisha vinavyoagizwa ndivyo hivyo vinavyopelekwa kule. Lakini tunawaagiza Waganga Wakuu wa Mikoa na ma-DMO wote (Waganga Wakuu wa Wilaya) wahakikishe wanaweka takwimu sahihi za magonjwa ili wanapokuwa wanaagiza wafamasia waagize vitu kwa uhitaji wa hospitali husika bila kuagiza kwa namna nyingine tofauti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, ndani ya wiki hii tuhakikishe tutatimiza ile ahadi yetu ambayo ilivunjika, twende Iringa tukakae pamoja, tujenge uelewa wa pamoja tuje tutatue matatizo ambayo Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa wamekuwa wakizungumzia dawa hasa na vilevile na Mbunge wa Iringa Mjini, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Mifungo na Uvuvi swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa.

Na. 39

## Operesheni ya Vijiji vya Kudhibiti Utoroshaji wa Mifugo

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA** aliuliza:-

Je, fedha kiasi gani zimepatikana katika operesheni ya kudhibiti utoroshaji wa mifugo nje ya nchi na fedha hizo zitumikaje?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo, Mheshimiwa Pauline Gekul.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako tukufu naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema na kunipa kibali pia kurudi katika Bunge hili.

Nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Nishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi pamoja na wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kuniamini na kuendelea kunifanya kuwa mwakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ililazimika kuanzisha operesheni ya kufuatilia utekelezaji wa sheria, kanuni, taratibu zinazosimamia biashara ya mifugo baada ya kubaini ukiukwaji mkubwa uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wadau wasiowaaminifu. Operesheni hii ilifanyika kwa awamu tatu, awamu ya kwanza Serikali ilikusanya shilingi bilioni 7.1, awamu ya pili Serikali ilikusanya shilingi bilioni 5.7, awamu ya tatu Serikali ilikusanya shilingi bilioni 3.5.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinazotokana na operesheni ziliingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kutumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Serikali kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Pia naomba nitumie nafasi hii kuiomba Wizara ya Mifugo kabla sijauliza maswali yangu waje wakutane na wadau wa mifugo na wafanyabiashara katika Wilaya yangu ya Longido waweze kutathmini matokeo chanya na matokeo hasi ya operesheni hii ambayo imeingizia Serikali fedha nyingi tu ambazo swali langu la kwanza ninaomba kufahamu kwamba kati ya fedha hizi ambazo zimepatikana ni miradi gani ya maendeleo katika sekta ya mifugo ambayo ama imetekelezwa au imepangwa kutekelezwa ili wafugaji hawa waone tija ya fedha hizi zinapoingia Serikalini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ninapenda kufahamu pamoja na changamoto ya hawa wanaosimamia operesheni ambao wamedhulumu watu ambao wamekamatiwa mifugo bila kuwa na hatia na wengine wenye hatia waliofilisika, lakini na wao kwa taarifa yangu hawajalipwa stahiki zao. Ni lini Serikali itakwenda kuwalipa stahiki zao kwa kazi kubwa waliyofanya?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kwanza amehitaji kufahamu ni miradi kiasi gani ambayo imetekelezwa kupitia fedha hizi ambazo tunazikusanya.

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara yetu katika *Vote* ya 99 ambayo tunapangiwa Bunge hili tukufu bajeti yetu ya maendeleo ni shilingi bilioni 5.6 lakini katika hizo bajeti shilingi bilioni 5.6 tunakarabati minada, tunarekebisho majosho, mfano kwenye bajeti kiasi cha majosho 75 kwa Halmashauri nchini zinakarabatiwa, lakini majosho 20 yanajengwa kwa shilingi milioni 500, lakini pia tunajenga kiwanda cha chanjo pale Kibaha TVLA zaidi ya shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Spika, fedha tunapopangiwa na Serikali kila Wizara na sisi tunapopokea na kwa mwaka huu wa fedha shilingi bilioni tano zinaendelea kurudi kwa wafugaji wetu kwa kukarabati miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amependa kufahamu swali lake la pili kwamba watumishi hao wanaofanya operesheni wanakuwa wanafanya kwa awamu mbalimbali, lakini wanahitaji malipo. Serikali imekuwa ikiwalipa watumishi hao ambao wamekuwa wakifanya operesheni ya kudhibiti utoroshwaji wa mifugo na madeni yao yameshapunguzwa, sasa watumishi hao kote nchini wanadai shilingi milioni 662.9 na hizo fedha zimeshakaguliwa Mheshimiwa Mbunge, hivi karibuni mchambuzi ukishakamilika Wizara ya Fedha watalipa fedha hizo.

**SPIKA:** Tunaendelea Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, uliza swali lako Mheshimiwa Malembeka tafadhali.

Na. 40

### **Ajira zitokanazo na Uvuvi wa Bahari Kuu**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Kuna mpango wa kujenga bandari kubwa ya uvuvi inayotegemewa kutoa ajira zipatazo 30,000.

Je, ajira kwa upande wa Zanzibar zitakuwa ngapi kati ya hizo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa kujenga bandari ya uvuvi nchini ambapo inaendelea kufanya upembuzi yakinifu, uchambuzi wa awali umetoa mapendekezo ya kujengwa kwa bandari ya uvuvi katika eneo la Mbegani, Bagamoyo. Aidha, uamuzi wa kujenga bandari ya uvuvi ni miongoni mwa vipaumbele vya Taifa, lakini katika sera ya uvuvi ya 2015 lakini Mpango wa Maendeleo Miaka Mitano wa Awamu ya III 2021 hadi 2026.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa bandari kunakadiriwa kutoa ajira zaidi ya 30,000 wakiwemo wananchi kutoka Zanzibar, aidha, Serikali itahakikisha kuwa Watanzania kutoka pande zote nchini wananufaika na fursa za ajira, biashara ya mazao ya uvuvi na uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kununua meli nane kubwa za uvuvi, ambapo nne zitaenda Zanzibar na nne zitakuwa Tanzania Bara. Je, ni lini meli hizo zitanunuliwa ili zianze kutoa ajira na kutoa huduma kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika jibu lake la kwanza ameelezea hiyo ujenzi wa bandari ya uvuvi,

ningependa kujua je, upande wa pili wa Muungano utashirikishwa vipi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ununuzi wa meli nane ambazo zimesemwa katika ahadi yetu ya Serikali ununuzi huu utaanza hivi karibuni kwa kuwa Serikali sasa iko katika mazungumzo na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo, maelezo na mazungumzo hayo yanaendelea, yakishafanyika Wizara ya Fedha sasa itaingia makubaliano na mfuko huu ili ununuzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge alihitaji kufahamu kazi hii ya ujenzi wa bandari ambayo inaendelea kwa upande wa Bara na upande wa Zanzibar nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mazungumzo haya yanapoendelea kwa upande wa Bara pia upande wa Zanzibar wameanza mazungumzo na nchi ya Comoro na bandari ya Zanzibar pia itaanza kujengwa na ikijengwa maana yake ajira hizi sasa zitatolewa kwa pande zote.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo litatoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Joseph Mkundi.

Na. 41

### **Hitaji la Umeme wa REA – Maeneo ya Vitongoji Nchini**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya kusambaza umeme vijijini kupitia Mradi wa *REA* bado kuna shida kubwa katika maeneo ya vitongoji kwenye vijiji hivyo.



Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa umeme unasogezwa kwenye maeneo ya vitongoji ambavyo havijapata huduma hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Byabato, Naibu Waziri Nishati, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji visivyokuwa na umeme kupitia mzunguko wa pili wa mradi jazilizi (*Densification IIA*) katika mikoa tisa ya Mbeya, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza kwa kupeleka umeme katika vitongoji 1,103 kwa kuunganisha umeme wateja wa awali wapatao 69,079. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 197. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021. Kazi hii ni endelevu inayofanyika pia kupitia Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*).

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza Azma ya Serikali ya kufikisha huduma ya umeme katika vitongoji, Serikali kupitia Mradi wa *Densification IIB* unaotarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2021 utaendelea kupeleka umeme katika vitongoji vya mikoa kumi ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu, Songwe, kwa kupeleka umeme katika vitongoji 1,686 na kuunganisha umeme wateja wa awali wapatao 95,334. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 230. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, katika vitongoji 514 vilivyoko Jimboni Ukerewe vitongoji 238 bado havina umeme, lakini hata vile vitongoji

276 ambavyo tayari vina umeme, umeme wake unakuwa una matatizo makubwa, umeme unakatika mara kwa mara kwenye Jimbo la Ukerewe na hii inatokana na *cable* inayosafirisha umeme kutoka Kisorya kwenye Lugezi kuchoka.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua sasa Serikali ina mpango gani ili kuweka *cable* nyingine mpya iliyo sahihi ili kurekebisha hali hiyo na kusababisha wananchi wa Ukerewe kupata umeme wa uhakika?

Lakini swali langu la pili, kupitia mradi huu wa *REA* Serikali iliingia mkataba na makampuni binafsi kusambaza umeme kwenye maeneo ya visiwa, baadhi ya makampuni yalifanya kazi muda mfupi lakini hayakukamilisha kazi kwenye baadhi ya visiwa kwa mfano Visiwa vya Ghana, Visiwa vya Bulubi; makampuni yalisimika nguzo lakini wananchi hawakuweza kupata umeme. Lakini baadhi ya visiwa makampuni yalitowa umeme kwa mfano Kisiwa cha Ukala, Kisiwa cha Ilugwa lakini umeme ule ukawa unauzwa kwa bei ghali na baada ya Serikali *intervene* gharama ile ilishuka lakini wananchi wakawa wanapata umeme kwa mgao.

Nini kauli ya Serikali sasa ili iweze kutoa faraja kwa wananchi wa maeneo haya ya Visiwa vya Ukerewe? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati Mheshimiwa Steven Lujwahuka Byabato tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jimbo la ukerewe ni moja wapo majimbo ambayo yako katika miradi ni jimbo linalopata umeme kwa miradi ya *TANESCO* ya Gridi na miradi ya *off grid*. Kwa hiyo ni kweli kwamba kuna tatizo la umeme ambalo linafahamika katika maeneo ya Ukerewe na hasa shida ni

kama alivyosema kwamba hiyo kebo inayopeleka umeme kule imekuwa ikipata matatizo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ukerewe linapata umeme kutoka *sub station* yetu ya Kibara iliyopo pale Bunda na umeme ukitoka pale unasafirishwa kwa waya za kawaida kuelekea kisolia baada ya Kisorya unaenda kupitia kwenye maji kwenda Igongo na baada ya Igongo unaingia Lugezi ambacho ni kisiwa chenye cha Ukerewe. Kutoka Bunda kwenda mpaka Igongo siyo shida tena, lakini kutoka Igongo kwenda mpaka Lugezi kuna mita 700 ambapo ndiyo sasa ile *cable* inayopitisha umeme inapita majini na imekuwa ikipata shida kwa sababu siyo ile *cable* ambayo inatakiwa kupita kwenye maji.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali kupitia *TANESCO* imeshaanda mazingira ya kufanya njia ya muda mfupi na njia ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba basi inawekwa *sub-marine cable* kwa hizo mita 700 kuhakikisha kwamba sasa umeme utakuwa ni wa uhakika kwa Jimbo la Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, shida nyingine iliyokuwepo ni kwamba nguzo ambazo zimekuwa zikishikilia umeme kwenye eneo la Igongo nguzo zinazotembea kwa kilometa angalau moja zimekuwa zikijaa zikiingia kwenye maji kwa hiyo zinaharibika kwa hiyo mradi wa muda mfupi tutaweka pale nguzo za zege kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi wa umeme unaweza kuwa wa uhakika kwenye jimbo letu la Ukerewe. Lakini njia ya muda mrefu inayotarajiwa kufanyika kuanzia mwezi Januari mwakani itakuwa ndiyo hiyo hiyo ya kuweka *marine cable* ambayo itaanzia kutoka Jimbo la Bunda pale kwenda mpaka Ukerewe itakuwa ni mradi wa uhakika ambao utafikisha sasa umeme kwenye jimbo letu la Ukerewe bila wasiwasi wowote na tunatarajia labda mwakani ndiyo serikali itajipanga kutekeleza mradi huo ambao utagharimu takribani bilioni 12.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili kuhusiana na wale wanaopeleka umeme ambao walikuwa siyo wa

*TANESCO*. Serikali kupitia *REA* ilipata watu wakandarasi mbalimbali wa kupeleka umeme kwenye maeneo ambayo Gridi ya Taifa haijafika na umeme wa jua tunaita nishati mbadala, nishati jadidifu. Ni kweli kwamba maeneo ya ukerewe na maeneo mengine ya visiwa vilivyopo Muleba na Geita vimekuwa vikipata shida ya bei na shida kubwa ya bei ilisababishwa na wakandarasi waliotengeneza hiyo miradi kuwa na gharama kubwa ya uuzaji wa umeme kuzidi kile kiwango ambacho *TANESCO* inakielekeza.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inauza *unit* moja kwa shilingi mia moja lakini wenzetu walikuwa wanauza *unit* moja hadi kufikia shilingi 3,500 na Serikali Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza mwaka jana kwamba gharama hizo zishuke kuja kwenye gharama ambazo ni za kawaida ili kuepusha kuwa na gharama ya double standard kwenye maeneo yale yale ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tunavyofahamu ni kwamba maelekezo hayo yalitelekezwa kama alivyosema Mheshimiwa Mkundi lakini yale maeneo mbayo bado maelekezo hayo hajatekelezwa basi tunaomba taarifa hizo zifikishwe ili tuweze kuchukuwa hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wazabuni hawa ambao walikuwa wanatoa umeme huo tumekuwa tukizungumza nao na majadiliano yanaendelea na tutahakikisha kwamba wanaendelea kupeleka umeme wa uhakika kwa gharama nafuu na kuwafikia wateja wote muda wote ili adhima ya Serikali ya kufikisha umeme kwa ajili ya maendeleo ya viwanda kuwa salama yaweze kufikiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, naona wakati wa maswali kuna *movement* nyingi humu ndani, ningewashauri sana ukifika kaa kwenye kiti chako tu usiamehame kwenda kwenye viti vingine na nini, jamani si mnanielewa lakini au hamjanielewa bado? Eeh yaani wewe ukifika wewe kaa

hapo kwako halafu ukimwitaji mtu basi unamvizia wakati tunapokuwa tunatoka mtakuwa mnatembea mnaongea huko na kadhalika. Ni vema sana kufuata ushauri huu, jitahidi sana na kama nilivyosema unamuhitaji mtu basi wewe mwandikie *message* iende, kuna vijana wanazunguka huku, mwandikie kwenye simu yaani punguzeni *movement*. *Strongly advised* punguzeni *movement*.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni Katibu wa Vijana Mkoa wa Songwe Ndugu Hassan Lyamba na rafiki yake Ndugu Fadhili Fyambo. Karibuni sana.

Wageni 29 wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni wapigakura wake kutoka Rungwe Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Katibu wake Ndugu Ibrahim Nzunda. Karibuni sana mmetoka Tukuyu kwenye baridi kule karibuni sana Mbunge yupo sijui yuko wapi, eeh yuko pale eeh yeye katika wachache. (*Makofi/Kicheko*)

Mgeni waMheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaye ni mtoto wa kaka yake na Afisa Tarafa Simanjiro Mkoa wa Manyara Ndugu Lawrence Kiruswa. Karibu sana. (*Makofi*)

Mgeni waMheshimiwa Rashid Abdallah ambaye ni mke wake kutoka Kwala Mkoa wa Kusini Pemba Ndugu Mafunda Ibrahim. Karibu sana shemeji yetu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mwisenge Mkoa wa Mara Ndugu George Marato. Karibu sana Mwenyekiti, huyu Mwenyekiti anatoka Musoma Mjini pale pale maana Mwisenge ni pale pale mjini. (*Makofi*)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo walimu 10 na wanafunzi 90 kutoka Shule ya Msingi ya Mt. Monica kutoka Jijini Arusha ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya shughuli zake. Ooh Mtakatifu Monica wanapendeza hao, Mheshimiwa Mrisho Gambo yupo? Uko wapi leo watoto wake hawa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wabunge 29 wa Bunge la Vijana mwaka 2019 kutoka Mikoa mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Hawa walikuwa Wabunge wa Bunge la vijana 2019 karibuni sana mwendeleze nia yenu ya kutaka kuwa Wabunge kamili siku zijazo. *(Makofi)*

Matangazo Ofisi ya Katibu wa Bunge inawatangazia Wabunge wanawake wote kwa maana hiyo *TWPG* kwamba leo tarehe 4 Februari mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Wabunge Wanawake wote katika ukumbi wa Msekwa Wabunge Wanawake wote ukumbi wa Msekwa saa saba mchana, ajenda ya kikao ni kuchagua viongozi wa *TWPG* kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Kwa hiyo *TWPG* mnachaguana leo saa saba mchana mkutane pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hili ni tangazo langu sasa, hivi karibuni baadhi ya Wabunge wenzetu wamekuwa wakitumia nembo ya Bunge katika barua zao. Wanatumia *headed paper* ya Bunge kwenye barua zao katika kutoa taarifa mbalimbali kuhusu masuala yao binafsi au ya majimboni kwao.

Baadhi ya matukio mtakumbuka ni Mbunge kutumia karatasi yenye nembo ya Bunge kuteua Makatibu wake katika Jimbo lake na Mbunge kutumia karatasi yenye nembo ya Bunge kuwafukuza kazi Makatibu hao hao. *(Kicheko)*

Tarehe 1 Februari, 2021 nilisitiza na kuwakumbusha kuwa hairuhusiwi kwa mtu yeyote kutumia nembo ya Bunge yenye masuala binafsi ambayo hayahusu Bunge hili. Hata hivyo pamoja na msisitizo huo na ufafanuzi niliutoa siku hiyo bado baadhi ya Wabunge wenzetu wameendelea kutumia nembo hiyo kinyume na maelekezo tuliyokwishayatoa katika Mkutano wa *Briefing* wa tarehe 1 Februari, 2021.

Mbunge mwenzetu mmoja jana ametoa taarifa kwa umma inayohusu ufadhili wa masomo kwa watu wa jimbo

lake na ametumia nembo ya Bunge huku akijua Ofisi ya Bunge haihusiki wala haijui jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kutumia nembo ya Bunge ni kuuaminisha umma kuwa nyaraka hiyo inatoka Bungeni jambo ambalo si sahihi. Hivyo napenda tena kusisitiza yafuatayo:-

Moja, matumizi halali ya nembo ya Bunge ni kwa ajili ya barua za kiofisi zinazosainiwa Spika, Katibu wa Bunge au Maafisa wa Ofisi ya Bunge wanaoandika nyaraka kwa niaba ya Bunge. Ni kosa kwa Mbunge au mtu yeyote ambaye hahusiki katika makundi niliyoyataja hapo juu kutumia nembo ya Bunge kwa nyaraka binafsi kwani nyaraka hiyo inatafsiriwa kama ni nyaraka ya Ofisi ya Bunge.

Ifahamike kuwa matumizi ya nembo ya Bunge katika nyaraka zisizohusu Ofisi ya Bunge ni jinai inayoendana na matumizi mabaya ya nyaraka za Serikali. *(Makofi)*

Hivyo basi kuanzia leo tarehe 4 Februari, 2021 napiga marufuku kwa mara nyingine tena matumizi ya nembo ya Bunge kwenye nyaraka au barua binafsi za Wabunge zinazohusu masuala yao wanayoyajua wao wenyewe na Ofisi ya Bunge hayayafahamu.

Waheshimiwa Wabunge, ningeoomba tuzingatie sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mwenyekiti wa Tawi la Simba Mjengoni anapenda kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge ambao ni wapenzi na mashabiki wa wanachama wa timu ya Simba kwenye dhifa ya chakula cha jioni leo tarehe 4 Februari saa moja jioni katika hoteli ya Morena hapa Dodoma, *actually* anawakaribisha Wabunge wote kabisa kwenye hoteli ya Morena pale na hasa ya wa Yanga mnakaribishwa sana pale. Aidha, dhifa hiyo itahudhuriwa na pia na viongozi na wachezaji wa Simba, karibuni sana. *(Makofi)*

Niliwahi kuwaambia kwamba nitakuja kutoa takwimu za Bunge letu hili kielimu likoje na Bunge letu hili kiumri likoje, lakini bahati mbaya sana inakuwa vigumu kufanya hivyo kwa sababu baadhi ya Wabunge *consistently* hawatupatii taarifa hizo, kwa hiyo, inakuwa vigumu kupata picha halisi ya Wabunge wote. Kwa mfano kwenye umri bado Wabunge 76 hawajaandika umri wao, Wabunge 76 nafikiri ni wengi sanam sasa sijui kwa nini? Lakini kwa wale ambao tuna umri wao ambao unatoa picha hata hao sabini watakuwa humo humo inaonesha kwamba walio chini ya miaka 40 ni wachache na waliozidi miaka 50 ni wachache; walio wengi wako kati miaka 40 na miaka 50 kwa hiyo, Bunge hili ukiliita la vijana unakosea, ukiliita la wazee unakosea, hiyo ndiyo takwimu ambayo nikaitoa sasa hivi. Ahsante sana Katibu tuendele. *(Makofi/Kicheko)*

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS DKT. JOHN POMBE JOSEPH  
MAGUFULI ALIYOITOA WAKATI WA UFUNGUZI WA BUNGE LA  
KUMI NA MBILI TAREHE 13 NOVEMBA, 2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, kama nilivyokuwa nawabembeleza juzi jamani changieni changieni mkawa mnasita sita maana kesho tunafunga dirisha na kesho nafasi zitakuwa chache sana. Kwa hiyo, wengi mtachangia leo na wote mtakaochangia leo wote ni dakika tano tano.

**MBUNGE FULANI:** Eeh.

**SPIKA:** Eeh ndiyo.

**MBUNGE FULANI:** Vyama vyote?

**SPIKA:** Ndio wote kwa sababu wenyewe hamkutaka tangu mwanzo kwa hiyo ni takika tano, kwa hiyo, ukisikia



kengele unakaa chini hakuna ya kwanza au ya pili dakika tano tano. Kwa hiyo, jitahidi sana nenda moja kwa moja pongeza na kufanya nini, sisi tuna *record* huku dakika tano unakaa chini na kadhalika.

Kwa hiyo tunaanza Dkt. Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry Silaa dakika tano tano.

**MHE. DKT. RITTA R. KABATI:** Mheshimiwa Spika, Ahsante naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini moja kwa moja niende kwenye *point* nimshukuru Mwenyezi Mungu, nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi lakini pia niwashukuru wajumbe walionichaguwa nikiwemo humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake aliyotoa hapa Bungeni kwa sababu kwanza alitoa dira na maelekezo nini tufanye na na Serikali nini ifanye kwa hiyo kwetu sisi kazi yetu kufanya.

Mheshimiwa Spika, hotuba ambayo imekuwa elekezi kwa viongozi wote vilevile naomba nichukue nafasi kupongeza ya uchaguzi kwa kusimamia zoezi lile vizuri kwa kuwa uchaguzi ulikuwa uhuru na haki na viongozi wote walioingia humu ndani wameingia kwa uhuru na haki, niwapongeze Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi lakini pia wa vyama vya upinzani kwa sababu wote tunajenga nyumba moja.

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja nielekeze katika miradi ya maji kwa sababu sisi ni Wabunge Wanawake ambao tunawakilisha wanawake tumeona hotuba hii imelenga moja kwa moja kuhusiana na miradi ya maji. Ujenzi wa miradi ya maji imefanya wanawake wengi sana sasa hivi hawahangaiki kutafuta maji, tunaona kwamba katika Mkoa wetu wa Iringa kulikuwa na tatizo kubwa hasa miradi ya vijijini kwamba miradi ya Kilolo, kule Mufindi, Isimani, wanawake walikuwa wanapata shida sana hata katika Mkoa wetu wa Iringa unaona maji yalikuwa yanatuletea adha kubwa, kuna ndoa nyingi sana ziliweza kupata matatizo kwa sababu maji

ni uhai, lakini mwanamke anaamka asubuhi *time* ambayo anatakiwa ailinde ndoa yake anaenda kuiangaikia maji. Kwa hiyo, kwa kweli Mheshimiwa Rais amelinda hata ndoa zetu katika Mkoa wetu wa Iringa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu hata mimi nitowe ushauri kwamba Serikali sasa hivi ianze kuangali uvunaji wa maji kwa sababu maji kumekuwa na upotevu wa maji mkubwa, tukitengeneza miundombinu ya kuvuna maji hasa katika mabwawa tutasaidia hata mifugo yetu wakati ule hakuna mvua itapata maji, lakini vilevile tunaona kwamba hizi mvua zimekuwa zikija na mafuriko makubwa, kwa hiyo, tukivuna haya maji yatasaidia pia kuzuia uharibifu katika mito yetu, lakini pia hata mabarabara na madaraja wakati wa mvua za masika.

Mheshimiwa Spika, nizingumzie kuhusu suala la afya niipongeze sana Serikali yetu imeweza kujenga zahanati 1,998, vituo vya afya 487, Hospitali za Wilaya 96, Hospitali za Kanda tatu lakini maboresho ya afya yamesababisha hata kupunguza vifo vya akinamama na watoto. Tunaona mwaka 2015 vifo vilikuwa 11,000 lakini sasa hivi mwaka 2020 unaona vifo vingi vimepungua vimefikia mpaka vifo 3,000 kwa mwaka, hii yote ni kwa sababu ya maboresho mazuri ya vituo vya afya, lakini vilevile Serikali ihakikishe kwamba inaweka watumishi kwenye vituo vya afya, inaleta madawa ya kutosha, lakini naomba ili kupunguza vifo vya watoto njiti iwekeze kwenye vituo vya afya kwa sababu tunaona katika vituo vya afya hakuna zile *incubator* kwa ajili ya watoto, watoto wengi sana wamekuwa wakipoteza maisha katika vituo vya afya, kwa hiyo naomba sasa Serikali iwekeze sana kwenye vituo vya afya mambo *incubator*.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 27, imezungumzia kuhusu kilimo, Serikali inakusudia kuongeza tija na kufanya kilimo kuwa cha biashara. Karibu asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima, kwa hiyo, tukiwekeza kwenye kilimo ina maana kwamba sasa hivi tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda na kwenye kilimo ndipo ambapo tutapata malighafi. Kwa hiyo, kwa kweli tukiondoa changamoto nyingi

ambazo zipo kwenye kilimo, ndipo ambapo tunaona hata Mheshimiwa Rais amesema kwamba ni aibu kubwa kuwa na njaa kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini sasa hivi nchi yetu ya Tanzania ina uwezo hata wa kupeleka vyakula katika nchi nyingine. Lakini kuna mkakati mahususi kuhakikisha kwamba sasa hivi...

*(Hapa kengele lilia kaushia kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jerry Silaa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Rais aliyoitoa Bungeni akifungua Bunge letu hili la Kumi na Mbili.

Kwanza na mimi kwa sababu ni mara ya kwanza, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa mimi kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge lako hili tukufu. *(Makofi)*

La pili, nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi, chama ambacho nimekitumikia kwa zaidi ya nusu ya uhai wangu, kwa kunipa fursa, namshukuru sana Mwenyekiti, navishukuru vikao vya uteuzi na wanachama wenzangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na wenzangu kuunga mkono hoja, lakini vilevile naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba hii iliyobeba dira na maelekeo ya nchi yetu kwa miaka mitano. Hotuba hii ukiisoma na ile ya Bunge la Kumi na Moja, ukisoma utekelezaji wa Ilani, ukisoma machapisho mbalimbali ya taarifa ya uchumi, utaona jinsi gani Rais wetu amefanya kazi kubwa kwa miaka mitano, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya uchumi, uchumi wa nchi yetu umekua, Pato la Taifa limekuwa, mfumuko wa bei umekua uko katika hali nzuri, haujazidi asilimia 4.4, akiba ya fedha za kigeni kwa mara ya kwanza iko juu na inaendelea kuongezeka, thamani ya shilingi imeimarika sana, pongezi kubwa kwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika huduma za jamii, kazi kubwa imefanyika, vituo vya afya, zahanati zimejengwa nchi nzima na tumeona kwenye hotuba hii tunayojadili.

Mheshimiwa Spika, lakini labda kwa kifupi sana ni kuomba Bunge lako tukufu kwamba tuna kazi kubwa baada ya kumpongeza Rais kumsaidia ili malengo aliyoyaweka kwenye miaka hii mitano yatimie na katika kumsaidia wote tuna wajibu wa kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wa kwanza ni wasaidizi wake, na bahati nzuri tunaye Waziri Mkuu mchapakazi, mpenda watu, anafikika na Waheshimiwa Wabunge mtakuwa ni mashahidi. Lakini wako wasaidizi wake wengine, watendaji wa Serikali nao wanafanya kazi nzuri, tumeanza vizuri. Sisi kule Dar es Salaam katika Jimbo langu la Ukonga, Mkurugenzi wetu Jumanne Shauri na watendaji wenzake wanatupa ushirikiano. Ingawa hatuwezi kuacaha kusema wako watendaji ambao inabidi wabadilike kuendana na kasi ya Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi sina taabu na wewe na ninaamini Wabunge wenzangu hawana shida na wewe, tunafahamu kasi yako. Tumeona juzi hapa Mawaziri walivyokuwa wanajibu maswali ukisimamia Serikali kutoa majibu yanayoendana na shida za wananchi. Niwaombe Wabunge wenzangu, sisi tuna kazi kubwa ya kusaidia Mheshimiwa Rais kufikia malengo haya ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge hawa wamefanya kazi kubwa ya kampeni. Ukiingia hapa asubuhi Wabunge wengi wakiweka sura zao zile mashine zinakataa, siyo kwamba

mashine ni mbovu ila sura walizokuja nazo hapa Novemba siyo sura walizonazo leo. *(Makofi/Kicheko)*

Tumefanya kazi kubwa, Waheshimiwa Wabunge wengine hapa wameosha vyombo, wengine wamepaka rangi kucha, tunayoyasema hapa ndiyo *reflection* ya matatizo ya wananchi wetu kule tunakotoka, tunaomba tusikilizwe na Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tuseme, na wasiposikia tuwafokee. Tufoke kwa niaba ya wananchi tunaowawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kuwa mmoja wa watu tuliokuwa tunaishauri Serikali kuanzisha *TARURA*. *TARURA* imekuja kuondoa matatizo ya urasimu ule wa kihalmashauri wa ujenzi wa barabara, ilikuja kuleta tija kwenye utendaji wa kihandisi, lakini matokeo yake, tulianza vizuri na mameneja wa *TARURA* wa wilaya, akawa kuna *coordinator* wa mkoa, leo kumetengenezwa Meneja wa Mkoa, Mhandisi wa *TARURA* yule Meneja wa Wilaya amegeuka kuwa karani. Hana fedha, hatafuti zabuni, hamlipi mkandarasi, nimshukuru Mheshimiwa Jafo ameanza kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Tulileta jambo lile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa neema na rehema zote, niwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Ludewa na chama changu Chama Cha Mapinduzi (CCM). Nimshukuru pia Mheshimiwa Rais na Serikali yake yote kwa

kazi nzuri ambazo zimekuwa zikifanyika na sisi kule Ludewa tumekuwa tukizona. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ludewa kwa kuniadini na kunituma nje niseme hapa Bungeni kwa niaba yao na vilevile sisi Wanaludewa tumezisoma vizuri hotuba zote za Mheshimiwa Rais na tukajitahidi kuzitafsiri ziendane na mazingira yetu ya Jimbo la Ludewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitaanza na eneo la uwekezaji kwenye miradi mikubwa ambayo inaweza ikaongeza mapato ya Taifa letu. Mwaka 1996 Baraza la Mawaziri kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 06/96 wa mwaka 1996 waliridhia miradi ya Mchuchuma na Liganga iweze kuanzishwa na viwanda vikubwa vijenge kule. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, NDC kwa maelekezo ya Serikali na Baraza la Mawaziri waliunda Kampuni ya ubia *Tanzania-China International Mineral Resources Limited*. Kampuni hii ilikwenda Ludewa na kufanya uthamini kwa nia ya kuwekeza kwenye huu mradi wa Mchuchuma na Liganga, baada ya kufanya upembuzi yakinifu na kujiridhisha eneo lile lina mali za kutosha.

Upande wa Liganga kuna chuma ambapo kampuni hii ingeweza kuzalisha zaidi ya tani milioni 2.9 kwa mwaka na kwa makaa ya mawe wangeweza kuzalisha tani milioni tatu kwa mwaka na ajira za moja kwa moja milioni sita na laki nne na ajira zisizo za moja kwa moja milioni 33. Lakini cha kushangaza ni kwamba mradi huu umekwama.

Mheshimiwa Spika, Wabunge watangulizi wangu wamejitahidi kupambana miradi ianze, lakini hatujaweza kufanikiwa. Wananchi wa Ludewa wana imani na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli na wanamwalika sana aweze kwenda kutembelea miradi hii mapema iwezekanavyo kwani Wabunge wengi hapa wamekuwa wakilalamika fedha *TARURA*. Mimi nikuhakikishie Serikali ikiamua kuwekeza kwenye miradi ile tutapata fedha

nyingi ambayo itatatua changamoto ya fedha na changamoto ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile upo mradi wa Chuo cha VETA ambao ulianzishwa pale Shaurimoyo ambao nao umekwama kwa muda mrefu sana. Tulikwenda kufanya ziara Desemba na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na ninamshukuru Rais kwa kutuletea Mkuu wa Mkoa mahiri, *Engioneer* Marwa Rubirya, tulikwenda naye, watu wa VETA waliahidi Januari wangeweza kuanza kujenga chuo kile, lakini cha kushangaza bado hakijafanikiwa. Kwa hiyo, tunaomba chuo kile kijengwe ili miradi hii inavyoanza na sisi wananchi wa Ludewa na Wananjombe tuweze kupata ajira kwenye miradi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye Sekta ya Maji; namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji, nilipata nafasi nikateta naye, akanihakikishia kwamba mambo yatakwenda vizuri. Pale Ludewa kuna mradi ulitengewa shilingi bilioni saba, lakini kwa miaka mitatu zimeletwa milioni 180 tu, kwa hiyo pana mkwamo mkubwa. Tarafa ya Masasi ina changamoto kubwa ya maji, pale Lupingu walitengeneza mradi wa maji ila umesombwa na maji kwa hiyo kuna changamoto.

Na vilevile pale Kiogo kuna wanafunzi huwa wanakwenda kuchota maji kwenye Mto Ruhuhu kwa hiyo wanaliwa sana na mamba. Manda Sekondari kuna changamoto kubwa ya maji na wataalam wamejitahidi kufanya upembuzi yakinifu Kata ya Mawengi na maeneo mengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Latifa Juakali. Mheshimiwa Kiruswa hayupo; Mheshimiwa Latifa; hayupo, naendelea. Na asiyekuwepo sitamtaja tena. Harakisha Mheshimiwa Latifa, muda.

**MHE. LATIFA KHAMISI JUAKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na wenzangu kwa kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunjalia kuwa hai, lakini pia kutujalia sote kuwa wazima.

Mheshimiwa Spika, kwa upekee sana naomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi ambacho kinaongozwa na jemedari wetu, jembe, mpambanaji, mtu mahiri sana, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa imani kubwa ambayo wamenionesha mimi kijana wao wa Chama Cha Mapinduzi kurejeshwa jina langu na kuja kuwawakilisha vijana wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana vijana wenzangu wote wa Tanzania nzima, tukianza na vijana wa Mkoa wangu wa Kusini Unguja na vijana wenzangu wote kwa imani ambayo wamenionesha, naomba niwaahidi kupitia kwenye Bunge lako hili tukufu kwamba sitawaangusha, nipo kwa niaba yao na nitafanya kazi kwa niaba yao. *(Makofi)*

Mwisho naomba niwashukuru wazazi wangu walezi kwa kunilea, kunitunza na kunifanya mpaka leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dakika zenyewe ni chache, naomba na mimi niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo iliwasilishwa hapa katika Bunge lililopita. Sote ni mashahidi, kazi ambayo imefanywa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kubwa na sote tunaijua na



Watanzania wote waijua, mwenye macho tunasema haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimetembea katika Tanzania nzima, nimeona miradi mbalimbali iliyofanywa chini ya usimamizi wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vituo vya afya, miradi ya maji, miundombinu, barabara, hakuna asiyejua kazi kubwa ambayo imefanyika chini ya usimamizi wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nichangie katika suala hili la elimu. Wachangiaji waliopita wamesema sana; elimu yetu ya Tanzania haimuandai kijana kuweza kujajiri mwenyewe ama kuajirika. Naomba sana niishauri Wizara yetu ya Elimu sasa tuweze kubadilisha mitaala ambayo itaweza kumsaidia kijana wetu aweze kuajirika, lakini hiyo mitaala atakayoweza kumsaidia kijana huyu yeye anapomaliza elimu yake ikiwa elimu ya sekondari lakini hata katika elimu ya chuo kikuu aweze kuajirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba sana Wizara yetu ya Elimu tuandae mitaala ambayo itakuwa inaendana na wakati. Sisi vijana tuna msemo wetu tunasema lazima tuwe *up to dated*. Kwa mfano sasa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tupo katika uchumi wa kati, kwa hiyo je, sisi Wizara tunajipangaje kuendana na kasi ya uchumi huu wa kati. Kwa hiyo, lazima tuandae mitaala ambayo inaendana na uchumi.

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri katika suala hili la mikopo, wenzetu wengi waliopita wamechangia kuwa lengo la mkopo ni kuwasaidia vijana wetu na kama lengo la mkopo ni kuwasaidia vijana wetu sasa ni vyema Bodi yetu ya Mikopo ikapunguza hii asilimia 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu asilimia kubwa ya wanaopata mikopo ni vijana maskini wenzetu. Kwa hiyo, kama ni vijana maskini, leo kijana huyu amekopa mkopo *let's say* milioni 10 ama milioni 15, lakini kijana huyu pengine

anakaa miaka mitatu hajaajiriwa, baada ya kuajiriwa pengine mshahara wake ni mdogo, pengine analipwa shilingi 300,000, hiyo hiyo shilingi 300,000 Bodi ya Mikopo kuna asilimia 15 ambayo inahitaji. Je, pengine analipwa shilingi 300,000 maana yake ukiwa unalipwa shilingi 300,000 Bodi ya Mikopo wanakata shilingi 45,000 kwa hiyo shilingi 300,000 toa shilingi 45,000 kuna kiasi kidogo ambacho kinabakia, bado hapa hujakatwa *tax* na vitu vingine; je hapa bado tutakuwa tumeendelea kuwa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. LATIFA KHAMISI JUAKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, muda hauko upande wako. Mheshimiwa Latifa kama mnamkumbuka Waheshimiwa Wabunge alikimbiza mwenge mwaka juzi ule kwa ushujaa mkubwa sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Asna Sharifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Mheshimiwa Asna Sharifu.

**MHE. ASYA SHARIFU OMAR:** Mheshimiwa Spika, ni Asya Sharifu.

**SPIKA:** Majina yalivyoandikwa hapa, basi endeela.

**MHE. ASYA SHARIFU OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kipekee nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi ambacho kimeniamini na kikanipa nafasi na mimi nikawa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba niwashukuru Wajumbe Wanawake wa UWT wa Mkoa wa Kaskazini Pemba

wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi ambao nao walinipa imani ya kuweza kufika katika Bunge lako hili tukufu la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upekee naomba nichangie hoja ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mimi binafsi nikiwa Mbunge wa Bunge hili tukufu ambaye natokea Mkoa wa Kaskazini Pemba nasema hoja ile ya Mheshimiwa Rais ambayo ameiwasilisha katika Bunge hili naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kisiwa cha Pemba kwa mara hii wameonesha umahiri na wameandika historia katika kisiwa chetu. Hii ni kutokana na utekelezaji wa Ilani ambao ulionesha imani kubwa kwa wananchi na Watanzania kwa ujumla wakiwemo wananchi wa Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Tume ya Uchaguzi, Tume hii ilifanya kazi nzuri ambayo wananchi wale waliweza kutumia haki yao ya demokrasia kwa uwazi na uhuru bila kulazimishwa wala kuonewa. Vyombo vya habari, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuvishukuru, vilifanya kazi nzuri sana bila upendeleo. Hii ni kuonekana kwamba nchi yetu ina amani, utulivu na mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ya Bunge hili tukufu, niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano mkubwa ambao umetujengea uwezo sisi Wabunge kushirikiana na Bunge letu hili na kuunganisha Watanzania wote bila ubaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wengi tunajishughulisha na shughuli za kilimo na uvuvi. Lakini ni juzi tu kupitia Muungano huu tuliokuwa nao Serikali imeweza kusaini suala zima la uwekezaji wa utalii.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu Kisiwa chetu cha Zanzibar kinajishughulisha sana na masuala ya utalii, ni

imani yangu kwamba wanufaika wakubwa tutakuwa sisi wanawake na vijana, kama ulivyosema Bunge hili huwezi kuliita ni Bunge la vijana au ni Bunge la wazee. Sasa sisi kule Pemba, wanaume hao kutokana na mambo ya dini, tunaolewa, tunakuwa na wake wenza wanne au watano. Sasa fursa hizi za Serikali... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, samahani ni wanne. Kwa sababu fursa za Serikali zimeweza kutoa suala la ujasiriamali na kweli lazima tuseme ukweli wanawake wajane tuko wengi sana. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba Serikali itaendelea kutusaidia katika kuona nyanja hizi za uchumi ambazo zitawezesha wanawake kupata ajira.

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. ASYA SHARIFU OMAR:** Mheshimiwa Spika, haiwezekani wanawake wote waajiriwe kwenye Serikali, ni lazima na ajira binafsi ziwepo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa imani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Huyu ni Mheshimiwa Asya Sharifu kutoka Pemba. Msalimie sana Mheshimiwa Faida Bakar huko utakaporudi. Karibu sana Mheshimiwa Asya Sharifu. Hao wajane huko waje Bara, kuna Wanyamwezi huku. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hotuba ya Rais. Kabla sijaendelea naomba nimshukuru Mungu kwamba amenipa maisha na amenisaidia kuwa mzima mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeangalia katika hotuba ya Rais ukurasa wa 10, alijikita kuzungumzia mambo ya viwanda. Viwanda ndivyo vinavyotoa ajira kwa vijana na ndivyo vinavyoongeza pato kwa Taifa. Ni kweli kwamba kuna kipindi

tulibinafsisha viwanda na kwenye ukurasa huo Mheshimiwa Rais alizungumzia kusuasua kwa viwanda vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi vilinunuliwa na watu wakabadilisha matumizi, siyo kama vile kusudio lilivyokuwa. Sisi katika Mkoa wetu wa Mbeya, Kiwanda cha Zana za Kilimo (ZZK) leo hii ukienda unakuta mtu amekodisha ghala za kuhifadhiya pombe kwa ajili ya kuuza kwa bei ya jumla. Nafikiri ni wakati sasa Serikali ifuatilie kwa wale watu ambao walibinafsishwa na wakasema wataendeleza kile kilichokuwa kikiendelea wakabadilisha matumizi, ninaomba Serikali isimamie hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika viwanda watu wengi wanataka kuwekeza, lakini unapotaka kuanzisha viwanda, kodi zinakuwa nyingi, lakini pia ufuatiliaji wa kodi hizo, unaenda madirisha mengi; unaenda *TRA*, unaenda sijui kwa watu wa viwango na vitu kama hivyo. Nashauri Serikali iweke dirisha moja ili watu waende kwa wakati mmoja, wafanye vitu vyote mahali pamoja.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi sana hapa nchini vingeeendelezwa vingeweza kusaidia ajira ya vijana. Kwa mfano, hapa Tanzania tuna zao la ngozi. Kwa bajeti ya mwaka jana wauzaji wa ngozi nje ya nchi wamepoteza takribani milioni 200 kwa kukosesha kwenda kuuza ngozi kwa sababu ziliharibika. Ninaomba urasimu katika kusaidia wafanyabiashara ya ngozi nje ya nchi, upunguzwe ili tuweze kuona vijana wetu wakipata ajira katika viwanda hivi. Maana ni zaidi ya vijana 400 ambao walikosa ajira mwaka 2020 baada ya ngozi hizi kushindwa kusafirishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rungwe kuna *Kiwira Coal Mining* ambayo ilibinafsishwa. Iliajiri wanawake wengi na vijana wengi, lakini mpaka leo imekuwa gofu. Hata hilo wazo la kwanza la Baba wa Taifa kuona inafaa kwa Taifa letu la Tanzania, ndoto za Wanakiwira pamoja na Wanambeya zimeishia hapo baada ya kufunga migodi kama ile.

Mheshimiwa Spika, nasema viwanda bila kilimo haiwezekani. Watu zaidi ya asilimia 75 ni wakulima. Ili uweze kupata malighafi ni lazima uwekeze kwenye kilimo. Leo hii tunalalamika habari ya pembejeo. Mheshimiwa mmoja amesema hapa, tunategemea mvua. Ni wakati sasa wa kubadilisha kilimo chetu, ni wakati wa kuona kilimo ni uti wa mgongo kama mbiu ya zamani ilivyokuwa inasema. Tuanzishe umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2019/2020 tulipitisha hapa Bungeni takribani shilingi bilioni 37 kwa ajili ya umwagiliaji. Hata hivyo, ni shilingi bilioni nne tu zilitoka kwenye Wizara ya Kilimo. Ninashauri, Bunge linapopitisha bajeti, ni vyema Serikali ikajikita kusaidia ili iweze kupeleka maendeleo kwa watu wetu na hasa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kilimo bila utafiti haiwezekani. Ili uwe na kilimo bora, lazima uwekeze kwenye asasi au taasisi za utafiti. Tuna Uyole pale Mbeya, ni Kituo cha Utafiti. Huu ni mwaka wa tatu sasa hawajapata fedha kwa ajili ya utafiti. Pana mitamba pale, ili uweze kujua mbegu bora ni lazima wasomi wetu *SUA* na sehemu nyingine wafanye utafiti. Naiomba Serikali iwekeze kwenye utafiti ili tuweze kupata mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, *TARURA*, watu wengi wamezungumzia habari ya *TARURA*, zamani ilikuwa kwenye Halmashauri. Labda kwa kusema leo, jana nilimsikia Mheshimiwa Jafo akizungumza, vitu vingi vimerudi kwenye Halmashauri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii. Pia nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehemu ambaye amenijalia kibali kusimama mahali hapa. Vilevile nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa heshima na imani ambayo walinipa. Pia nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Momba kwa kuniamini na kunituma mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niendeleo kuwashukuru sana wazazi wangu kwa kunilea na ushirikiano mkubwa ambao walinipa kipindi cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia 101. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais huyu na kusema kwamba ni miongoni mwa viumbe ambao wamemkopesha Mungu kwa kiasi kikubwa sana. Maandiko matakatifu yanasema kwamba anayemsaidia mnyonge na maskini anakuwa amemkopesha Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika kipindi chake cha miaka mitano amefanya mambo mengi ambayo amewagusa wanyonge na maskini wengi sana na watu ambao walikuwa hawana watu wa kuwasemea, yeye amekuwa ni msemaji wao. Kwa hiyo, ninaamini hata katika vipindi vyake vigumu ambavyo atapatia, Mungu atazikumbuka na kuzitakabali hizo sadaka zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ni kwa sababu ya muda, nilitamani kuchangia kwa kirefu kuhusiana na eneo la biashara. Kwenye eneo la biashara nitaenda kuongelea zaidi kwenye masuala ya mipaka. Sehemu nyingi ambazo ni za *border* kumeonekana kuwa na mwamko mzuri sana wa biashara. Nikitolea mfano kwa *border* ya Namanga na Tunduma, ni sehemu ambazo zina wafanyakazi ambao wamesoma na kuajiriwa wachache sana kuliko

wafanyabiashara wanaokuwepo pale. Hivyo, inapelekea kuwepo kwa maendeleo mbalimbali ya kijamii, pia hata vijana na watu mbalimbali kuendelea kupata riziki na watu wengi kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 26 nataka ku-*quote* kipengele kidogo tu kwa sehemu, Mheshimiwa Rais anasema hivi; "...na kwa bahati nzuri tangu mwaka jana tumeanza kutekeleza mpango wetu wa kuboresha mazingira ya biashara nchini, yaani *blueprint for regulatory reforms to improve the business environment in Tanzania.*"

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi, nitolee mfano wa mpaka wa Zambia na Tanzania ambapo kidogo angalau nimekuwepo kwa hizi nchi za Kusini mwa Afrika na Afrika ya Kati. Naomba kuishauri Serikali na kuiomba, kama mawazo haya yanaweza yakawa chanya na yakasikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweze ku-*expand* mipaka yake. Pamoja na kuipongeza kwamba imepiga hatua sana katika kujenga hizi *One Stop Border*, mfano *border* ya Namanga na Tunduma, zimejengwa katika kipindi cha miaka mitano, lakini ipo hasara kubwa sana ambayo Serikali inapata kwenye hii mipaka. Bado biashara nyingi ambazo ni haramu, biashara za magendo, kutoroshwa kwa mazao vinaendelea kufanyika kwenye hii mipaka kiasi kwamba kama Serikali ingeamua ku-*expand* ile mipaka tungeweza kuzuia biashara haramu nyingi na biashara nyingi za magendo ambazo zinafanyika kwenye hii mipaka, ikasababisha Taifa likaendelea kukusanya fedha ya kutosha ambayo itaendelea kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nikitolea mfano mpaka wa Zambia na Tanzania, ndiyo mpaka ambao unabeba karibu nchi zote ambazo ziko Kusini mwa Afrika. Mfano, tunapongelea mji mmoja wa Livingstone pale Zambia, ndiyo mji ambao unapokea mpaka wa Botswana, Namibia na Zimbabwe. Kwa hiyo, nitolee mfano labda bidhaa za magendo zinapotaka kupitia lile jengo la *SADC* zinapitaje?



Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa kwenye Jimbo langu na hapa ninaiomba Serikali ikiwapendeza tupewe geti. Kwenye mfano huu naeleza, unapotoka pale Livingstone, kwenye zile nchi tatu, tuchukulie amekuja na biashara za magendo, anataka kukwepa kodi ya Serikali... *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Condester Michael Sichalwe. Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, utafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii nikushukuru wewe, lakini kipekee sana namshukuru Mwenyezi Mungu na nimshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote ni mashahidi kwamba wakati Mheshimiwa Dkt. Magufuli anaingia, nchi yetu ilikuwa inakusanya mapato machache sana. Hivi sasa tuna uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi trilioni mbili kwa mwezi. Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya maombi yetu yote ambayo tunayatoa hapa ya maji, elimu na barabara hayawezi kutokea iwapo hatutamuunga mkono Rais katika kusimamia ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge wenzangu, tutakapofika Bunge la Bajeti, tuweke mikakati ya kuisaidia Serikali ili tuwezekuongoze mapato, ili haya mahitaji ya Watanzania ambayo wote tuna azma kubwa ya kuitimiliza, yaweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Rais, lakini pia nampongeza kwa kuja na *approach* ya kuanzisha Mamlaka ya Maji yaani *RUWASA*. Sisi sote ni mashahidi, kabla hatujaanzisha Wakala wa *RUWASA*, maji na upatikanaji wa maji katika vijiji vyetu ilikuwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki, tuna mradi mmoja mkubwa wa shilingi bilioni 11 wa Kitinku/Lusilile. Huu mradi una-*cover* vijiji 11 na tayari tumeshapata takribani shilingi bilioni mbili. Mbali ya kwamba tumeanzisha hizi Wakala, bado nina ushauri kwa Wizara ya Maji. Ushauri wa kwanza ni kwamba nadhani tusiwe na utitiri wa miradi ya maji. Tujitathmini kwa miradi ambayo tumeianzisha, tutengeneze *acceleration plan*, kwamba kwa kipindi gani tutamalizia ile miradi ambayo tayari tumeshaianzisha.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ni mtu wa matokeo, anataka kuona matokeo kwa kitu alichokianzisha. Kwa hiyo, naishauri sana Wizara ya Maji, kwa miradi ambayo tumeianzisha, tusikimbilie kuanzisha mradi mpya, tutengeneze *acceleration plan* ya lini tutamalizia ile miradi, halafu tuangalie ni jinsi gani tunaweza ku-*scale up* hii *approach* ambayo tumeanza nayo kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba Wizara ya Maji iongeze wigo wa *financing* ya Mfuko wa Maji. Kutegemea chanzo kimoja ku-*finance* miradi ya maji, bado naona tunaipa mzigo sana Serikali. Naomba wakati Bunge la Bajeti likifika Wabunge tuangalie jinsi gani tutaisaidia Wizara ya Maji, tuje na *options* mbalimbali za kupanua wigo wa kuongeza *financing mechanism* ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, suala la *TARURA*, vilevile namuunga mkono Rais hasa kwa kuanzisha Wakala wa Barabara (*TARURA*). Sote ni mashahidi, kulikuwa na tatizo kubwa sana la ujenzi wa barabara za *TARURA*, lakini wachangiaji wengi wameelezea suala la kuongeza na kubadilisha *allocation formula* ya 70 kwa 30.

Mheshimiwa Spika, nina hoja mbili; hoja ya kwanza, nadhani tatizo ni ile *fixed approach*, kwa sababu tunatumia 70 kama ilivyo na 30 kama ilivyo. Nashauri tuwe *flexible*. Mahitaji ya utengenezaji wa barabara yanategemeana na *demand* ya mwaka huo. Kuna kipindi *demand* ya barabara ya vijijini ni kubwa kuliko *demand* ya barabara za mjini

ambazo zinasimamiwa na *TANROADS*. Nashauri sasa kwamba inapofika kipindi ambacho tunahitaji kupeleka bajeti *TARURA* na *TANROADS*, basi mfuko wa barabara usikilize mawazo ya *TARURA* na *TANROADS*, wa-*present* waone kwamba je, kweli *TARURA* wanahitaji asilimia 30 au wanahitaji zaidi ya asilimia 30? Hiyo ndiyo hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, lingine nashauri kwamba, tuna-*depend* sana kwenye chanzo kimoja cha ku-*finance* *TARURA*. Tuna-*depend* sana kwenye *fuel levy*, ambacho nadhani kimelemewa. Nashauri Bunge lako tukufu tutafute *options* nyingine za ku-*finance* *TARURA*. Badala ya kusema tuongeze asilimia 30, nadhani kuna haja sasa ya kuhakikisha tunaongeza wigo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Zungu, utafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema; nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi na wananchi wa Jimbo la Ilala kwa kunirudisha tena kuwa mtumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais ametoa hotuba kubwa sana. Ameshatoa *vision* ya nchi, kazi kubwa sasa ya wasaidizi wa Rais pamoja na Bunge ni kuweka *road map* ya utekelezaji wa mambo aliyoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake aliyoitoa kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili, ametoa maelekezo ya kupunguza au kufuta kodi za kero katika utalii. Utalii unaleta fedha nyingi sana Tanzania. Sasa hivi kutokana na *Covid 19*, watalii wengi ambao walikuwa wanakuja Tanzania, mishahara yao na mapato yao kwenye nchi walizotoka, nazo zimeathirika kutokana na kutokuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, waanze kufanyia kazi kuona ni kodi zipi za kero wanaweza kuzipunguza. Nataka nijue na niulize Serikali, je, watalii hao wanaokuja nchini mwetu, mamlaka zinazohusika au Wizara zinazohusika wanayo *data* ya watalii wanaokuja Tanzania kwa maana ya anuani zao, majina yao na nchi zao ili kuweza kuwafuatilia, kuwasalimia kwenye siku za sikukuu au siku zao za kuzaliwa ili kuweka kama undugu wao na Tanzania ili waweze kuwa na hamu ya kurudi?

Mheshimiwa Spika, taarifa zinasema watalii hawarudi Tanzania. Je, tumejua kwa nini watalii hawarudi? Kama kodi ni kubwa, kama kuna kodi za kero na Rais ameshatoa maono yake, basi wataalam wetu wajitahidi kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kafanya mapinduzi makubwa sana kwenye mapato ya mawasiliano nchini mwetu, makubwa sana. Miaka ya nyuma Serikali ilikuwa haiwezi kuingia kwenye *network cooperating center* za *vendors* wa simu kwa sababu walikuwa hawana uwezo huo na Serikali ilikuwa haina *appetite* na makampuni hayo yalikuwa yanafanya *self assessment* kwenye kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, leo Serikali hii ya Dkt. Magufuli inaweza kujua *every revenue user* kwa kila mteja wa simu, kwa maana kodi sasa zinaku-*cessed* kitaalam na Mamlaka za Mapato. Ndiyo maana mapato ya kodi ya simu yamekuwa makubwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili na ninamshukuru kwa kuanzisha Wizara hii nzuri na imepata Waziri mzuri ambaye anachapa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa kwenye shamba la mkonge. Miaka 60 mkonge ulikuwa unazalishwa Tanzania tani 130,000; Watanzania walikuwa 6,000,000. Leo tunazalisha mkonge tani 30,000 na Watanzania tuko milioni 60. Lazima Serikali ije na *affirmative action* ya kunyanyua mkonge, kunyanyua mazao ya mawese ili Taifa liweze kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kuwe na programu ya kuwafanya vijana kupenda kilimo. Tuwe na machinga duka na tuwe na machinga kilimo. Kuna siku zitakuja, walimaji sasa hivi wana umri mkubwa sana. Itakuja kuwa na hatari Tanzania itakosa walimaji kwa sababu vijana wengi hawana programu au mapenzi na kilimo. Serikali ije na programu; Ethiopia wamefanya, wamechukua vijana zaidi ya 15,000, wamewaingiza kwenye programu na sasa vijana wengi wanajua umuhimu wa kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa mchango wako ndani ya muda. Sasa ni Mheshimiwa Asia Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Najma Giga na Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika katika Bunge lako hili tukufu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kupata kura za kutosha na za kihistoria ambazo toka tumeingia katika chaguzi za vyama vingi uchaguzi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameshinda kwa kishindi, ninampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kukishukuru Chama chetu Cha Mapinduzi pamoja na jumuiya zake zote kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya wakati wote na

hatimaye tumekwenda kwenye uchaguzi na Chama Cha Mapinduzi tukashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bila kusahau Jumuiya ya Umoja wa Vijana kwa kuhakikisha kuwa inalinda na kutetea itikadi ya Chama Cha Mapinduzi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nina mengi ya kuchangia lakini kulingana na dakika tano ninaomba niende kwa haraka. Niende kuwasemea vijana ambao wametoka juzi JKT. Vijana takribani 10,000 ambao wamepata mafunzo mbalimbali ya kijeshi na ya kuweza kuzalisha na kutengeneza uchumi katika Taifa letu. Vijana hawa wamekwenda kukaa kwa miaka mitatu Jeshini pamoja na kupata mafunzo, vijana hawa wamerudi mtaani hawana ajira na wote tunafahamu JKT haiwezi kuajiri vijana hawa wote.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kuona sasa ni namna gani tunaweza kuwasaidia vijana hawa wakawezeshwa. Mfano, tuna Kambi ya Makutupora ambayo inazalisha zabibu, tuone vijana hawa wanaotoka katika kambi hii na tayari wana mafunzo ya kutosha wanawezeshwa ili na wao waweze kulima zabibu kwa sababu wana ujuzi huo na ikiwezekana Makutupora ipokee zao hilo kutoka kwa vijana hawa na kuwezesha nchi yetu kufikia sasa kile kilimo ambacho ni nia na dhahiri ya Mheshimiwa Rais kupitia hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tunao mfano wa Kambi zingine, tuna kambi ya Kigoma kule ambayo inalima mchikichi, tuna kambi ya Ruvu. Wote hawa vijana wana mafunzo ya kutosha, tuone sasa Serikali kwa namna gani inawawezesha kiuchumi ili vijana hawa kwa miaka hiyo mitatu na sasa hivi wako mtaani, hawana mitaji hawajui pa kwenda, hawana chochote. Tunazalisha bomu lingine katika nchi yetu bila kujua utatuzi wa vijana hawa wanapotoka makambini wanakuja kufanya nini huku uraiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa nia njema ya kuwasaidia vijana kwa kutoa mikopo kwa vijana,

akina mama na watu wenye uhitaji maalum mikopo ya asilimia 10. Tuombe sasa Serikali ifike ichukue hatua ya kuona mbali zaidi kwa kuwakopesha vijana mmoja mmoja na ikiwezekana Serikali kupitia Halmashauri ijifunze namna gani Bodi ya Mikopo inavyoweza kuwakopesha vijana na kila mwaka kurudisha fedha hizo na basi vijana hawa mmoja mmoja waweze kuaminika na kukopeshwa na Serikali kwa kijana mmoja mmoja badala ya vijana kwa makundi. Ni kweli, njia ya vikundi ni njia sahihi lakini sio vijana wote wanaoweza kupitia makundi kwa sababu hawalingani mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusemea suala la mkopo Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Ilani yake, lakini pia hotuba ya Mheshimiwa Rais lengo ni jema, yote yaliyoandikwa kama dhamira hii tutaichukua, viongozi wa Serikali tukaenda kutekeleza na kusimamia...

*(Hapa kengele illia kuasiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia zaidi ya 1,000. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Najma Giga nilishakutaja, Mheshimiwa Aida ajjandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yote ambayo ametujaalia lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa tena kwa kura nyingi kama ambavyo wametangulia kusema wenzangu na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika pamoja na Wabunge wote ambao tumebarikiwa kurudi tena kwa awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi pia nimshukuru kiongozi wangu wa Umoja wa Wazazi na timu yake yote pamoja na Chama Cha Mapinduzi kwa kuniamini kwa mara nyingine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais imejimwaga katika maeneo mengi ambayo ndiyo mwelekeo na dira ya miaka mitayo iliyopo. Pia mwisho wa hotuba yake aliwaelekeza Mawaziri ambao atawateua ambao tayari wako mbele yangu hapa kwamba warudi wakaisome Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa maeneo ambayo yeye hakuweza kuyafafanua kwa siku ile. Kwa hiyo na mimi nitaenda moja kwa moja katika eneo ambalo hakulifafanua siku hiyo ambalo liko kwenye ukurasa wa 144 hadi 145 ambayo inahusu ustawi wa jamii kwenye suala zima la ustawi wa Watoto na familia.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu bado ina changamoto katika suala hili, lakini nitumie fursa hii kushukuru sana wote waliopanga timu hii ya Ilani iliyotengeneza kwa kuweza kufafanua vifungu ambavyo sasa vitatuelekeza tunaondokana vipi na mporomoko wa maadili unaosababisha kuondoa furaha na amani ya watoto wetu, ndoa zetu ndani ya nyumba zetu na mambo yote yawe yameelekezwa hapo kuanzia kifungu (a) mpaka (n) vya Ilani katika ukurasa huo wa 144 na 145.

Kwa hiyo, nitaomba sana waheshimiwa Mawaziri kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliomba kwamba mfanye kazi hiyo kupitia ilani mimi nitakuwa na ninyi sambamba katika miaka mitano hii kuhakikisha kwamba vile vifungu vyote ambavyo vimeelekezwa kwenye ilani tunavishughulikia ipasavyo. Kama ni kutunga sheria, kama ni kurekebisha sheria, kama ni kutoa elimu kwa jamii basi nitawahamasisha na Wabunge wenzangu tuhakikishe tunakwenda Tanzania nzima kuhakikisha kwamba suala la mporomoko wa maadili ambao unasababisha matatizo mengi mojawapo likiwa ni mimba za utotoni tunalitokomeza Tanzania. Lakini pia, suala la talaka za hovyoo nchi yetu imezidi jamani Waheshimiwa Wabunge! Tunashindwa kudumisha ndoa zetu na badala yake tunasababisha kutelekezwa kwa familia zetu na watoto wetu ambao mwisho wa siku ndiyo wanaenda kupata mimba za utotoni. Kwa hiyo, hilo ni janga ambalo kama hatukuliandea vizuri na tukalitilia mkazo basi haya maendeleo



ambayo tuanzungumzia huko baadae tutakuja kukosa maendeleo mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sio hilo tu, kuna suala zima la kuwarudisha nyuma watoto wa kike katika kutafuta elimu. Bado ni changamoto katika nchi yetu. Kwa hiyo nitashirikiana na Wabunge wenzangu, lakini pia kuna suala zima la udhalilishaji wa watoto wadogo. Hili jamani mara hii litakuja kwa mwendo mpya. Ninaomba Mheshimiwa Dorothy Gwajima ajiandae kwa hilo. Mimi sitakubali kwa sababu tunashindwa kabisa ni nini tufanye jinsi ambavyo watoto wetu wanaharibiwa katika nchi yetu hii. Hilo ni jambo la kusikitisha, tumelizungumza miaka mingi, lakini safari hii naomba kutokana na haya yaliyoandikwa kwenye Ilani yetu kwenye vifungu hivi 14 nina hakika kabisa kama tutavisimamia ipasavyo na tutaisimamia ipasavyo Serikali katika vifungu hivi vilivyoainishwa kwenye Ilani kumlinda mtoto katika nchi yetu naamini kabisa miaka mitano hii tutafika mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo tu. Naipongeza kabisa hotuba ya Mheshimiwa Rais na naomba tushirikiane kuitekeleza ambavyo ameelekeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijaalia uzima kufikia siku ya leo, lakini niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Nkasi Kaskazini kwa kuniamini na leo niko ndani ya Bunge kuwasilisha mawazo waliyonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulingana na dakika tano nitazungumza kwa uchache sana. Siku alipokuja Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge nilikuwepo hapa na leo tunazungumzia hotuba yake ambayo ni mwelekeo kwa Taifa letu. Ukitazama nchi yetu ya Tanzania kila kanda ina vitu ambavyo vipo vinaweza vikasaidia Taifa. Kanda yetu ya Nyanda za Juu

Kusini na kwenye hotuba Mheshimiwa Rais amezungumzia zaidi kujikita kwenye kilimo. Nyanda za Juu Kusini tunajishughulisha na kilimo. Lakini pamoja na kilimo hicho ni namna gani kinanufaisha Taifa kwa ujumla. Ukizungumzia Nyanda za juu Kusini unazungumzia miko a mitano ambayo inazalisha chakula na mazao ya biashara lakini sisi tumebahatika pia kupya bandari ya Kabwe, bandari ile ingetumika vizuri kulingana na mazao yanayozalishwa kwenye Nyanda za Juu Kusini sio tu kusaidia Nyanda za Juu Kusini, ingesaidia pia Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kupitia bandari ile ambayo tayari Taifa limewekeza fedha nyingi tunategemea kupata matokeo ambayo yatakuwa ni matokeo chanya yatawasaidia wananchi wanaozunguka eneo lile la bandari lakini pia yatasaidia Taifa. Ili tuweze kusafirisha mazao ambayo tunaamini tunaweza tukapeleka nchi za jirani ambao wanaweza kutumia bandari yetu ya Kabwe ni lazima kiwe ni kilimo chenye tija. Wakati nazungumzia kilimo kwenye Nyanda za Juu Kusini tayari Serikali imeweka fedha nyingi kwenye miradi ya umwagiliaji, lakini ni miradi mingapi inafanya kazi mpaka leo? Unaitazama dhana ya Serikali kuwekeza fedha lakini namna gani tunakwenda kumalizia hizo fedha au viporo ambavyo tayari tumekwisha vianzisha?

Mheshimiwa Spika, wakati nazungumzia kilimo si kuwasaidia tu wakulima, lakini ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais naye amekiri kwamba ajira zinazopatikana kwa mwaka haziendani na uhitimu wa wanafunzi kulingana na *level* mbalimbali. Tunaamini kilimo ndiyo ingekuwa muarobaini wa kuweza kumaliza jambo hilo. Kilimo tunachozungumzia hatuzungumzii kilimo cha mazoea. Kama tumeanzisha miradi ya umwagiliaji wanakwenda kuazalisha nini? Je, wanachozalisha watauza wapi? Mheshimiwa Rais baada ya kuzungumza ndani ya Bunge ni kazi ya Mawaziri sasa. Kwa mfano, natambua kwamba janga la *Corona* limepita dunia nzima hatufurahishwi nalo, lakini sisi tumebahatika wananchi wetu wameendelea kulima wamezalisha kwa wingi. Mpaka sasa tunatumiaje fursa hiyo

kuweza kuwasaidia wananchi wetu ambao ni wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumza hapa pia tayari Serikali imewekeza fedha kwenye vyuo mbalimbali na hapa mimi nategemea TAMISEMI na Wizara ya Elimu hii asilimia nne ya kwenda kuwasaidia vijana hawa ambao wamemaliza *level* mbalimbali hawana ajira haisaidii sana, haileti yale matokeo ambayo tulikusudia. Leo hivi vyuo vya VETA wanakuwa wameshapata ujuzi. Kwa nini pale wanapokaribia kuhitimu wasipewe fedha kwa ajili ya mikopo na fedha hiyo ni rahisi kurudisha tofauti na sasa ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wanamaliza wanakwenda kukaa tu mtaani. Kwa hiyo inakuwa haina utofauti na wale ambao wametoka shuleni hawajafundishwa namna ya kujijajiri. Lakini hawa tayari wameshapewa ni namna gani wanaweza kujijajiri. Kwa hiyo tunaweza tukatumia ile fedha badala ya kuwapa kiasi kidogo tukaangalia wahitimu ni kiasi gani watapewa fedha hizo waweze kusaidia na wale mataajiri watu wengine kupitia mafunzo ambayo wameyapata na itakuwa na maana Zaidi juu ya kwenda kuwa *empower* vijana pamoja na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tukirudi kwenye kilimo hapo hapo hivi Vyuo vya Utafiti vikiwezesha kikamilifu watu watakuwa na uhakika wa kulimo wanachokilima. Watakuwa na uhakika wa mbegu zinazotoka kwa sababu tayari zimefanyiwa utafiti. Lakini leo hata ukiangalia maeneo ambayo watu wanalima, mtu anaamua kwamba yule alipata gunia 10 na mimi leo nitalima gunia 10. Hapana, tuambieni aina ya udongo huu mnaweza kulima zao fulani. Mkituambia pia tutajua soko la zao hilo liko wapi. Kwa hiyo, hata mtu anapoingia kwenye kilimo havezi tena kufikiri ajira. Leo tutakwenda kuwafundisha vijana namna bora ni namna gani wanaweza kujijajiri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mheshimiwa Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema. Si kwa ujanja wetu bali ni kwa huruma na rehema yake. Nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Singida kwa kumchagua Mheshimiwa Rais kwa kura nyingi za kishindo, Madiwani na Wabunge wa CCM. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwashukuru sana wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Singida ambao wamenipa fursa ya kuwakilisha katika Bunge letu tukufu. Ninawashukuru sana ninakiri kwamba ninalo deni kubwa kwao la kuwakilisha na pia kamwe sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kwa kuwa Spika wa viwango, mwenye kujali maslahi ya Wabunge wake na ambaye umeleta mapinduzi makubwa sana ya kidijitali katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo imetoa dira na mwelekeo wapi Tanzania mpya tunatakiwa kuwa katika miaka mitano ijayo. Ni hotuba iliyogusa sekta zote muhimu katika kukuza uchumi, ni hotuba iliyogusa maslahi mapana ya wanyonge. Ni hotuba inayokwenda kutofautisha Tanzania na nchi nyingine za Afrika katika suala zima la kukuza uchumi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiisoma hotuba hii ya Mheshimiwa Rais utatambua kwamba Mheshimiwa Rais anayo dhamira ya dhati ya kujenga Tanzania mpya ya kuifikisha uchumi wa juu kabisa. Ukurasa wa 10 wa kitabu cha Mheshimiwa Rais ameahidi kuongeza juhudi za kuwapa mikopo isiyo na riba au yenye riba nafuu. Pia ameagiza mifuko na programu mbalimbali ambazo zitasaidia uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi kuunganishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili limewafurahisha sana wananchi na vijana wa Mkoa wa Singida na wameniangiza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi huo na kwa kuwa asilimia 10 zinazotolewa katika Halmashauri zetu hazikidhi mahitaji ya wananchi wetu. Niiombe sana Serikali iharakishe mchakato wa kuunganisha mifuko hiyo ili wale bodaboda wangu, mama na baba lishe na wajasiriamali wadogo wadogo waweze kunufaika na mifuko hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia makundi haya utaona kwamba ni makundi ambayo hayana dhamana ya kukopa kwenye benki zetu, hivyo uwepo wa mfuko huo utawasaidia sana wananchi wale wa kipato cha chini kuweza kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Awa,u ya Tano kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maji lakini nikiri kwamba bado kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji safi na salama hususan maeneo ya vijijini. Mfano, katika mkoa wangu wa Singida upo mradi mkubwa wa Kitinku - Lusilile. Mradi huu umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu bila ya kukamilika. Niiombe sana Serikali katika bajeti ya mwaka ujao itenge fedha za kutosha ili miradi ile ambayo hajakamilika ikiwemo huu Mradi wa Kitinku – Lusilile uweze kukamilika na wannachi waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu katika suala zima la kilimo ambapo katika hotuba ya Mheshimiwa Rais...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota. Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika hadhira hii ningeanza kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataalah*, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein ambaye kwa kweli amenilea na kunikuza na kuniadini kunipa Idara ya Misitu kuweza kuiendesha kwa miaka karibu minne ambayo ndiyo imenijenga na kuwa mtu wa namna hii hapa nilipo.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kumshukuru mama yangu Bi. Jira binti Machano na mke wangu Shufaa binti Suleiman Hamad pamoja na wanangu bila kusahau wanachama wa Chama Cha Mapinduzi na wannachi wa Jimbo la Donge ambao wamenipa imani kubwa ambayo imenisababisha mimi leo kusimama hapa nikiwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja niende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais na nianzie ukurasa namba tisa ambapo Mheshimiwa Rais ameipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kuendesha uchaguzi katika hali nzuri, lakini pia kutoa matokeo haraka na kuipongeza kwa kuweza kubana matumizi kwenye bajeti ambayo walikuwa wametengewa ya shilingi bilioni 331 na kutumia shilingi za Kitanzania bilioni 262.

Mheshimiwa Spika, hapa nilikuwa napenda kutoa angalizo maalum kwamba aliyepaswa kushukuriwa zaidi hapa ni Mheshimiwa Rais mwenyewe pamoja na Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa sababu viongozi hawa wameweka

alama katika uchaguzi wa mara hii kwa sababu ni mara ya kwanza Tanzania imeweza kuendesha uchaguzi kwa kutegemea fedha za ndani tofauti na miaka yote iliyopita. Kwa kweli tunawashukuru sana viongozi wawili hawa kwa sababu wameweka alama.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ningependa kwenda kwenye *page number* 13 ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuelezea kwamba, atazieni tunu za Taifa letu ambazo zinajumuisha amani, uhuru, mshikamano, umoja, Muungano pamoja na Mapinduzi ya Zanzibar. Pia ameendelea kwa kusema kwamba, atashirikiana na Rais Dkt. Mwinyi kuweza kuhakikisha kwamba tunu hizi zinalindwa kwa gharama zozote zile.

Mheshimiwa Spika, hapa ningetoa pia angalizo kwa sababu kuna watu wanapenda kuchezea Muungano wetu na halikadhalika nafikiri juzi mnakumbuka kwamba kuna kiongozi mmoja wa kisiasa amejaribu kuzungumza kumzungumzia kiongozi mkuu wa Serikali kwamba, ana maradhi na lengo lake sote tulikuwa tunalifahamu kwamba ilikuwa ni kuleta mshtuko miongoni mwa jamii ambayo hivi sasa kama tunavyofahamu uchumi wetu umeanza kuwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule tulikotoka ndege zilikuwa hazionekani, watalii walikuwa hawaonekani, lakini hivi sasa tumeanza kuimarika, kwa hiyo, nafikiri bado ambao hawapendi mshikamano na umoja wa nchi yetu, Muungano una dumu, basi wanatafuta kila aina ya visingizio kuweza kutumia fursa kuweza kuleta chokochoko. Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa angalizo hili kwamba atashirikiana na Dkt. Mwinyi kuweza kuhakikisha kwamba analinda tunu hizi za Taifa kwa gharama yoyote.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kumalizia kwa kuhusu maliasili na utalii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud. Nimeshamtaja Mheshimiwa Abdallah Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shaban Taya na Mheshimiwa Miraji Mtaturu ajjandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kukutana katika Bunge hili la Kumi na Mbili, lakini kipekee nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi na wananchi wa Jimbo la Nanyamba kwa imani yao kwa kunirejesha tena kwa mara ya pili, nawashukuruni sana. Na niwaahidi Wana Nanyamba kwamba nina nguvu na nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuhakikisha changamoto za Nanyamba tunapata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ina mambo mengi na imetoa maelekezo mengi katika sekta mbalimbali na mimi nitajikita katika sekta mbili, ya kilimo na miundombinu na nianze na sekta ya kilimo. Hotuba imeelezea vizuri kwamba kilimo chetu sasa kinataka kuwa cha kibiashara, lakini Mheshimiwa Rais ametoa ahadi ya upatikanaji wa pembejeo na viuatilifu kwa wakulima tena kwa wakati sahihi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, sisi Wana-Mtwara zao kuu la uchumi ni zao la korosho. Niiombe Serikali sasa kuwe na mkakati maalum wa kuhakikisha pembejeo ambazo zinatumika kwenye zao la korosho zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu, lakini sio hivyo tu tuhakikishe kwamba zao la korosho tunapanua soko lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna minada ambayo inaendelea, lakini tuna *TMX*, *TMX* sasa hivi wanashiriki wanunuzi wale wale ambao wanaingia minadani. Hebu *TMX* iwezeshe ili tuwapate wanunuzi wakubwa kutoka Vietnam,



China na maeneo mengine wasi-*bid* wale wanunuzi ambao tunawaona kwenye minada. Tuwe na tofauti kwenye *TMX* tuwaone wale wanunuzi wakubwa na huku kwenye minada tuone wale wa kawaida ambao tunakuwanao. (*Makofi*)

Vilevile niombe Serikali sasa ielekeze kwenye kuwawezesha wabanguaji wadogo tuongeze thamani korosho badala ya kuuza korosho ghafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, naomba niipongeze *TARURA* kwa kazi nzuri ambayo imefanya na ambayo inaendelea kuifanya, lakini kama walivyosema Wabunge wenzangu kuna changamoto ya kibajeti. Naomba Serikali itafute chanzo kingine cha fedha ili kuiongezea fedha *TARURA* ili iendeleo kufanya kazi nzuri ambayo inaendelea kuzifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, miundombinu kwa upande wetu wa Kusini tuna barabara yetu ya Ulinzi inatoka Mtwara mpaka Newala, Tunduru hadi Songea. Nivipongeze vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri ambayo vinaifanya katika mpaka huu wetu wa Kusini, mpaka wa Mto Ruvuma, lakini kwa changamoto ya usalama kwa nchi za jirani sasa barabara hii naomba ijengwe kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara kwenda Newala, Tunduru mpaka Mbinga na maeneo ya Songea. Barabara hii ni muhimu na ni muhimu kwa ulinzi na usalama wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu vilevile kuna changamoto ya Bandari yetu ya Mtwara. Naibu Waziri hapa asubuhi amejibu kwamba kuna uwekezaji wa bilioni 157 zimepelekwa pale na kuna changamoto ya meli kwenda Mtwara, lakini sababu kubwa ni kwa sababu ya zao moja tu la korosho. Mimi naomba Serikali itoe kiwango maalum cha tozo kwa meli zinazolingia Mtwara ili kuvutia wamiliki wa meli wapeleke meli nyingi kwa wakati huu kwa sababu ukiifanya Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara kuwa na *rate* sawa watu hawawezi kupeleka meli Bandari yetu ya Mtwara. Kwa hiyo, naomba sana kuwe na kiwango maalum ili kuwavutia wasafirishaji waleti meli Mtwara.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na changamoto ya maji. Niiombe Serikali sasa kwamba kwa changamoto ya maji kwa maeneo ya Mtwara tutumie maji ya Mto Ruvuma kujenga miradi mikubwa ya maji.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba. Nilitaka kukwambia tu kwamba sasa zao la korosho kuanzia Katavi kuja mpaka Singida mpaka Dodoma katika miaka mitatu, minne, mitano ijayo Kusini hamtaongelea, mtakuwa daraja la pili, kwa hiyo, fungeni mkanda. Mtapitwa sasa hivi msipoangalia. *(Makofi/Kicheko)*

Ahsante, nilishakutaja Mheshimiwa Hadija Shabani Taya maarufu Keisha.

**MHE. HADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Ikiwa leo ni siku ya kwanza nazungumza katika Bunge lako hili tukufu naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu sana, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu amenijalia mimi kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais na chama chake, Chama Cha Mapinduzi, Wajumbe wa Baraza wa Dodoma hii Mkoa, Wajumbe wa Baraza wa Taifa, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Ndugu Heri James na Umoja wa Vijana na Wazazi wote ahsante sana, muda hautoshi kushukuru wote, lakini naomba niishukuru familia yangu sana kwa *support* kubwa ambayo wamenionesha mpaka sasa kufikia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa leo ni siku saratani duniani, mimi kama mtu mwenye ualbino nimeomba niongee leo ili

niwaambie umma kwamba Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri sana kwa watu wenye ulemavu au watu wenye ualbino, amefanya kazi nzuri sana. Amenunua mashine ambazo zinasaidia kuondoa tatizo la saratani. Hizi mashine ziko saba katika mikoa ya Singida, Iringa, Mara, Lindi, Zanzibar na kwingineko, lakini naomba nimuombe Mheshimiwa Rais kwa huruma yake, kwa uwezo wake, kwa kupenda kwake wanyonge, aongeze hizi mashine zitapakae mikoa yote kwa sababu hizi mashine mimi ni shuhuda wa hizi mashine. Nilikuwa na alama hapa shingoni kwangu ambayo ingeweza kunisababishia kupata saratani, hii mashine imenisaidia mimi kupona leo hii ninavyozungumza hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba Serikali yako tukufu, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, naomba kwa sababu ni sikivu sana, iongeze idadi ya *lotions* kwa watu wenye ualbino. Hizi *lotions* zinatusaidia sana kuondoa tatizo la kupata mionzi ya jua, hili tatizo ambalo linatufanya sisi tusiishi kwa amani tupate saratani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natamani kila Mbunge aliyekuwepo hapa aende *Ocean Road* aone jinsi gani saratani ya ngozi inavyotumaliza na namna gani saratani ya ngozi inavyotuu. Na hata *life span* yetu ni miaka 35. Hapa nipo nina miaka 33 naingia miaka 34 tarehe 7 Februari, keshokutwa nashukuru Mungu kwa sababu familia yangu imeweza kunitunza na labda pia wamekuwa na uwezo kwa muda mrefu kunipa haya mafuta, lakini si kila familia ina uwezo wa kupata haya mafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na yote haya naomba nimshukuru Rais mara ya mwisho kabisa. Nimwambie Mheshimiwa Rais ahsante sana kwa miaka mitano aliyoingia yeye ameondoa lile janga kubwa lililokuwa linaumiza Watanzania, lililokuwa linawaumiza na kuwaliza, lilimliza Waziri wetu Mkuu katika Bunge hili tukufu, janga la kuwauwa watu wenye ualbino. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, imani ile potofu imeondoka na sasa hivi tunaishi kwa raha, tunaishi kwa amani, tunajidai.

Ahsante sana Mheshimiwa Rais, lakini naomba nikwambie tena umejali sana watu wenye ulemavu, sasa hivi kila shule inajengwa kwa kuzingatia mazingira mazuri kwa watu wenye ulemavu kupita, lakini Mheshimiwa Rais pia nakuomba uboreshe mazingira ya vyoo kwa ajili ya afya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niunge hoja, naungana na hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimepata taabu kukatiza Mheshimiwa Keisha.

**MHE. HADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, basi naomba niendeleo.

**SPIKA:** Hapana, basi tena. Siku nyingine nitakufikiria leo muda umebana kidogo. *(Kicheko)*

Jamani Mheshimiwa Keisha, Hadija Shabani Taya ni dada wa watoto watatu na ana wa kwake, kwa hiyo, Waheshimiwa. Tunaendelea, nimeshamtaja Mheshimiwa Miraji Mtaturu. Mheshimiwa Miraji.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kuniona na kuweza kuniweka kwenye orodha hii. Kwa hakika ni bahati ya pekee kwa sababu ya muda, lakini nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara ya kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunijalia afya na uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Singida Mashariki pamoja na chama changu, Chama Cha Mapinduzi chini ya Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunituwa na kugombea ubunge na hatimaye wananchi wa Singida Mashariki walinichagua kwa kura nyingi za kishindo. Niwahakikishie uongozi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu na maneno machache kwa maana ya kwamba, kiongozi wetu, Rais wetu ametoa hotuba nzuri ambayo imetoa muelekeo wa miaka mitano ijayo Tanzania tunayoitaka na hii imeanza toka mwaka 2016 alivyoingia hapa alionyesha dira na kwa miaka mitano tumeona mambo makubwa yaliyofanywa katika nchi hii na kwa hakika ni historia ambayo haitafutika. Lazima sisi kama Watanzania tujivunie viongozi wa aina hii na tuendeleo kuwapa moyo na kuwauunga mkono kwa sababu Tanzania yetu imepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ambavyo unajua miundombinu ipo ili iweze kuwezesha Watanzania au wananchi kuweza kuleta maendeleo. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, ni vizuri kama Watanzania tuendeleo kuunga mkono juhudi hizi na kwa hakika kwa miaka mitano ijayo tumeona dira yake kwa hiyo, ombi langu tu nilikuwa nataka nieleze maneno machache kwenye eneo la elimu.

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto kwenye maeneo ya miundombinu ya elimu. Niombe sana Serikali kupitia Rais alivyoeleza tuendeleo kuongeza nguvu ya kuleta fedha kwa ajili ya kuimarisha vyumba vya madarasa, kuimarisha mambo ya maabara, kuimarisha suala la mabweni kwa ajili ya watoto, hasa watoto wa kike. Watoto wa kike wengi wanapoteza ndoto zao za kusoma kwa sababu mazingira ni magumu katika shule zetu za kata ambazo wanatembea karibu kilometa zaidi ya tisa kufuata shule hizo. Kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini nieleze hili suala ambalo wenzangu wote wamesema, suala la miundombinu ya barabara. Ninaamini kabisa *TANROADS* inafanya kazi nzuri kwa sababu imewezeshwa, lakini tulivyoamua kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (*TARURA*), lengo lilikuwa ni kuondoa urasimu uliokuwepo wa kuleta fedha kupitia Mfuko wa Barabara. Leo hii tunavyoleta mgawanyo wa asilimia 70 kwa *TANROADS* na asilimia 30 kwa barabara za *TARURA* ni kama vile tunaifanya taasisi isifanye kazi yake,

inakuwa haina maana ya kuianzisha *TARURA* kama hatuipi fedha.

Mheshimiwa Spika, leo hii tuna barabara nyingi sana kwenye vijiji vyetu ambazo zinaenda kuboresha kilimo. Niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja basi aeleze mipango ya kuiongezea *TARURA* fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara za vijijini ambazo zinaleta huduma mbalimbali ikiwemo elimu, afya, zahanati nyingi ziko vijijini. Tusipokuwa na barabara nzuri maana yake hatuwezi kuwahudumia wananchi ambao wako maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nieleze maneno machache sana. Mheshimiwa Rais alikiri mbele ya Bunge kwamba ataboresha demokrasia, lakini utawala bora. Kwa miaka mitano tumeona kazi nzuri iliyofanyika ikiwemo kusimamia watumishi wa umma ambao walikuwa hawafanyi vizuri sana katika maeneo yetu. Watumishi wa umma wengi walikuwa wengine hawawatendei haki Watanzania na tumekuwa wengi tunalalamika hapa.

Mheshimiwa Spika, leo hii Mheshimiwa Rais amesimama amesema, lakini sisi wote ni mashahidi, leo hii kuna baadhi wanasimama hapa wanasema hakuna demokrasia, lakini utawala bora hakuna. Niwaulize wao wenyewe hivi leo wanataka turudi tulikotoka ambapo Watanzania wengi walikuwa wanalalamika baadhi ya watumishi ambao hawafanyi vizuri katika maeneo fulani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana kama chama cha siasa wajibu wako wewe ni kuhakikisha unahudumia wananchi, lazima utatue kero zao. Wenzetu hawa wanaongea...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa sababu ya muda naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Mheshimiwa Angelina Malembeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabula.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa tarehe 13 Novemba, 2020.

Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kurudi tena katika jengo hili. Pia nakishukuru Chama change Cha Mapinduzi, Jumia ya UWT, wapiga kura wangu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na wote kwa namna moja au nyingine walioshiriki kunifikisha katika jengo hili, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi pia kwa Mheshimiwa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mama Samia na Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa. Pongezi hizi hazitatimia kama sitaweza kutoa pongezi kwa Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi pamoja na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba zote mbili nilizisikia na nilizisoma kwenye vitabu. Nitachangia kwa machache nikianza kwanza kwa kuungana na wenzangu kuunga mkono asilimia mia moja hotuba hii. Pia niseme kwamba wengi wanatuambia tunapenda sana kupongeza, niseme tu tunapongeza kwa sababu vya kupongeza vipo, kama hakuna vya kupongeza hatutapongeza, tunaendelea kupongeza kwa sababu vya kupongeza vipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa tatu na wa nne ameelezea juu ya Tume ya Uchaguzi ilivyofanya vizuri. Mimi naunga mkono na niwapongee sana, kitendo alichokifanya ni sawasawa na mtende kuota jangwani, kati ya shilingi bilioni

331 wameweza kutumia shilingi bilioni 262 na kubakiza shilingi bilioni 69 hayo ni maajabu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiruswa umevunja utaratibu, umepita kati yangu na mzungumzaji, kwa hiyo, rudi ulikotoka. Kwa Wabunge wageni Mbunge yeyote anayeongea unaacha *line* yake na Spika huruhusiwi kuikatiza. Endelea Angelina Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitunziwe muda wangu. Ninaendelea kusema kwamba naipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kutumia shilingi bilioni 262 kati ya shilingi bilioni 331 na kubakiza shilingi bilioni 69, nimesema hayo ni maajabu ya mtende kuota jangwani. Hii imeonesha uadilifu mkubwa kwa watumishi wa umma na imeonesha jinsi gani nidhamu sasa ilivyotapakaa, ninaomba hali hii iendelee katika siku zijazo tuisifie sasa halafu baadae mambo yakawa yamebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa saba Mheshimiwa Rais alielezea jinsi gani ambavyo atatoa ushirikiano wa kutosha kwa Rais wa Zanzibar. Suala hilo sisi tumelifurahia sana kwa sababu wakati hata anaomba kura Zanzibar alisema nilettee Dkt. Mwinyi nitawasaidia, nitawanyanyua uchumi wa Zanzibar na sasa hivi tuko katika Zanzibar upya, uchumi mpya tunategemea haya aliyoyasema atayatekeleza na tunamuomba kila la kheri ayatekeleze ili Zanzibar ibadilike kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wake wa 11 alielezea mifuko mbalimbali na programu ambazo zimeanzishwa ili kusaidia wananchi ikiwepo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Mfuko wa Taifa wa Kuendesha Wajasiriamali, Mfuko wa Kutoa Mikopo, lakini katika mifuko hiyo hakuna mfuko wa wavuvi wadogo wadogo.

Nilikuwa ninaomba basi uanzishwe mfuko kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo waweze kukopa wao kwa riba



nafuu au mkopo usio na riba ili waweze kununua vifaa vya kisasa vya uvuvi ambavyo vitasaidia pia kuondoa uvuvi haramu katika bahari zetu na tukiangalia sasa hivi tunaingia katika uvuvi wa bahari kuu na uchumi wa *blue* ambapo tunategemea kwamba meli kubwa za kisasa zinanunuliwa ziweze kufanyakazi. (*Makofi*)

Lakini kama tutanunua meli kubwa za kisasa, lakini bado wavuvi wadogo wadogo wanaendelea kutumia mabomu kuvua bado tutakuwa hatujafanya kazi. Kwa hiyo niombe kwamba mfuko maalum uandaliwe kwaajili ya wavuvi wadogo wadogo waweze kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo uwekezaji katika sekta ya uvuvi basi wale wawekezaji wazawa nao wapunguziwe kodi ili waweze kuleta samaki wengi na wakileta samaki wengi samaki bei itashuka na kila mwananchi ataweza kula samaki na hivyo kuboresha afya zetu. Tukiwawekea kodi kubwa na meli za uvuvi zitakuwepo halafu samaki tutashindwa kununua, kwa hiyo nilikuwa naomba hilo pia liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nimeona nilizungumzie ni kuhusiana na suala la *Corona* ambalo katika ukurasa wa 32 na 33 limezungumziwa. Tumeona umuhimu wa kutumia dawa tiba au mitishamba au dawa mbadala, hili suala kwa kweli nimshukuru Mheshimiwa Rais ametupa ujasiri ametupa nguvu tunasimama hatuhangaiki, sasa hivi hata mtu tukimuona anakohoa tunajua jinsi gani ya kufanya, lakini mwanzo ilikuwa hata ukiona jirani yako anakohoa unatafuta kiti cha kuhama umkimbie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi tumepata ujasiri, tumeendelea kutumia hizo dawa lakini pia nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Jafo kwamba mzee wa nyungu tumepata nguvu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Angelina, tunakushukuru sana.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Ninaomba zile taasisi zinazoshughulika na utafiti pamoja na kutoa vibali kwaajili ya dawa hizo zifanye haraka ili dawa zisambae wananchi wapate huduma naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kumpongeza Mheshimiwa Jafo kwa kusisitiza masuala ya nyungu, mzee wa nyungu.

Nilishakutaja Mheshimiwa Kabula na atafatiwa na Mheshimiwa Deus Sangu na Mheshimiwa Dennis Londo ajiandae.

**MHE. KABULA E. SHITOBEO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na amani tele hasa kwa kunipa kibali cha kuwa katika Bunge hili lako tukufu la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Napenda kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi hasa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Rais Dkt. John Pombe Magufuli na viongozi wote wa chama bila kusahau viongozi wangu wote wa chama wa UWT Mkoa na Taifa, bila kuwasahau wapiga kura wangu wote wakinamama wa mkoa wa Mwanza, ahsanteni sana kwa kuniamini nije kuwawakilisha katika Bunge hili tukufu la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuishukuru familia yangu kwa kuwa wamenipa faraja sana kipindi cha kutafuta kura na siku zote za maisha yangu na mpaka leo niko hapa ni kwa sababu ya faraja zao, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipo hapa kwa dhati kabisa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano, nimesoma hotuba hizi zote mbili ya mwaka 2015 na 2020.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite zaidi kwenye suala la afya. Katika ukurasa wa 32 miaka mitano iliyopita (Awamu ya Tano) ya Serikali hii imefanya mengi katika afya kama kujenga vituo vya afya na kutoa huduma ya afya kwa vituo 1887, zahanati 1198, vituo vya afya 487 na Hospitali za Wilaya 99 pamoja na Hospitali za Mkoa 10 na Hospitali za Rufaa Kanda tatu. Pia imeweza kupunguza vifo vya akinamama wajawazito, miaka mitano iliyopita ilikuwa kila mwaka wakinamama 11,000 wanafariki kwa mwaka mmoja. Lakini kutoka mwaka 2015 mpaka 2020 limeweza kupungua kabisa tatizo hilo na kurudi kuwa wanawake wajawazito wanaofariki dunia ni watu 3,000 tu kutoka kwenye 11,000. Kwa hiyo napenda kuipongeza sana Serikali na Wizara ya Afya kwa ujumla kwa kujitahidi kwa jitihada zao hizo nzuri ya kumuokoa mama mjamzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali sasa iweke kipaumbele zaidi kumaliza kabisa tatizo hili kama ambavyo imeweza kupunguza tatizo kutoka wanawake 11,000 kwa mwaka kufikia wanawake 3,000 ninajua kwa jinsi spidi tuliyonayo Serikali hii ikisimamia vizuri na Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dorothy Gwajima namuamini mama huyu ni shupavu, akisimama kama yeye pia ni mwanamke ambaye ameshaingia *labor* anajua uchungu wa mama mjamzito jinsi gani anapata matatizo. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iliingalie kwa umakini kabisa jambo hili ili kumaliza kabisa vifo vya mwanamke na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niko mbele yako pia kuomba suala la pili katika hospitali zetu za wilaya za Mwanza Wilaya zote hasa Wilaya ya Ukerewe jiografia yake ya kufikika au ya kutoka kuja Mwanza kwenye Hospitali ya Rufaa ni ngumu. Mfano Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe hakuna chumba maalum au wodi maalum kwajili ya mtoto njiti. Sasa pale *complication* yoyote au mtoto akizaliwa kabla ya muda, kwa hiyo kumuokoa yule mtoto inakuwa taabu sana. Ombi langu kwa Serikali nilitaka niombe ikiwezekana kujengwe japo wodi

ambayo ya kulingana na Wilaya ile kwa ajili ya kuokoa mtoto njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabula watu mnatoa toa macho tu mtoto wa kigogo huyo. Mheshimiwa Deus Sangu tafadhali Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba zote za Mheshimiwa Rais, kwanza kabisa ikiwa mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako tukufu, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuweza kufika mahali hapa. Lakini kwa namna ya pekee wananchi wa Jimbo la Kwela kwa kuniadini kuwa Mbunge wao, naomba niwahakikishie nitawatumikia kwa nguvu zangu zote na uwezo wangu kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyowasilisha hotuba nzuri sana alipolihutubia Bunge hili la Kumi na Mbili. Kuna mambo mengi mazuri yameelezwa katika hotuba hiyo, lakini mimi kwanza nianze na sekta ya madini. Kweli tupongeze hasa alivyoitendea haki kwa miaka mitano iliyopita ambayo sasa sekta ya madini imeweza kuchangia Pato la Taifa. Kutoka mwaka 2015 ilikuwa ni 3.4% na sasa sekta ya madini inachangia Pato la Taifa kwa 5.2% ni mafanikio makubwa yanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika hotuba yake Mheshimiwa Rais aliongelea jambo kubwa sana na kuantangazia ulimwengu juu ya kuvumbua kwa gesi ya *helium* ndani ya Bonde la Ziwa Rukwa. Gesi hii inaenda kuleta mapinduzi makubwa katika uchumi wa Tanzania, lakini naomba nitoe rai na juzi nilikuwa nateta na Naibu Waziri wa Madini akanihakikishia kwamba mwezi nne zoezi la kufanya *inflation* na *drilling* inaweza ikaanza, changamoto ninayoiona

ni maandalizi. Mara nyingi tunakuwa na miradi mikubwa kama hii kwa mfano hii gesi ya *helium* wasiojuwa ni gesi yenye thamani kubwa na Tanzania tuna ujazo unaokaribia futi za ujazo bilioni 1.38 ambao tunawazidi hadi nchi ya Marekani mara mbili na ambao uchimbaji wa gesi hiyo wao mwaka huu inaelekea kufikia ukomo. Kwa hiyo sisi kama Tanzania tutakuwa tunaweza kuongoza soko hilo la dunia na kuweza kullisha dunia kwa miaka 20 ijayo na jambo hili liko kwenye Bonde la Ziwa Rukwa ndani ya Jimbo langu la Kwela kuna hekta 3,500. Maandalizi ninayosema ni kuandaa wananchi maana yake huu mradi unaweza kwenda kwao wakaupokea kama tu muujiza kwa kuwa hawakuandaliwa yakatokea mambo kama yale yaliyotokea Mtwara.

Pili, miundombinu naona bado si rafiki sana, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wewe ni shahidi siku ya mwaka mpya tulikuwa ndani ya eneo hilo ninalolisema ulijionea hali ya miundombinu ya barabara kuwa ni mibovu, sasa tuna mradi mkubwa kama huu, miundombinu ya barabara ni mibovu kiasi kile na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi mwaka juzi ulikuja kule Bonde la Ziwa Rukwa ulijionea mpaka ukaanza kuuliza kuna njia nyingine tutarudi tena tulikotoka, lakini njia ndiyo hizo hizo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, niombe tunapokuwa na mradi mkubwa tufanye maandalizi mazuri ili huu mradi uweze kuleta manufaa makubwa kwa taifa lakini kwa watu wale ambao wanaishi maeneo yanayozunguka mradi mkubwa kama huu.

Mheshimiwa Spika, pili nichukue nafasi hii kuongelea sekta ya kilimo na naomba hapa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu mnisikilize kwa makini. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais ameeleza wazi kwamba tunaagiza ngano kutoka nje karibu tani 800,000 kila mwaka, lakini nitangaze neema ndani ya Bunge lako tukufu, ndani ya Mkoa wa Rukwa tuna ekta zipatazo zaidi ya 60,000 ambazo zimefanyiwa tafiti na zinafaa kwa kilimo cha ngano. Tukiwekeza huko hakika hata hizi *shortage* ya tani 800,000 itakuwa historia. Tayari Mkoa wa Rukwa hasa katika Jimbo langu la Kwela eneo hilo lipo,

nakuomba Mheshimiwa Waziri wa kilimo na Naibu Waziri kama mtaweza yeyote atakayeweza afike huko twendeni mkajionee jambo hili na pia tuitumie Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa maana ya Benki ya Kilimo waje waweze kuwawezesha wananchi ili hii *shortage* ambayo inatokea, sisi tumeumizwa sana, tumelima kwa nguvu kubwa, mahindi tumezalisha tani nyingi, tumebaki nayo majumbani yanaoza na mwaka huu tumelima sana hatujui tutapeleka wapi walau hii ujio wa ngano hii na sisi tutapata ahueni kama mkoa na kuachana sasa tuanze kugawa tulime nusu mahindi na nusu ngano kwa sababu mahindi yametutesa, hatujui wapi kwa kupeleka na hali ni nguvu pamoja na hayo uzalishaji huu tunaofanya unategemea tu mvua, umwagiliaji miradi mingi tuliyonayo hasa kwenye Jimbo langu ime-*prove failure*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deus Sangu, tunakushukuru sana kutukaribisha Kwela huko Mheshimiwa Dennis Londo nilishakutaja, ajiandae Mheshimiwa Fakharia Shomari.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako tukufu, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye imempendeza mimi kiumbe wake kuwa sehemu ya Bunge lako hili la Kumi na Mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya kipekee nikishukuru Chama changu chini ya uongozi wake Mwenyekiti wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kunipa imani, lakini kwa namna ya kipekee pia nishukuru familia yangu na wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa imani yao juu yangu kuwakilisha katika Bunge lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako la Kumi na Moja lilifanyakazi kubwa, kazi ambayo imemsaidia Rais wetu na Serikali yetu kwenda kwenye uchumi wa kati. Jukumu la Bunge hili la Kumi na Mbili naamini ni kwenda kutoa tafsiri

chanya ya uchumi wa kati katika maisha ya Mtanzania mmoja mmoja. Hotuba ya Mheshimiwa Rais inatupa dira na mwangaza wa nini ambacho anataka kutoka kwetu, lakini pia anatuonesha ni jinsi gani tunaweza kuipeleka Tanzania katika uchumi wa viwanda ili Mtanzania mmoja mmoja aone matunda ya nchi yake kuwa katika uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili tunapoenda kuzungumzia uchumi wa kiwanda sekta ya kilimo hatuwezi kuiacha nyuma kilimo ndiyo uti wa mgongo kilimo ndiyo kila kitu. Kuna mengi ambayo naamini yako nje ya uwezo wetu ambayo Serikali bado inayafanyia kazi. Lakini kuna mengi ambayo yako ndani ya uwezo wetu naamini tukisimama pamoja tunaweza kumkomboa mkulima na mkulima akawa sehemu ya uti wa mgongo katika Tanzania ya viwanda ambayo wengi tunaitarajia na wengi tuna matumaini nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto naomba nichukue kilimo cha miwa kama mfano. Jimbo la Mikumi wakulima wa miwa katika Bonde la Kilombero wanauwezo wa kuzalisha tani 900,000 za miwa, mnunuzi ni mmoja tu kiwanda cha sukari Kilombero ambaye uwezo wake kila mwaka ni kununua tani 600,000 tu. Maana yake tunaenda kupoteza tani 300,000 kila mwaka. Hakuna namna ambayo tunaweza kuelezea zaidi ya wananchi kukosa matumaini na hujuma kuwa sehemu ya maisha ya wakazi ama wakulima wa bonde lile.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano msimu huu zaidi ya ekari 1,300 ama zaidi ya tani 30,000 za miwa zimeteketea kwa moto, hasara hii kubwa ambayo wakulima hawa wa miwa wameipata inaelezea ndwele ambayo inaelezea changamoto wakulima wanaipitia. Katika hali hii mimi naamini Tanzania haipaswi kuwa na nakisi ya sukari ama kuagiza nje sukari kama tunaweza kujiweka vizuri na kujipanga pamoja na nakisi ya sukari ambayo tunayo viwanda hivi ambavyo kazi yake ni kuzalisha sukari vimekuwa na jukumu la kuagizia sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwanza jukumu la kuagiza sukari lisiachiwe wazalishaji wa sukari, kwa kuwafanyia hivyo maana yake wanakosa *incentive* ya kuhakikisha miwa ya wakulima inaenda kusangwa katika viwanda vyao. Jukumu hili libebwe na Bodi ya Sukari ama Serikali yenyewe na viwanda hivi vijikite katika suala zima la uzalishaji wa sukari ndani. Tukifanya hivi maana yake tunaondoa *incentive* kwao. Lakini la pili miwa ya wakulima isiuzwe kwa tani za miwa, tuuze kwa *suclose*, kwa kufanya hivi mkulima anaenda kupata thamani ya zao ambalo amelitolea jasho lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiondoka hapo kwa namna ya kipekee nilikuwa naomba kuzungumzia suala zima la utalii. Tunaambiwa watalii 20 kati ya 100 ndiyo ambao wanarudi Tanzania kwa ajili ya kutalii. Tuna swali la kujuliza kwanini hawa 80 hawarudi? Wakati tunaendelea kutafakari hili naamini majibu mazuri ya Serikali yanaweza yakaboresha sekta ya utalii na kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya watalii kwa kuhoji maeneo ambayo tuna changamoto nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusiana na hii barabara ambayo inahudumia SGR...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Londo. Mheshimiwa Fakharia Shomari atafatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Juliana Masaburi ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na kukushukuru wewe pia na kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi pamoja na UWT kwa kuniwezesha leo miye kuwa bado niko Bungeni. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, kwanza nitazungumzia ujio wa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuja Zanzibar wakati wa kampeni. Amekuja Zanzibar kwa kweli tulimpokea kwa shangwe kubwa na tukakuweko pale Mnazi Mmoja tuliujaza uwanja na kwa kweli wananchi wa Zanzibar walifurahi na tunzo yao waliyoitoa kwamba majimbo yote ya Ugunja wamechukua na ngome ya Pemba tumeivunja na hadi hii leo tunakwenda kifua mbele Zanzibar, haya yote yalikuwa ni matunda ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kufika na kutuhamasisha na kutupa busara katika hotuba zake alizokuwa akituelezea pale Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 15 Mheshimiwa Rais alisema tunu ya Taifa, tunu ya Taifa kuna vitu alivitaja na hivyo na ndivyo vilivyotupa moyo sisi kule Zanzibar, ambapo alisema amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Muungano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli atakuwa karibu na atashirikiana sana na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hilo la kwa Zanzibar tumelipokea na lilikuwa jambo la tunu kwetu na tumekubali katika tunu zake alizozisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Kumi na Mbili, wakati anakuja kutuhabia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, alizungumza kwamba atashirikiana na akinamama kwa karibu na kwa kweli Mama Samia anafanya kazi nzuri na Mheshimiwa wetu na yeye ndiye aliyetupelekea akatuona kwamba wanawake tunafaa na akasema wanawake ukiwakabidhi dhamana ni watendaji wazuri na hii lazima tumpongeze kwa sababu yeye katuweka karibu, baadhi ya Mawaziri wanawake wapo na wanafanya kazi nzuri, Makatibu Wakuu wako wanafanya kazi nzuri ili kwetu sisi lazima tumlipe wema wanawake wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa nini tumeingia? Mheshimiwa alijitoa alitembea mikoa yote, na akatuletea

kura za kishindo, leo humu ndani wengi wetu UWT tunatamba na tusingeweza kutamba kama sisi yeye Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kutupatia kura nyingi tukaweza kuingia humu Bungeni, hatuna la kumshukuru isipokuwa tufanye kazi nzuri akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna lingine katika ukurasa wake wa 15 Mheshimiwa Rais alisema kwamba anampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwyni kwa kuimarisha utawala bora hususan kwa kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma na kuzidisha mapambano dhidi ya ubadhirifu, rushwa, wizi, ufnisadi na hili kwa Zanzibar ambapo yeye ameweza kuonesha njia kwa Bara na Zanzibar alivyokuwa amelizungumza hili...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia. Sasa nimuite Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Juliana ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

La kwanza kabisa ni shukrani kwa Mungu ambaye amenipa uhai, lakini la pili shukrani ziende kwa Chama changu cha Mapinduzi ambacho kimenipa nafasi ya kuchaguliwa kuwa Mbunge. Wakati huo huo nawashukuru sana wananchi wa Urambo wamenipa kura nyingi sana najivunia kura zao nawaahidi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu nisiwaangushe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naikumbuka familia yangu imenisaidia sana, nawaombea kwa Mungu nao waendeleo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umenipa nafasi hii wakati muafaka, nashukuru sana kwa sababu leo umetangaza kwamba kutakuwa na uchaguzi wa *TWPG* na nimeona ni vizuri nichukue nafasi hii kwa niaba ya wenzangu wote tuliofanya kazi ndani ya *TWPG* kumshukuru sana Mungu alitupa nafasi tukafanya kazi nyingi sana, ahsanteni sana Wabunge Wanawake mliokuwepo, ahsante sana Wabunge wanaume mliokuwepo wote tulifanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tukushukuru wewe, akinamama wenzangu Wabunge naomba na kinababa wote waliotuunga mkono tumpigie sana makofi mengi sana Mheshimiwa Spika kwa jinsi alivyotusaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema mbele ya Mwenyezi Mungu ametusaidia sana ndugu zangu tulikuwa na shughuli kubwa wa mradi ule unaoendelea wa *Bunge Girls High School*, bila wewe tusingefanikiwa jamani, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kwa niaba ya wenzangu kushukuru ofisi yako bila kumsahau Naibu Spika, Katibu wa Bunge, ofisi yake yote wafanyakazi wa Bunge walisimama mstari wa mbele chini ya uongozi wako tukafanikiwa sasa Waheshimiwa Wabunge tuna *Bunge Girls High School*, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifika ofisi kwako kukushukuru na pia nakuaga kwamba tumefanya kazi kwa karibu sana na wewe na ofisi yako na wote nakushukuru sana. Tuwatakie wenzetu mema ambao watakuwa kwenye uongozi unaokuja, lakini muwe na uhakika Spika tunaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kushukuru kwa upande wa *TWPG*, nirudi sasa kwa hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hotuba ya Mheshimiwa Rais inahitaji sana kupongezwa kwa hali ya juu, mambo mengi yamefanywa, wenzangu Wabunge mliotangulia mmeongelea mambo ya afya ambayo pia

imetugusa Urambo, mambo ya maji, umeme, mengi kwa kweli yaliyofanyika pia na sisi yametugusa Wilaya ya Urambo, cha maana tumuombee Rais wetu maisha mema na kuitakia la heri Serikali kwa kuwa kweli Mawaziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wanafanya kazi kubwa tuwaombee na kuwatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kama ifuatavyo, kwa kweli kwa sasa hivi wenzangu wameshaongea sehemu za vijijini barabara ni mbaya, tuombe Serikali yetu iongezee fedha *TARURA* kwa sababu barabara zetu zinahitaji kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa upande wa kilimo, nafahamu kabisa Mawaziri walioko na Serikali kwa ujumla wanajitahidi, lakini bado tuwaombe pembejeo zifike kwa wakati lakini pia mazao yetu yapate bei ya kutosha kwa kupata wanunuzi wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nishukuru Serikali yetu, tuna *VETA* zipo na Urambo ninayo lakini kama walivyotangulia kuongea wenzetu ziongezewe aina mbalimbali za ufundi. Nishukuru sana kuona kwenye kipindi kimoja *VETA* moja tayari inatengeneza simu hayo ndiyo mambo tunayotaka. Kwa hiyo, tunaomba kwamba *VETA* iongezewe aina mbalimbali za ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wa wafanyakazi nitakuwa sikutenda haki bila kutajia suala la wafanyakazi, kuna ukurasa hapa ambao unasema Serikali itaendelea kuwajali wafanyakazi. Naomba kwa siku ya leo wafanyakazi kwa kweli wanapopandishwa madaraja warekebishiwe mishahara kwa haraka ili isilete matatizo wanapostaafu. Nina orodha ya walimu wengi ambao wanaendelea kuomba wamestaafu, lakini mishahara yao haikurekebishiwa kwa hiyo, kutengenezewa mafao yao inakuwa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limejitokeza nashukuru kwamba Serikali yetu imeanzisha mtindo wa e-

*Government* yaani mambo ya kutumia mtandao, wasaidiwe kwa upande wa uhamisho, inawapa tabu sana wafanyakazi. Baada ya kusema hayo nampongeza Mheshimiwa Rais...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Lakini bado nakupongeza Mheshimiwa Spika kwa kutusaidia *TWPG*, Mwenyezi Mungu isaidie *TWPG*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, mama yetu Mheshimiwa Mama Margaret Sitta na shukrani kwa kutushukuru. Mheshimiwa Juliana Masaburi atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Sabu.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii name niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais alipofungua Bunge letu la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi kwa vile ni mara ya kwanza kusimama hapa kwenye Bunge lako tukufu napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa kibali kuwa mmoja wa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi, kwa kutupa nafasi za upendeleo hasa sisi mabinti vijana kuja kwenye Bunge lako kuwawakilisha vijana wote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anafungua Bunge aliongelea kuhusu ukuzaji wa uchumi, katika ukuzaji wa uchumi aligusia kuhusu Serikali kuongeza jitahada za kuwezesha wananchi wake kiuchumi, lakini pia alisema kuwapatia mikopo ambayo haina riba au yenye riba nafuu. Hii mikopo napenda kuwapongeza Serikali kwamba

Halmashauri zetu kote nchi inatoa hii mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, akinamama na walemavu, na inafanya vizuri sana kusema kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado hii mikopo haitoleta matokeo chanya kama tuvyotarajia, kwa sababu kwanza zile pesa ambazo zinatolewa na Halmashauri ni ndogo lakini pia Halmashauri au Serikali imesema kwamba mikopo hii itolewe kwa vikundi mbali za vijana, akinamama na walemavu, kwenye vikundi sio kila kijana wana *idea* ya kuwa pamoja na jinsi gani ya kufanya biashara. kwa hiyo, wanajikuta wanachukua hii mikopo baada ya kuchukua hii mikopo wanaanza kugombana kwa sababu kila mtu ana *idea* yake na kikundi kinavunjika. Vikundi vinavyovunjika pia mikopo ile iliyochukuliwa kwenye Halmashauri haiwezi kurejeshwa kwa wakati, kwa hiyo, inapelekea hii mikopo kutoonekana faida yake kubwa kwa vikundi ambavyo vinachukua mikopo na hasa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuishauri Serikali ingeangalia ni jinsi gani inaweza kumwezesha kijana mmoja mmoja kuchukua hii mikopo amesema Mbunge mwenzangu wa vijana pale Mheshimiwa Asia kwamba kijana mmoja akiji-*commit* akachukua mkopo akaaminiwa akachukua mkopo ni rahisi kurejesha kwa wakati ili kijana mwingine au watu wengine waweze kukopa zaidi. Lakini yule kijana pia ataajiri vijana wengine nyuma yake, watano au kumi atakuwa ameongeza ajira kwa vijana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali iangalie jinsi gani inamsaidia sasa kijana benki zetu nchini Tanzania hazi-*support* vijana sana. Unakuta benki wanakwambia ukienda na *business idea* wanakwambia kwamba ni lazima uwe na *collateral* au uwe na *bank statement* kuanzia miezi sita, mwaka au miaka mitatu. Sasa kijana kama mimi nimetoka kwenye chuo VETA nina ujuzi, nina kila kitu, sina hiyo *collateral*, sina hiyo *bank statement* sina *cash flow* nitawezaje kuanzisha biashara bila kuangalia mfumo mzuri wa kutu-*support* vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia benki zetu zimekuwa rahisi sana kukopesha wafanyabiashara wakubwa, sisi Wabunge na wafanyakazi wa Kiserikali, lakini vijana imeweka kwamba ni lazima wawe na *security*. Ningependa kuishauri Serikali iangalie ni jinsi gani itakaa na hizi taasisi za kifedha itaangalia ni jinsi gani inaweza kumsaidia kijana mwenye *idea* nzuri ya kibiashara iweke tu uaminifu, kijana ana *business idea* nzuri, anachokiongea anakijua, anaweza kufanya biashara imuamini imwezeshe afanye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati anafungua hili Bunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juliana Masaburi, sasa Mheshimiwa Lucy Sabu.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuunga hoja iliyoko mezani. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kunijalia kibali kuwa mahali hapa. Lakini nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniamini hususani Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiupekee sana Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais imeeleza mambo mengi ambayo yametoa dira na vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imewapa Tanzania matumaini makubwa hususan kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi. Mambo haya yote yatafanikiwa endapo sisi tulioaminiwa kuwa wawakilishi wa wananchi wenzetu tutafanya kazi kwa bidii katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijikite zaidi katika hotuba ya Mheshimiwa Rais hususan kwenye suala zima la mikopo itolewayo na Halmashauri zetu. Mikopo hii lengo la Serikali kuwaweza vijana lilikuwa ni nzuri zaidi endapo kama tutaendelea kuwajengea vijana uwezo hususan kwa kutoa elimu ya kutosha, lakini na mafunzo ya ujasiriamali. Kwa sababu kitu kinachotokea vijana wanapounda makundi wanakuwa hawana uzoefu na elimu ya kutosha hususan kwenye ujasiriamali wanakuwa hawana. Hivyo basi kama ambavyo tulivyo na miradi ya maendeleo ya kimkakati basi tulibebe na hili liwe ni fursa ya kimkakati hususan katika kuwaajiri vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali hususan kwenye hii mikopo isiwe ni sehemu muafaka sasa tuunde benki kwa ajili ya vijana ambapo hela zote ambazo zinatoka kwenye halmashauri ziingie kwenye ile benki ambayo tutaifungua lakini pia na mifuko hii ya uwezeshaji mifuko 18 ambayo ipo kwenye Ofisi ya Waziri iingie kwenye benki ambayo tutaianzisha. Nina imani kupitia kuanzisha benki hii itaweza kutoa mikopo kwa mtu mmoja tofauti na ambavyo inatolewa mikopo kwa vikundi. Kwa sababu kwenye vikundi kila mtu ana *idea* zake tofauti tofauti, unajikuta vijana hao wanashindwa kurudisha marejesho ya pesa wanazopewa Halmashauri zetu. Mwisho wa siku tunakuwa tunapoteza fedha ambazo zinakuwa ni changamoto kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile malizia hizi dakika zilizobaki.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii hapa leo. Pia nimshukuru Rais wetu kwa ushindi wa kishindo, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii ya leo kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, nimepata nafasi ya kuisoma, hotuba ni nzuri sana na inakwenda kuakisi sifa kuu za kiongozi, kiongozi sharti awe mcha Mungu, awe na maono na awe na utekelezaji wa haya ninayoyapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiisoma hotuba hii nitaangalia maneno machache, mfano ukurasa wa 26 unazungumzia viwanda, naomba nifungamanishe viwanda pamoja na miundombinu. Rais wetu ametupa sifa kuu tatu ya aina ya viwanda wanavyovitaka; moja, viwe ni viwanda ambavyo malighafi zake zinapatikana nchini; pili, viwe ni viwanda ambavyo vinatumika bidhaa zake na Watanzania walio wengi; lakini tatu, viwe ni viwanda ambavyo vinatoa ajira na alisema ikiwezekana asilimia 40 za ajira zote nchini zitokane na viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli tukiamua kujenga viwanda, kazi ambayo najua Mawaziri wetu mnaifanya vizuri sana lazima tuangalie maeneo ya kimkakati. Naomba nitazame kipekee eneo kama la kwetu pale Mufindi Kusini kuna viwanda zaidi ya tisa, kikiwemo kiwanda kikubwa cha Mgololo, barabara zake mpaka sasa hivi bado sio za lami, magari yanapita maelfu kwa kila siku na kodi tunalipa zaidi ya shilingi bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama tunataka tukuze sekta hii tunapotazama maeneo ya barabara na mikoa, barabara za wilaya za nchi, lakini maeneo kama haya ambako ndiko kuna wale ng'ombe wetu ambao kimsingi wanatoa maziwa mengi, tutaweza kusaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia kwa kazi kubwa ambayo imefanywa kwenye nishati, sote ni mashahidi vijiji vilikuwepo 2,108 vyenye umeme wakati huo leo vijiji 9,184 tulikuwa tunazalisha megawati 1308 leo tunazungumza megawati 1601. Tuna mradi mkubwa wa *Stigler's Gorge* ambao unakwenda kutuzalishia karibia megawati 2115 hii ni kazi kubwa sana ambayo amefanya Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu maeneo yaliyobaki sasa ni vema Wizara ikaweka mkakati kwa kuzingatia maeneo matatu; moja, baada ya kukamilisha vijiji vilivyobakia vile sasa twende kwenye maeneo ya taasisi iwe ni mkakati kwamba kila shule, kila zahanati, kila ofisi ya kijiji ikawe na umeme, vitongoji vilivyobakia pia vikapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda ni mdogo nigusie kidogo eneo la maji, maji ni uhai, tumeona na tumeshuhudia kipindi hicho ambacho kimsingi miaka mitano. Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli amewaza kumuvuzisha nchi kutoka kwenye asilimia 41 maji vijiji mpaka asilimia 70 sasa. *(Makofi)*

Ombi langu sasa tuongeze bajeti ikiwemo maeneo yetu ya Jimbo letu la Mufindi Kusini, ambapo kulikuwa na miradi kama ya Himayi, ilikuwa ni miradi mikubwa ili angalau tukapate maji kwa wingi zaidi. Sekta hii iongezewe maji kwa sababu kama ni wataalam inayo wazuri, Waziri wa Maji ni mzuri, mchapakazi, anakesha kwenye *site*, na tukitatu tatizo la maji Watanzania walio wengi zaidi watakuwa wameanza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ningependa kuzungumzia ajira. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo, ametueleza kwamba atakwenda kuunganisha mifuko 18 ya vijana na ndiyo ilikuwa kazi ya kwanza aliyomkabidhi Waziri wetu Mkuu akaifanye, pamoja na jambo hilo lakini naomba tukatazame kwenye mitaala yetu. Je, mitaala tuliyonayo ina *reflect* mahitaji halisi huko mtaani? Hatusemi kwamba kusoma *zinjanthropus* na sokwe sio jambo baya, lakini kama vijana wanakwenda kujiajiri kwenye kilimo, pengine kwenye ujasiriamali, kwenye biashara, hayo ndiyo masomo ya lazima kwa sababu walio wengi wanakwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutazame pia kwenye sekta ya utalii sote ni mashahidi nchi yetu hii mwaka 2015 watalii waliokuwa wanakuja nchini ni milioni 1.2 leo wako milioni 1.5 mkakati ni kupata watalii milioni tano ikifika mwaka 2025.

Tumetoka kwenye kupata dola za kigeni karibu bilioni 2.6 leo tunakaribia bilioni sita, lazima tunapofikiria kupata watalii milioni tano tutazame maeneo mengine kwa sababu leo karibu asilimia 80 ya watalii upande wa Kaskazini, hapa tuna Mbuga yetu ya Ruaha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja ilishatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, basi nawashukuruni sana kwa jinsi ambavyo tumefanya kazi asubuhi hii mpaka saa hizi, mambo haya yaendeleo mnanielewa. Kwa hiyo, jioni orodha ni kubwa sana lakini kila aliyelea jina awepo tu kwa sababu *possibility* ya kupata nafasi ya kuzungumza ni kubwa bado.

Waheshimiwa Wabunge, katika orodha ya leo sijafika hata nusu, lakini tutajitahidi sana kila mtu a-*fit* na wale wachache watakaobakia basi kesho tuweze kumaliza. Naendelea kuwashukuruni sana, tunaendelea vizuri.

Kwa hatua hii naomba nisishe shughuli hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS DKT. JOHN POMBE JOSEPH  
MAGUFULI ALIYOITOA WAKATI WA UFUNGUZI WA BUNGE LA  
KUMI NA MBILI TAREHE 13 NOVEMBA, 2020**

B

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Dkt. Kiruswa tuanzishie atafuatiwa Mheshimiwa Jackline Kainja Andrea.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ili na mimi niungane na Wabunge wenzangu katika kuchangia hii hotuba madhubuti, imara iliyojaa kila aina ya maelezo sahihi ya dira ya taifa letu kwa miaka mitano ijayo. Lakini nikiri pia kwamba baada ya kuangalia hotuba zote mbili kuna kitu kimoja ambacho Wabunge wengi hawajakiongelea mimi kimenigusa sana. Ni kwamba Rais wetu katika kupanga vipaumbele ametanguliza katika hotuba zote haja ya kuendelea kulinda na kusimamia tunu za Taifa ambazo ni amani, umoja, mshikamano pamoja na kuimarisha Muungano wetu na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi hivi vitu hasa amani imenigusa sana kwa sababu ni rahisi sana watu kuchukuwa *for granted* kitu ambacho wanacho kizuri bila kujuwa dhamani. Uki-*imagine* nchi ambazo zina vita katika dunia hii, nchi ambazo hazina, amani, umoja, mshikamano halafu sisi Watanzania tangu Uhuru tume-*enjoy* hivyo vitu na Rais alivyoji-*commit* kwamba moja ya kipaumbele chake namba moja ni kuendeleza amani ya nchi hii na umoja na mshikamano mimi nawiwa kusema kwamba tumpigie Rais makofi kwa sababu amelinda kwa dhati hayo mambo yanayohusu umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa sababu ametoa dira ya vipaumbele mbalimbali na muda huu wa dakika tano

hautoshi kupitia vyote acha nichukue ya sekta inagusa roho ya wapiga kura yangu sekta ya mifugo. Napenda kumpongeza Rais kwa sababu ameelekeza kabisa na ameona umuhimu wa sekta hii ya mifugo kwa uchumi wa nchi yetu na ndiyo maana amekusudia kuongeza hekta zinazopatikana kwa ajili ya ufugaji kutoka milioni 2.8 mpaka zifike hekta milioni sita.

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa kweli kwa jamii ya wafugaji wa nchi hii na uhakika ni faraja kubwa sana na niombe kuishauri Serikali basi kwa sababu Rais ameshaonesha dira kwamba tunahitaji kukuza sekta ya mifugo kama moja ya vyanzo vikuu vya kuongeza mapato ya nchi hii na kutuelekeza kwenye uchumi wa kati, ningepomba sera zingine za Serikali kama za uhifadhi kwa mfano basi waangalie vizuri hili suala kwa maana Rais ameshaonesha nia ya kuongeza maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa masikitiko kuna maeneo mengine ambayo Wizara zingine niki-*refer* Wizara ya Maliasili wao wako katika harakati ya kupunguza maeneo ya malisho ili waongeze maeneo ya uhifadhi na wakati kiutamaduni au sijui kiasilia mifugo na wanyamapori vinarandana. Wilaya kama Wilaya yangu ya Longido ambayo asilimia 95 ni eneo la ufugaji na ni eneo pia la wanyamapori, tangu kuanzishwa kwa dunia imekuwa hivyo na ndiyo maana walioanzisha *game controlled areas* walianzisha tu wakijuwa kwamba ni maeneo ya wafugaji, lakini kulikuwa na *proposal* ya kutaka kumegua lile eneo la Longido asilimia isiyopungua 30 kwa sababu ni vijiji 14 kuvifanya viwe ni *game reserve*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nikafikiri kwamba hiyo itakuwa inaenda kinyume na azma ya Rais ya kuongeza maeneo ya malisho, maana ukishatengeneza *game reserve* maana yake mifugo hawana nafasi na bahati mbaya sana katika eneo kama lile la Longido yale maeneo ambayo *game reserve* ingetengenezwa ndiyo yale maeneo ya kimbilio ya wafugaji wakati wa kiangazi, milima kama ya Gelai, Ketumbeine, milima ile ya ... ambayo inatokeza mpaka upande wa Namanga na maeneo ya *Lake Natron*. Kwa hiyo,

ningefikiri hiyo dhana ya *game controlled* pamoja na sheria iliyopo ambayo napendekeza pia ifanyiwe marekebisho ili mifugo na wanyamapori pale ambapo matumizi mseto yanaendelezeka yanaendeleee kuachwa hivyo hivyo maana sasa hivi *game controlled areaskwa* sheria iliyopo ndiyo watu wasiishi ndani lakini zimekuja tu sheria zimeweka wakati watu mule na maeneo ya wafugaji tu, hakuna shughuli nyingine na mimi naomba kwamba hii azma ya Rais ya kupanua maeneo ya malisho ya mifugo iendeleee kuungwa mkono asilimia mia moja kuhakikisha kwamba Wizara zingine haziingilii Wizara nyingine katika kuhakikisha kwamba maeneo haya yapo, yanahifadhiwa maana yanahifadhiwa kwa ajili ya mifugo na siyo kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hiyo nigusie eneo la kilimo, kwa kweli linahitaji nalo tuangalie namna ya kuondokana na kilimo duni cha jembe la mkono twende kwenye kilimo cha kisasa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Kiruswa dakika tano ni chache sana. Nilisha kutaja Jackline Kainja Andrea, atafuatiwa na Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. JACKLINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia Bunge lako tukufu Bunge la Kumi na Mbili. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunjialia kuwepo humu kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Napenda niweze kushukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunipa nafasi yakuwa mwakilishi

wa wanawake kutoka Tabora, pia niweze kuwashukuru akinamama wa Mkoa wa Tabora kwa kuniamini kuwa mwakilishi wao na mimi nawahahidi sitawahangusha. *(Makofi)*

Vilevile naomba nitowe shukrani zangu za dhati kwa familia yangu mume wangu mpenzi Mr. Seleman Sungi pamoja na watoto wangu watatu Tarik Seleman Sungi, Lion Seleman Sungi na Cairo Selemani Sungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo naomba name nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hotuba nzuri nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri iliyojaa matumaini kwa wananchi watanzania wote lakini niende moja kwa moja eneo la afya, niipongeze wizara ya afya kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuboresha sekta ya afya, tukiangalia miundombinu wachangiaji wa mwanzo walliona hilo na mimi pia naona nigusie hapo.

Mheshimiwa Spika, kuboresha miundombinu katika zahanati na vituo vya afya kutoka zahanati 1,198 na vituo 487; tunaona hayo ni maendeleo ndani ya miaka mitano iliyopita. Lakini vilevile niipongeze wizara ya afya na Serikali kwa kuweza kupunguza vifo vya akinamama wajawazito wakati wa kujifungua kutoka 11,000 kwa mwaka 2015 na mpaka kufikia 3,000 tunaona kwa miaka mitano tayari tumeokoa wa mama idadi 8,000 kwa mwaka. Kwa hiyo niombe Serikali kwa idadi hii iliyobaki Mungu akitujalia *Inshallah* hotuba ijayo tuweze kupata asilimia sifuri ya vifo vya akinamama wajawazito wakati wa kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naipongeza Wizara ya Afya kwa namna ambavyo wameweza kuboresha na kuweza Hospitali za Kanda za Rufaa kama Bugando, KCMC, Muhimbili, Benjamin Mkapa pamoja na *Mbeya Referral Hospital*.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali iweze kuangalia kanda ya Magharibi yenye Mikoa ya Katavi, Kigoma pamoja na Tabora. Jambo najuwa mpango upo

basi Serikali iweze kutusaidia kwa haraka ili wananchi hawa wa Kanda hii ya Magharibi waweze kunufaika na wao kutokana na adha wanaoyopata ya hospitali ya rufaa kutoka Mkoa wa Katavi aende Mwanza basi iwepo kwenye Kanda yao ya Magharibi.

Naomba niongelee suala la maji napenda niipongeze Serikali na Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumtua ndoo mwanamke wa kitandania na nimpongeze Mheshimiwa Rais tarehe 30 Januari, 2021 ameweza kuzindua Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, Mkoa wa Tabora. Lakini nilikuwa naiomba Wizara husika iweze kuangalia kwenye Wilaya na maeneo ambayo bado maji ya mradi huu wa Ziwa Victoria haujafika kama Urambo, Sikonge, Kaliua, Jimbo la Igalula ili wanawake hawa/akinamama wa Kinyamwezi waweze kupumzika na ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo naomba niunge mkono hoja naunga asilimia zote nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Jackline Kainja Andrea kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Furaha Matondo na atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Mohamed.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako tukufu ikiwa ni mara yangu ya kwanza, lakini pia nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kuwa hapa siku ya leo kwa ajili ya mchango wa hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyofanya kwa wananchi wetu wa Tanzania kwa kuonesha kwamba imani ya Tanzania inapatikana na mpaka leo hii tukiwa Bungeni tuna amani kubwa sana, lakini pia niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mwanza kwa kuniamini na kuweza kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, ninakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwa kunichaguwa na kunipa nafasi ya kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja nijikite kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba tuna haja ya Wizara hii kupata kipaumbele kikubwa ambavyo vimewapatia katika hotuba yake tumeisoma sote ni hotuba ambayo imelenga kujenga sana kwenye Kanda zetu za Ziwa na hata kwenye bahari.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kwa wale wavuvi wadogo wadogo ambao wao bado hawajatatizama vizuri, waweze kuona ni jinsi gani wanaweza kupatiwa zana za kuweza kufanya kazi ili waweze kuondokana na changamoto za uvuvi harama. *(Makofi)*

Katika Kanda ya Ziwa hasa Mkoa wa Mwanza kuna akinamama ambao ni wafanyabiashara na wanafanyabiashara ndogo ndogo, lakini akinamama wale wanaitwa akinamama wachakataji, tunaomba sasa waweze kupatiwa vitendea kazi ili waweze kupata chanja za kuanika dagaa na hata kuanika samaki ili wasiweze kuanika chini na hata samaki wale na dagaa wakawa na mchanga kitu ambacho kinawanyima soko, lakini pia hatupati afya bora kwa sababu tunakula chakula siyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kidogo niongelee suala la elimu; ninashukuru sana Serikali yetu imeweza kutoa vipaumbele kwa wanafunzi wetu ambao wanasoma bure mpaka *form six*, lakini pia wameweza kujenga majengo ya shule kila sehemu imeonekana. Niombe tu tunawanafunzi wetu watoto wa kike ambao ningeomba kila Wilaya basi angalau ipate shule ya bweni ya kuweza kuwawezesha mabinti zetu waweze kusoma wakiwa wametulia ili waweze kupata elimu bora tunapokwenda kusema hamsini kwa hamsini ili iweze kuwa *ratio* sawa na hata mabinti zetu waweze kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kidogo kuhusu suala la afya, naishukuru sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa kuona kwamba hatuwezi kuenenda bila kuwa na afya njema, hilo ninamshikuru sana. Ameweza kujenga vituo vya afya, hospitali za kanda na kila kata kuna hospitali. Lakini niombe, naomba tuweze kupata matabibu katika vituo vya afya, lakini pia tuweze kupata madaktari watakaoweza kutoa dawa za usingizi kwa sababu majengo yamejengwa, lakini ni madaktari wetu kidogo wamekuwa ni wachache basi niombe Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli iweze kuona kuna haja sasa ya kuajiri madaktari na wanaotoa dawa za usingizi ili wananchi wetu wasiweze kuhangaika kwenda kupata huduma mbali wakati huduma wameshawekewa karibu.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa sababu Serikali yetu imeona ni jinsi gani akinamama tunahangaika ikaona kuna haja ya kuweza kupata mikopo ya asilimia kumi. Sasa niombe Wizara husika iweze kusimamia ili asilimia kumi iweze kutoka kwa wakati na wanufaika waweze kupata kile walichokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Furaha Matondo, nilishakutaja Mheshimiwa Asya Mohamed na atafuatiwa na Mheshimiwa Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma mjini.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi jioni ya leo nami kuchangia hoja ya Mheshimiwa Rais ambayo alitubia siku ya uzinduzi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa pumzi na mimi leo nikasimama mbele yako ili kuweza kuchangia hayo ambayo yanakuja juu yako. Katika hotuba ya Mheshimiwa

Rais nimeipitia, amezungumza vitu vingi, lakini mimi ninaomba kurudia ukurasa wa 13 na 14 ambao Mheshimiwa Rais alisisitiza zaidi kuhusu ulinzi wa amani, umoja, kuyalinda Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, lakini vile vile suala zima la Muungano.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuzungumza kipengele kidogo kuhusiana na kero kubwa za Muungano ambazo zinakumba Taifa hili. Tangu ninapata ufahamu na kulifahamu Bunge lako tukufu na nikiwa nikilifuatilia vipindi mbalimbali nimesikia watu sana Wabunge walioipita walikuwa wakilalamika juu ya mustakabali mzima wa kero za Muungano, lakini bado kero zinaendelea na hadi sasa tunaona kwamba kuna changamoto hizi zinaweza kuondoka kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, vikao vinakaliwa mbalimbali kujadili mustakabali mzima wa kero za Muungano lakini bado kuna kero ambazo tunakutana nazo asubuhi na jioni, na niweze kutoa mfano, kwenye kero kubwa ya masuala mazima ya biashara. Wazanzibari tunafahamu kwamba tumelelewa na utamaduni mkubwa wa masuala mazima ya ufanyaji wa biashara. Suala hili kwenye kero za Muungano linaudhi sana kwa sababu ndugu zetu kutoka Tanzania Bara hawawezi kuja kununua vitu kutoka Zanzibar, wakisafirisha kufika bandarini wanadaiwa malipo (*charged*) wanaambiwa hiyo ni mali ya Wazanzibari.

Sasa tunaona hapa ni jinsi gani kunakuwa na stofahamu kati ya bande hizi mbili wakati Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amesema anasisitiza kuweka sawa suala hili nzima na kusema kwamba hatahakikisha usawa na maendeleo yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini maendeleo pia yawezi kupatikana bila kuwa na elimu, tunazona changamoto za elimu kati ya Tanzania Visiwani na Tanzania Bara kitu ambacho ukiangalia *syllabus* ya msingi wa Tanzania Bara ambao unakuwa umetengenezwa na Wizara ya Elimu ya Tanzania bara lakini *syllabus* ya elimu ya msingi kwa upande wa SMZ *syllabus* hii pia inatengenezwa maana yake iko

tofauti. Lakini *syllabus* hiyo hiyo ukienda kwenye sekondari wanatumia *syllabus* moja, lakini inapelekea kwamba bara wanasoma vitabu vyao na Tanzania Visiwani wana vitabu vyao. Hii ni changamoto kubwa kwa watoto wetu wa Kizanzibari inawapelekea sana na siku zote katika *drop failure* ya *school* huwa tunawaona watoto wa Kinzanzibari *wana-fail* sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Wizara husika inayosimamia masuala mazima ya Muungano naomba walichukue na walifanyie kazi kiukweli ni kero kubwa na inawaumiza sana Wazanzibari.

Kwa kuwa ni muda ni mchache sana naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 46 unaozungumzia *issue* nzima za utalii. Mheshimiwa Rais alituambia kwamba mwaka 2015 kulikuwa na wageni ambao wanaingia 1,137,182 lakini kutoka *gap* ya mwaka 2015 mpaka 2019 ametuambia tena kuna *gap* ya wageni ambao waliokuwa wanaingia 1,510,051.

Mheshimiwa Spika, hapo unaoiona hii *distance* ambayo inaonekana bado miaka mitano yaani *interval* ya wageni kuongezeka ndani ya Tanzania imekuwa ndogo sana. Nishauri kwa Wizara husika ambazo zinasimamia masuala ya utalii waweze kuongeza nguvu za ziada kuweza kukaribisha wageni, waweze kufika ndani ya Tanzania, lakini vilevile tuna vivutio vingi ndani ya Tanzania yetu, kitu ambacho vitu hivi havisimamiwi ipasavyo na havitengenezwi vizuri, kwa hiyo, tunakosa wageni kufika. Mimi mwenyewe nimefika katika Makumbusho ya Bagamoyo na nimekwenda, hali ilikuwa hainiridhishi. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya, dakika zako zimeshakwisha.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie...

**SPIKA:** Unga mkono hoja.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, suingi mkono hoja. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa sababu ya muda nitakwenda moja kwa moja kwenye hotuba ambayo tunajadili hapa.

Mheshimiwa Spika, nimesoma vizuri hotuba zote mbili; ya Bunge la Kumi na Moja na Bunge la Kumi na Mbili. Kusema kweli kama ukizipitia vizuri unaona dhahiri kwamba yale mambo aliyoyasema Mheshimiwa Rais katika Bunge la Kumi na Moja na utekelezaji wake katika Bunge la Kumi na Mbili unathibitisha kwamba Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ameweza kutembea katika maneno yake. Kwa hiyo, tunampongeza sana kwa kazi hiyo nzuri na kwa namna ambayo sasa nchi inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja; Watanzania wengi tunafika mahali tunasahau, zamani hata katika nchi zingine walikuwa wanasema Tanzania ni nzuri kwa kuweka mipango mizuri, ikishaweka ile mipango inatekelezwa katika nchi za wenzetu, majirani zetu. Lakini leo hao waliokuwa wanasema hivyo hiyo nafasi hawana maana wanashangaa jinsi ambavyo tunapanga mambo na jinsi ambavyo utekelezaji wake unavyokwenda. Kwa hiyo ukiangalia nchi zote, ziwe na Afrika mpaka kwa wale wenzetu wa Ulaya, wanatutamani, wanatamani Tanzania jinsi inavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo sasa ni vizuri tukaendelea tu kufanya tafakari kwamba hata huko

tuendako hivi baadae mambo haya tutaendelea ku-*maintain* hii *pace* tuliyonayo au baadae mambo yatakuja yatushinde. Nadhani hilo ni jambo ambalo huko mbeleni tunahitaji kuendelea kulitafakari katika mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo sasa mimi nitoe tu mchango katika maeneo mawili kwa sababu ya muda. Eneo la kwanza ambalo tunahitaji sasa tuliangalie katika hiki kipindi tunachoenda nacho kwa kweli tatizo la ajira kwa vijana wetu bado ni tatizo kubwa kwa sababu vijana wengi wanamaliza chuo, lakini mwisho wa yote ajira imekuwa ni tatizo.

Kwa hiyo, ninadhani ni vizuri sasa Serikali ingejiangaliza huko, itengeneze programu maalum kwa ajili ya vijana hawa wanaotoka sekondari, wanaoshindwa kuendelea, lakini na wale vijana wanaomaliza vyuo vikuu, kwamba namna gani sasa tunaweza kuwa-*accommodate* katika kupunguza hili tatizo la ajira. Kwa hiyo, hilo ni moja ya eneo ambalo tunahitaji kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, viko vitu vingine ambavyo vilevile hata sasa hivi yawezekana hatuoni *impact* yake lakini bado *impact* yake ni kubwa. Leo ukipita katika vituo vyote vya polisi, maana yake vilevile tumezungumza kwamba kati ya watu tunaohitaji kuwasaidia ni hawa waendesha bodaboda. Kuna bodaboda zaidi ya 1,000 katika kila kituo cha polisi. Sasa ukija kuzijumlisha katika nchi nzima ziko nyingi sana na ziko pale zinaoza. Na unakuta wakati mwingine bodaboda mwingine alishikwa na ile bodaboda alikuwa hana leseni akakimbia na ameshindwa kwenda kuitoa ile pikipiki.

Kwa hiyo, nadhani Serikali inahitaji iziangalie kwamba badala ya zile rasilimali kuendelea kupotelea pale, basi ni vizuri ikaangalia utaratibu mzuri wa kuunda tume au kamati fulani hivi ambayo inapita katika kila Wilaya iziangalie zile bodaboda zote zilizoko pale pamoja na makosa waliyofanya halafu waamue kwamba badala ya kufia pale ama Serikali izitaifishe au basi wale wa kurudishiwa waweze kurudishiwa

kuliko ambavyo tunaendelea kutumia fedha za kigeni kuagiza bodaboda zingine, lakini tuna bodaboda nyingi zimejaa kule kituoni. Kwa hiyo, nadhani upande huo napo Serikali inahitaji kuliangalia namna ya kulisaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ukienda kwa hawa vijana wetu wa JKT, kusema kweli mimi ule mpango niliupenda na ni mpango ambao niliufurahia kwamba wale vijana wanakaa pale JKT ile miaka mitatu baadae kati ya hao vijana wanapata ajira. Lakini wale vijana wakitumiwa vizuri, wakifundishwa vizuri elimu ya ujasiriamali, wao wenyewe wana uwezo wa kuzalisha na kile watakachokizalisha na kwa kuwa watakuwa wamepata mafunzo, basi hicho hicho bado wanaweza kupewa tena baada ya ile miaka mitatu na wakaenda kuanza maisha na tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo itawasaidia sana kuliko ile ambayo wakishatoka pale chuoni, wakishatoka JKT baada ya ile miaka mitatu halafu wengine tunawarudisha nyumbani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini. Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Askofu Gwajima ajiandae.

**MHE KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nikipongeze Chama changu cha Mapinduzi kwa uwepo wangu hapa, kikiongozwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli; lakini zaidi niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Handeni pamoja na familia yangu kwa kunifanya niwepo mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi hapa kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hotuba yenyewe ilijielekeza kutoa uelekeo wa nchi yetu kwa miaka mitano ijayo, pamoja na yote ambayo Mheshimiwa Rais anayafikiria

ni ya muhimu na ambayo yatatuvusha kama taifa kuelekea miaka mitano na pamoja na hoja zote ambazo Wabunge wamezichangia. Kimsingi ukiangalia ni kwamba mambo haya mwisho wa siku yanahitaji fedha; ili tuweze kuyafanya yanahitaji fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka nichangie ili kujaribu kuishauri Serikali ni namna gani kama nchi tutajidhatiti kuweza ku-raise hizi fedha ambazo zinahitajika kwa ajili ya kuyatekeleza mambo haya ya kutuvusha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo nataka nilishauri kwa Serikali yangu, tutakumbuka mwaka 2019 Bunge lako lilipitisha *Finance Act* yenye maboresho ya kikodi mengi sana, na moja kati ya maboresho hayo ilikuwa ni kupendekezwa kuanzishwa kwa Ofisi ya *Tax Ombudsman*, jambo ambalo mpaka leo halijafanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali yangu sikivu ianzishe ofisi hii muhimu ili kuendana na hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 12 ambapo ameelekeza kwamba lazima tuwe tunafanya *business disputes*, njia pekee ya kufikia hapo ni kuanzisha ofisi hiyo muhimu ya *Tax Ombudsman*.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka nilishauri ni *structure* yetu ya chombo chetu muhimu cha *TRA*. Yote tunayotategemea yanategemea makusanyo ya ndani yanayofanywa na ofisi hii ya *TRA*. Ninachoishauri Serikali yangu ni kwamba *TRA* isiogope kuajiri vijana kwa sababu waajiriwa wa *TRA* siyo sawa na waajiriwa wengine wa pande nyingine za idara za Serikali, hawa unaajiri watu ambao wanakwenda kuzalisha moja kwa moja, wanatusaidia kukusanya kodi. Haiwezekani eneo la kimkakati kikodi kama ilivyo ilala unakuwa bado una ofisi zenye watumishi wasiotosha, tunajichelewesha wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka nilishauri ni habari ya *informal sector*. *Informal sector* inafanya biashara kubwa sana lakini haiwi *captured* kwenye mifumo



ya kikodi. Hili ninapendekeza ufanyike utafiti mzuri na wa kutosha ili watu wetu wa *TRA* waweze kutoza kodi sehemu zote zinazozalisha ambazo ziko kwenye *informal sector*. Tusipojaribu kuli-*balance* hili litakuja kutuingiza matatizoni kwa sababu *formal sector* inayolipa kodi itakuja nayo kugeuka kuwa *informal sector*, ni lazima tufanye utafiti na tujaribu kuya-*balance* haya mawili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na makusanyo mazuri yanayofanywa na *TRA*, ninashauri tusiwe tunapima ufanisi wa *TRA* kwa kuangalia *increment* ya makusanyo yao, kwamba mwaka jana walikusanya hapa, mwaka huu wameongeza kiwango hiki, hicho si kipimo peke yake cha kuonesha ufanisi wa taasisi hii muhimu kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba *TRA* na Serikali yetu kupitia Wizara ya Fedha wawe wanaangalia *ratio* kati ya *taxes* zinazokusanywa kwa uwiano na *GDP* ya kwetu. Tusipofanya hivyo hatari yake ni kwamba tutakuwa tuna-*impose tax burden* kwa walipakodi wachache kwa sababu *increment* hiyo unaweza ukakuta ni kwa sababu ya *vertical raise* kwa kuongeza tu makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara walewale waliopo badala ya kui-*spread* ile kodi kwa uchumi wote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilishauri ni habari ya mamlaka za Kiserikali. Mamlaka zetu za Serikali zinakuwa *supplied* na wafanyabiashara, sasa wafanyabiashara wanapokuwa wame-*supply* Serikalini ukichelewa kuwalipa maana yake unajichelewesha mwenyewe kuchukua kodi yako. Ni bora hata ukafanyika utaratibu kama fedha ya kuwalipa inakuwa haijapatikana, ile *component* ambayo ina kodi ndani ilipwe kwanza halafu ndiyo waendeleo na *procedures* nyingine. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa  
Mzungumzaji)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

**MHE KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mchango wako ulikuwa mzuri sana ndiyo maana nikakumezea kidogo, sasa ujipange wiki ijayo ya mipango ushuke ufafanue vizuri zaidi maana yake utakuwa na dakika nyingi kuliko hizi. (*Makofi*)

Ni kweli tusipoangalia tutakuwa tunakuwa na *tax burden* ambayo ni kubwa zaidi kwa watu walewale, na kwa sababu *tax base* inakuwa ndogo kwa hiyo wengine hawafikiwi. Inafika mahali itafifisha hata wale ambao wanalipa sasa nao watazidiwa maana yake watafilisika, kwa hiyo, badala ya kukuza sekta binafsi tutajikuta...

Mheshimiwa Pindi Chana, kama hayupo Mheshimiwa Askofu Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa dakika chache hizi za kuchangia na mimi katika hotuba ya Rais ya kufunga Bunge na hotuba ya kufunga Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kila mara ninapomkumbuka Dkt. John Pombe Magufuli na hotuba zake na uongozi wake inanikumbusha kitabu kimoja kilichoandikwa na Dkt. John C. Maxwell. Kwenye kitabu chake anasema; ikitokea vita kati ya kundi hili na kundi lile au kati ya nchi hii na nchi ile na ikatokea kwamba jeshi moja wanajeshi wake wote ni simba na kiongozi wake ni simba na jeshi lingine wanajeshi wake wote ni kondoo na kiongozi wake ni simba, basi hizi timu mbili zikipigana kwa maana ya timu ambayo kiongozi ni simba na askari ni simba na timu ambayo kiongozi ni kondoo na askari ni simba, *definitely* timu ambayo kiongozi ni kondoo itapoteza vibaya sana. (*Makofi*)

Lakini pia Maxwell akasema kwamba; pamoja na kwamba jeshi linaweza kuwa na masimba wote ilimradi tu kiongozi ni kondoo, lazima jeshi hilo litapoteza; alikuwa anaongea kwa habari ya dhana ya uongozi, kwamba

maendeleo au ushindi ni kiongozi. Kwa bahati nzuri Tanzania tumepata kiongozi Simba na majeshi nayo ni simba na kwa hakika ushindi wetu upo kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninapokumbuka dhana ya uongozi wa kidiplomasia, ninakumbuka mambo mawili; kwenye diplomasia, uchumi wa kidiplomasia tuna mambo mawili; tuna uchumi pamoja na biashara, lakini kwenye diplomasia ya uongozi tuna mambo matatu; cha kwanza tunasema *strong power*, cha pili *soft power* na cha tatu *smart power*.

Mheshimiwa Spika, sasa *strong power* ni nini; *strong power* ni mahali ambapo kiongozi anashawishika kwamba watu wangu nikiwapeleka mpaka pale wantanufaika na maisha yao na maisha yao yatakuwa salama. Lakini watu wale ama kwa kujua au kwa kutokujua hawajui kwamba wakifika pale watakuwa salama. Sasa *strong power* maana yake ni kiongozi huyu anawakokota hawa watu wapende wasipende wakifika pale wakagundua faida zake wanamshukuru yule kiongozi wanasema ahsante kwa kutufikisha hapa, hiyo inaitwa *strong power*.

Mheshimiwa Spika, *soft power* ni kwamba unaanza kuwabembelezabembeleza, unawaeleza faida za wanakokwenda, watakokofika na mambo ambayo watayapata, unawabembelezabembeleza mpaka unawafikisha pale baadaye wanakushukuru wanasema ahsante kwa kutufikisha hapa, hiyo inaitwa *soft power*.

Mheshimiwa Spika, lakini *smart power* unaunganisha *strong power* pamoja na *soft power*; kuna wakati mwingine unawaburuza wanakwenda, kuna wakati mwingine unawabembeleza na hiyo ndiyo aina ya uongozi ambayo Dkt. John Pombe Magufuli anayo. Dkt. John Pombe Magufuli ni *smart power* na Mawaziri wetu na Waziri Mkuu pia ni *smart power*, watatufikisha tunakotakiwa kwenda kwa uhakika kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *TARURA*; hai-*make sense* ukiona kwamba mtandao wa barabara za *TARURA* ni takribani kilometa 130,000 na mtandao wa barabara za *TANROADS* ni takribani kilometa 40,000, hai-*make sense* kwa nini mpaka leo *TARURA* anapewa asilimia 30 na *TANROADS* anapewa asilimia 70; hai-*make sense*. (*Makofi*)

Nikisema hivyo sina maana kwamba nadharau ukweli wa kwamba ubora wa barabara za *TANROADS* unatakiwa kuwa imara zaidi kwa sababu una-*cut accross* mikoa kwa mikoa, lakini hai-*make sense* kwa nini huyu ambaye ana mtandao wa kilometa 130,000 apewe asilimia 30 na huyu mwenye mtandao wa kilometa 40,000 apewe mgao wa asilimia 70; hakuna mateso tuliyonayo Wabunge kama *TARURA* kukosa fedha kule mikoani, ni ngumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano kwenye Jimbo langu la Kawe. Kwenye Jimbo la Kawe Wilaya nzima ya Kinondoni tuna kilometa za barabara za ndani 1,663. Kilometa 200 ziko Jimbo la Kinondoni kwa pacha wangu Mheshimiwa Tarimba, lakini kilometa 1,463 ziko Jimbo la Kawe; kilometa 1,463, ni sawasawa na kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma lakini zote ziko ndani ya Jimbo la Kawe. Nilipowatembelea *TARURA* wana fedha za kutengeneza kilometa 120. Ina maana kuna kilometa 1,300 ambazo haziwezi kutengenezwa, *this is not acceptable* kwa wakati wowote katika nchi yetu; haikubaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kama kweli tuna ndoto ya kuwaletea watu maendeleo, siyo Jimbo la Kawe tu, lakini kwenye kila jimbo barabara zinazotakiwa kujengwa kwa kutumia *fund* ya *TARURA* hazitajengwa kabisa kama *TARURA* hataongezewa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Road Fund* kama unavyojua ni mawazo yaliyoanza mwaka 1999 mpaka 2000 nyakati zile Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa Waziri wa Ujenzi. Kuanza kuchukua shilingi 200 kwenye kila lita moja ya mafuta na kuchukua asilimia 70 kwenda *TANROADS* na asilimia 30 kwenda *TARURA*.

Ninawaomba watendaji wawaze mawazo mengine tena ya kuongezea fedha. wasitegemee mawazo yaleyale ya Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa Waziri wa Ujenzi, wawaze mawazo mengine ya kuongezea fedha. *There is nobody here who is a copy of the other, everybody is an original from the Almighty God*; lazima watendaji kazi wetu mjiongezee zaidi, muwaze zaidi, muwe *creative* zaidi kwa namna ya kumuongezea *TARURA* fedha, vinginevyo *it is a nightmare* kuwapa watu maendeleo kwa kupitia *TARURA*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna huyu mdudu anaitwa *Corona...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, dakika tano zimekwisha. (Makofi/Kicheko)

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Wazo la kwamba *TARURA* waongezewe fedha Waheshimiwa wenzetu Serikalini ni wazo limesemwa miaka mingi na kila *road board*, kila mtu anaongelea jambo hili, haiwezekani tu. Hatusemi sijui iwe ni nini na nini, lakini *TARURA* iongezewe hata iwe 40 basi, lakini lazima pafanyike *changes*. Hatuwezi kuendelea hivi. Haiwezekani. Yaani vitu viko wazi tu; lakini ukitaka mawazo hayo uyapate kutoka *TANROADS* ndio wawashauri wao kwamba wapunguziwe hela, haiwezekani hata siku moja.

Kwa hiyo, lazima tufike mahali tuliamue jambo hili, yaani *over the years*, hata mwakani mtasikia michango ni hivi hivi, hata mwaka kesho kutwa ni hivi hivi, hata mwaka unaofuata ni hivi hivi. Sasa itakuwa muda wa Bunge ni

kuongelea jambo hilo hilo moja kila siku, inakuwa kidogo kama haipendezi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni jambo la kulitazama kwenye bajeti hii inayokuja, tuangalie *whether* hiyo *formula* ilikuwa *plugged* kwenye sheria au ilikuwa wapi? Basi inahitaji iangaliwe kwa kweli. Ni kilio cha miaka mingi. Wabunge wengi wamekuwa hawarudi hapa, adhabu zao kubwa ni barabara. (*Makofi*)

Eeh, tukuchague wakati daraja letu limevunjika miaka kumi halijatengenezwa! Angalia barabara hii, Mbunge gani wewe? Wanaanguka, wanakuja wanya, wanaanguka. *TARURA!* Sasa safari hii hebu hili tulishike kama Wabunge, maana vinginevyo na ninyi hamrudi. Ninyi chekeni chekeni tu na *TARURA*. Barabara zilizo nyingi ni *TARURA*, mpaka mjini hapa Dodoma ni *TARURA*, mpaka Mwanza Mjini *TARURA* ipo, yaani yenyewe iko vijjini na mijini. Kwani Kawe ni wapi? Si ni mjini! Bado ni *TARURA*. Sasa huwezi kusema *TANROADS* yeye tu peke yake, haiwezekani. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, hii hoja kwa kweli, hela hazitoshi siku zote, lakini angalau kamgao kidogo kawepo kawepo hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud Protas. Wanyamwezi hawapo hawa! Mheshimiwa Protas wa Tabora huko huko.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais iliyotolewa mwezi Novemba, 2020 na mimi nikiwa kama Mbunge, nimesimama hapa kwenye Bunge hili tukufu kwa mara yangu ya kwanza, nianze kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetufikisha hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi ambacho kilinipigania mpaka nimeweza kuingia kwenye chombo hiki muhimu sana. Tatu, nawashukuru familia yangu, walikuwa nami bega kwa bega kupambana katika

kuhakikisha mimi nasimama imara kwa maslahi ya Wanaigalula wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa ni dira ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano. Nisiende mbali, kwanza naiunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu sisi wote wana-CCM tulisimama kote kule tukiinadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hotuba yake yote imepitia ilani, ndiyo maana akaja na mpangokazi wa miaka mitano, nini Serikali ifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa wasaidizi wake, wameanza kazi vizuri. Tangu ametangaza Baraza la Mawaziri, tumeanza kupishana huko majimboni, wanafanya kazi nzuri sana, tuendeleo na mwendo huu huu. Mheshimiwa Rais ameaminika na wananchi wote na Watanzania wote wamemwamini, ndiyo maana wakampa kura zaidi ya asilimia 84, na sisi Wabunge tumeaminiwa na wananchi, wana imani kwa kipindi cha miaka mitano wataona mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie sehemu chake, kutokana na muda, sisi tunaotoka majimbo ya vijijini, katika Halmashauri yetu ya Wilaya yetu ya Uyui, changamoto kubwa ni barabara, ndiyo kero ya Waheshimiwa Wabunge wote walioko humu ndani, kila utakapoenda, shida ni barabara. Katika mtandao huu wa barabara, kuna baadhi tukiwaachia *TARURA* hawawezi kutekeleza kwa kipindi cha miaka mitano. Kuna barabara gharama yake na bajeti inayokuja kwenye Halmashauri ya *TARURA*, ukiiipa kwa kipindi cha miaka mitano ika-*deal* na barabara moja, haiwezi kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna barabara yenye urefu wa kilometa 89 ya kutoka Miswaki – Roya kwenda Maguliati mpaka Iyumbu, Mkoa wa Singida. Barabara hii ina madaraja 16 madogo madogo na daraja moja kubwa lenye mita 120. Hii barabara kwa takwimu ya mkandarasi ni zaidi ya shilingi bilioni sita. Halmashauri yetu inapokea shilingi bilioni 1.3 kwa mwaka. Kwa hiyo, ukisema uelekeze nguvu kule, haiwezi ikakidhi kwa kipindi cha miaka sita, barabara nyingi zote zitakuwa zimesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kupiga kelele *TARURA* iongezewe bajeti ili tuweze kukwamua kero za wananchi wetu, wapate barabara. Kwa sababu na kule kuna wapiga kura, tena wanajitokezaga sana kipindi cha kupiga kura. Naomba sana Serikali itusaidie kwenye hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye suala lingine. Sisi Wanasiasa na viongozi mbalimbali tumekuwa tukipita kwenye majimbo tukiwahimiza wananchi wetu wachangie baadhi ya maendeleo, lakini...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, muda!

**SPIKA:** Eeeh! (*Kicheko*)

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Wanyamwezi. Mheshimiwa Agness Marwa...

**MBUNGE FULANI:** Alichangia jana.

**SPIKA:** Alichangia jana! Nimewekewa orodha ya watu waliochangia jana hapa nashangaa. Mheshimiwa Cecil Mwambe, jana pia eh! Haya, nimeshamkata. Twende na Mheshimiwa Omar Ali Omar.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia na mimi fursa hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu wetu muumba wa mbingu na ardhi, aliyetuwezesha kusimama hapa na kukaa kitako huku tukiwa na hali ya afya njema wakati wenzetu wengine sasa hivi wako makaburini na wengine wako hoi bin taabani



mahospitalini. Tuwaombea dua wote hao wapate nafuu ili tuungane nao katika kujenga Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwanza kutoa shukrani zangu za dhati...

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, vipi walioko mahospitalini wana nafuu?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, vizuri sana.

**SPIKA:** Aah, basi. Haya endelea Mheshimiwa Omar. *(Kicheko)*

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Wete, Pemba. Wengi wamezoea kule tuseme kwamba Wazanzibar walio wengi hasa wakiingia kwenye Kisiwa cha Pemba wanasema waja leo warudi leo? Kwa maana ya kwamba hiyo ni jumla ya *question mark*. Usiende ukarudi, ukienda ubakie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakishukuru chama change cha *ACT*- Wazalendo. Kwanza namshukuru sana kiongozi wangu wa chama, Ndugu Zuberi Kabwe pamoja na Mwenyekiti wangu wa Chama cha *ACT*- Wazalendo, Ndugu Seif Sharif Hamad ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar, samahani kidogo. Kwani hicho chama bado kipo? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naenda moja kwa moja kwenye hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwenye ukurasa wake wa 14 ambapo alitamka

bayana katika hotuba yake ile kwa kusema kwamba katika kipindi hiki cha awamu yake ya tano ya miaka mitano inayofuata atatoa ushirikiano mkubwa na kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia ya kuleta maendeleo kwa pande zote za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Rais kwa hatua hiyo na kwa nia yake safi na tayari matunda yake tumeanza kuyaona, kwa sababu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tayari amepanga safu nzuri sana ya kuhakikisha kwamba sasa Zanzibar inafikia uchumi wa kati, kwa sababu ameanza kutumbua majipu. Nafikiri labda yeye kafuata kichogo cha mlezi wake, naukifuata kichogo cha mlezi wako, basi inawezekana wewe ukafanya vizuri zaidi kuliko hata mlezi wako huko nyuma kwa sababu kazi yako itakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba sasa niende moja kwa moja kuchangia katika hoja hizo, kuangalia zaidi ya changamoto za Muungano. Zamani tulikuwa tunaziita kero, lakini siku moja nilikutana na Mheshimiwa Waziri akasema sasa tusiziite tena kero, tuziite changamoto. Na mimi nakubaliana naye kwamba changamoto hizo, kwa sababu tayari Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Zanzibar, kero zile zinazofika nadhani 21 kama sikosei, tayari kero 11 zimeanza kupatiwa ufumbuzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Mheshimiwa Waziri anayehusika na Muungano akae chini na kutafakari na kutumia juhudi na maarifa na uwezo wake wote kuhakikisha kwamba zile changamoto ambazo zimebakia basi zimeondolewa kabisa. Ili kwamba sasa Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano tusizungumze tena kero, tuzungumze maendeleo. Baadhi ya kero hizo, ni wafanyabiashara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Endelea.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wa Zanzibar wanapochukua bidhaa zao kutoka Zanzibar na kuzileta Tanzania Bara, wanatozwa kodi mara mbili. Hilo ni tatizo kubwa ambalo ni moja katika vitu ambavyo vinatakiwa vipatiwe ufumbuzi.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Omar, nakushukuru sana.

**MFUNGE FULANI:** Aunge mkono hoja. *(Kicheko)*

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ila ungeniongezea kidogo kwa sababu ulichukua muda wangu kidogo.

**SPIKA:** Unataka kuunga mkono hoja?

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, nilitaka uniongezee japo dakika moja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar. *(Kicheko)*

Wiki ijayo tutakuwa na muda mwingi zaidi wa dakika kumi kwenye kujadili Mipango, kwa hiyo, utamalizia.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni kwenye *gallery* ya Spika. Tunaye Ndugu Nicholas Mtenga, amefuatana na Mtangazaji maarufu wa *BBC* Ndugu Salim Kikeke. Karibuni sana watangazaji wetu, tunawashukuru kwa kazi nzuri, mnatuwakilisha kwenye mataifa ya huko mliko, basi mzidi kuboresha kazi na siku fulani ikifika, basi mnarudi nyumbani. Nyumbani ni nyumbani. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nawashukuru

wananchi wa Mafinga na kila mmoja ambaye kwa namna moja ama nyingine amefanikisha mimi kurejea hapa na mimi kama ulivyositiza suala la *TARURA*, tumelisema sana, ni wakati sasa kama walivyosema watu wengine, tuje na ubunifu wa kutafuta chanzo ambacho kitasaidia *TARURA* kupata fedha ya kutosha ili angalau watu tuwe na uhakika wa kurudi hapa mwaka 2025. Kwa sababu pale Mafinga bila kuwa na barabara za lami maana yake ni kwamba wakati huo ukifika bora nisiende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiunganisha na jambo hili, jana nilikuwa na swali nikiuliza Serikali, ni lini wataanza ujenzi wa barabara za lami? Majibu kutoka TAMISEMI ni kwamba Serikali iko katika hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba ile miji 45 chini ya utaratibu wa uendelezaji miji, itakwenda kuanza kunufaika muda siyo mrefu ujao kwa sababu wako katika mazungumzo ya hatua za mwisho. Kwa hiyo, naisihi Serikali na kuiomba basi mazungumzo hayo yaende kwa haraka ili kusudi miji hiyo 45 ianze kunufaika na hivyo kupunguza mzigo kiasi fulani wa *TARURA* katika kuhudumia barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi ni mwanamichezo, najielekeza moja kwa moja katika ukurasa wa 37 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ambaye wamesema, katika miaka mitano ijayo tutakuza sanaa, michezo na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, sanaa, michezo na utamaduni imekuwa chanzo kikubwa cha mapato katika dunia ya sasa ambapo matumizi ya *internet* yamekuwa makubwa sana. Nina takwimu hapa, *projection* ya *PWC* inasema kwamba mwaka 2017 mapato yaliyotokana na *media and entertainment industry* katika Tanzania yalikuwa takribani dola milioni 496. *Projection* kufikia 2022 itakuwa bilioni 1.1 ambayo ni sawa trilioni 2.5. Kwa hiyo, hii ni sekta ambayo ni chanzo kikubwa cha mapato, lakini pia ni chanzo kikubwa cha kuchangia ajira, katika zile ajira milioni nane ambazo Mheshimiwa Rais amepanga tuzizalishe katika mwaka 2020 – 2025.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza TCRA, baada ya kuwa wamewafungia *Wasafi Tv*, sasa wamesema kwamba adhabu imepungua. Najielekeza katika COSOTA na BASATA. Mheshimiwa Rais alielekeza nami nimezungumza karibu miaka mitano, imekuwa sasa *under one roof*, lakini haitoshi. Ikiwa TCRA, NEMC wako mpaka *level* ya kanda, kwa nini BASATA na COSOTA wasirudi hadi *level* ya kanda kuwapunguzia wasanii safari na gharama za kusafiri mpaka Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, tazama msanii atoke Kongwa, aende Dar es Salaam, anaingia gharama nyingi. Atoke Tandahimba, Ilemela au Mafinga, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba kama hii ni sekta ambayo inazalisha mapato ya kiasi cha shilingi trilioni 2.2 na ni chanzo cha ajira, ukiangalia hapa matamasha mbalimbali ambayo huwa yanafanywa hapa nchini kwetu, yamekuwa ni chanzo kikubwa cha ajira.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, nawapongeza Wizara ya Habari, wana tamasha hili la *Serengeti Festival*, ukienda pale Jamhuri kuanzia mama ntilie, muuza mahindi, muuza *Big G* atapata pesa. Matamasha mbalimbali kama muziki mnene *EFM*, kama tamasha la Tunawasha la Wasafi, matamasha kama *Fiesta* la *Clouds*, mtikisiko la Redio Ebony kule Iringa, yaani wakati ule wa tamasha, mzunguko wa fedha unakuwa umeongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaposema tumsaidie Mheshimiwa Rais, taasisi ambazo zinalea sekta hii, ninashauri zishuke mpaka ngazi ya chini, BASATA, COSOTA na Bodi ya Filamu waende mpaka kiwango cha angalau ngazi ya kanda ili ku-*facillitate* wasanii, kusudi lile lengo la kuzalisha ajira milioni nane na kuongeza mapato katika Serikali na mtu mmoja mmoja yapate kutimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema *easy way of doing business* maana yake ni kupeleka zile huduma karibu na wale ambao wana *contribution* na mapato na kuzalisha ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja, nitachangia ipasavyo na kikamilifu katika Mpango. Mungu atubariki sote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Mheshimiwa Mwantumu Zodo nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Kwanza kabisa kama utamaduni wetu Watanzania kushukuru na mimi naomba nishukuru kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili tukufu, naomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kikiongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Mwenyekiti wa chama chetu, Wajumbe wa Kamati Kuu, lakini pia nawashukuru akinamama wa Mkoa wa Tanga kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Kamati yangu ya Utekelezaji Mkoa wa Tanga na Taifa pamoja na familia yangu kwa kuni-support. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais kwenye kipengele cha elimu. Kutokana na muda sasa hivi ni mchache, dakika tano, nitakwenda moja kwa moja kwenye elimu, sitaweza kugusa vitu vyote na kwa kuwa mambo mengi yameshaongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi toka tumeanza mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la elimu, Serikali ya Chama chetu cha Mapinduzi ikiongozwa na Jemadari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa; kutoa elimu bure ndani ya kipindi cha miaka mitano. Kuanzia 2016 mpaka leo tumetoa shilingi trilioni 1.01 ambayo imesababisha ongezeko la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na elimu bure, pia Rais John Pombe Magufuli chini ya uongozi wake ameongeza idadi

ya madarasa katika shule za msingi kutoka madarasa 16,899 tuliyokuwa nayo hapo awali mpaka kufikia madarasa 17,804. Pia tumeongea shule za sekondari kutoka shule 4,708 mpaka shule 5,330. Pia tumekarabati shule kongwe na wengi tunaotoka huko mikoani ni mashahidi kati ya shule 89, shule 73 zimekarabatiwa na zimebaki shule 16 na ni Imani yangu kwa Serikali hii na kasi hii ya Awamu ya Tano tutakwenda kumalizia shule hizi 16 kwa kipindi hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mabweni 253 yamejengwa, kwa hiyo, ni mafanikio makubwa. Vyumba 227 vya maabara vimejengwa na maabara 2,956 zimepatiwa vifaa. Tumeona ongezeko la madawati la asilimia 200. Hayo ni mafanikio makubwa kwa Rais huyu mtetea wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi nimesema kutoka 1,648,359 mpaka 2,185,037 kwa shule za sekondari. Kupitia kipengele hicho cha elimu na mafanikio hayo makubwa na kazi kubwa naomba nishauri kitu. Naomba nishauri upande wa mtaala. Tumeona mambo ni makubwa yaliyofanywa lakini kwenye kipengele cha mtaala iko haja ya ku-review mtaala wetu, malengo ya mtaala.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru, naomba niunge mkono hoja kwa mafanikio hayo makubwa yaliyopatikana kwenye elimu na Wizara nyingine zote. Ahsante nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Zodo. Basi wiki ijayo jiandae uje uanzie hapo kwenye mitaala hapo usonge mbele ili Profesa Ndalichako aweze kuandika *point* zako. *(Makofi)*

Nilishakutaja Mheshimiwa Kunti, utafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na mimi kwa kunipatia fursa ya kuweza ushauri wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutujaalia uhai na afya njema imetusababisha tunaendelea kukutana katika ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nisemee suala zima la huduma ya afya kwa Watanzania. Mheshimiwa Rais amesema kwenye hotuba yake kwamba tumeongeza vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali za wilaya na mikoa na ukarabati wa hospitali zetu za kanda. Kwenye hili, kujenga vituo vya afya kwa maana ya majengo, kujenga zahanati kwa maana ya majengo, kujenga hospitali za wilaya kwa maana ya majengo bila kuwa na dawa pamoja na vifaatiba na wahudumu kwenye hospitali zetu ni sawasawa na kutwanga maji kwenye kinu, mshahara wake ni kuloa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kama jinsi mlivyojenga haya majengo tunwaomba muende mkawaajiri watumishi wa Wizara ya Afya ili waende kwenye hospitali zetu hizo kuanzia zahanati mpaka hospitali zetu za rufaa waweze kupata huduma.

Pili, muende mkanunue vifaatiba. Asubuhi dada yangu Mheshimiwa Ritta aliuza swali kuhusiana na *CT-Scan* kwenye hospitali ya Mkoa wa Iringa. Lakini hata sisi Dodoma hapa, *CT-Scan* tunayo Ntyuka pale ni shilingi 200,000; ni Mtanzania gani anayeweza kumudu kipimo hicho? Kwa hiyo niombe Wizara na Serikali iweze kuona kwenda kununua vifaatiba hivi ili Watanzania wenzetu waendeleo kupata huduma iliyo bora ya afya na waimarishe afya zao ili waweze kujenga uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala zima la maji; mwaka 2015 mlituahidi wakati wa kampeni mkatuambia mnakwenda kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani. Watanzania tukaenda tukapiga kura, ndoo ya mwanamke kichwani bado haijatulika kichwani. Bado mwanamke wa Kitanzania hususan



anayeishi vijijini anateseka kutembea umbali mrefu akiwa na ndoo yake na mtoto mgongoni anatafuta maji.

Niiombe Serikali safari hii mkija kwenye suala zima la Wizara ya Maji, twendeni tukatenge bajeti ambayo haitakuwa bajeti ya maandishi na maneno na ya kusifiana humu ndani, twendeni tukatenge bajeti itakayokwenda kutekeleza miradi ya maendeleo kama jinsi Mheshimiwa Spika tulivyokwenda kuwekeza kwenye miradi mikubwa *Stiegler's*, tumenunua ndege. Basi vivyo hivyo hebu twende tukaone suala zima la upatikanaji wa maji ndani ya Taifa letu ili tuweze kuepuka maradhi, lakini pili tupate fursa ya kupoteza na kuokoa muda ambao tunautumia kwenda kutafuta maji. Muda ule utusaidie kujenga uchumi wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema kitanda usichokilalia huwezi kuwajua kunguni wake. Tunapoomba suala zima la Katiba Mpya, sio kwamba tunaomba ili tuweze kujifurahisha. Tumekuwa hatuna imani na suala zima la Tume yetu ya Uchaguzi na unaweza ukasema Kunti unasema huna imani na Tume ya Uchaguzi mbona wewe uko humu ndani, mimi nilishiriki uchaguzi wa Jimbo yaliyotokea ni mengi. Kwa maoni yetu tunatamani hiyo Katiba Mpya ambayo yale maoni ya wananchi waliyoyatoa kwenye mapendekezo ya hiyo Katiba Mpya ambayo yatakwenda kutupatia Tume Huru ya Uchaguzi yanaweza kutujengea faraja sisi wa vyama vya upinzani pamoja na Watanzania kwenda kuamini tena kwamba tutakuwa kwenye Taifa letu uchaguzi wa huru na wa haki na wa kidemokrasia katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti. Umeunga mkono hoja? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kunti umeongelea habari ya *CT-Scan* shilingi 200,000 lakini ile nadhani ni *once off* yaani ukishapima

*CT-Scans* sasa unaendelea na mambo mengine, yaani hurudi kesho na kesho kutwa labda kama kuna sababu kubwa mno. Namuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya yuko hapa. Naambiwa, sina hakika wakati huu kuna baadhi ya hospitali za *private* hapa nchini na hasa Dar es Salaam ambapo ile mashine ya kupumua (*ventilator*) kuna baadhi ya hospitali ambazo zina *charge* shilingi 1,000,000 kwa siku, kuna ambazo zina-*charge* 850,000 kwa siku, shilingi 700,000 kwa siku. Nikasema *yarrab* toba! Hata kama ni za *private* lko haja ya Wizara kuangalia hilo jambo kabisa. Ndiyo maana nasema afadhali ya shilingi 200,000 kwa wakati mmoja angalau. Sasa hii shilingi 1,000,000 kutwa? Kwa mwaka shilingi shilingi 365,000,000 kweli? Endapo jambo hilo ni kweli.

Mheshimiwa Issa Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hii hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa tarehe 13 Novemba, 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema lolote na mimi kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu sana kwa kunipa nafasi hii. Pili, nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipitisha mimi kuwa mgombea na kunisaidia kushinda kwa kura nyingi sana. Pia nisiache kuwashukuru sana sehemu kubwa ya familia yangu, mke wangu na wanangu kunivumilia katika kipindi cha uchaguzi ambacho kilikuwa kigumu sana. Kwa sababu ya muda niendeele moja kwa moja na nijielekeze katika maeneo machache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele kadhaa karibu vitano lakini kimoja cha kuimarisha utawala bora wa kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma, rushwa na wizi niseme machache hapo. Ni kweli Mheshimiwa Rais amefanya makubwa katika kipindi chake cha Awamu ya Kwanza ya miaka mitano. Tumeona wametumbuliwa watu wengi, tumeona watumishi wazembe ambao wamewajibishwa, taarifa inatuambia takriban watu au

watumishi 32,555 walichukuliwa hatua mbalimbali. Pamoja na haya, Mheshimiwa Rais katika ukurasa wa tisa nikinukuu amesema ataboresha mazingira ya kazi pamoja na maslahi ya watumishi wote ili yaendane na hali halisi ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli katika kipindi cha miaka mitano, watumishi wa umma hawajakaa katika hali nzuri, ukweli hawajaona mishahara lakini hii yote ilikuwa inatokana na jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais alikuwa ana kazi kubwa ya kuona jinsi gani uchumi na hali ya Kitanzania katika mapato inapanda. Tuemona uchumi umepanda takribani kwa asilimia saba kila mwaka. Tumeona Pato la Taifa limepanda kutoka trilioni 94 hadi 139. Tumeona ameweza kudhibiti mfumuko wa bei. Sasa kwa yote haya ninaona kabisa hili ambalo Mheshimiwa Rais anataka kwenda kulitekeleza katika kipindi kijacho kinaenda kuwa bora kwa watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, niseme pia juu ya hili la kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Pamoja na mambo mengine lakini liko jambo hili asilimia 10 kutoka mapato ghafi ya Manispaa zetu. Wengi wamesema katika eneo hili, lakini mimi ninaliona pamoja wametamkwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa asilimia 4:4:2; lakini naona kundi la vijana kuanzia miaka 35 na wazee wamesahaulika kabisa. Hao ni kuanzia umri kama wa kwangu na kuendelea. Akinamama kuanzia umri wa ujana hadi wanazeeka wanawezeshwa katika asilimia hizi 10. Inajionesha wazi katika sura za usoni wazee au vijana wanaokuja kuwa wazee watakuja kukosa nguvu za kiuchumi na hali mbaya itakuja kwa wakati huo. Hilo niliona likae hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niseme juu ya fedha hizi zinazotolewa hasa katika kundi la vijana. Sasa tunawapa asilimia nne zao lakini hatuwaoni wanaenda kufanya biashara maeneo gani. Wale vijana wanaowawakilisha wamesema vizuri, lakini mimi nataka kusema katika Mkoa wa Dar es Salaam, Wilaya ya Ubungo hususan katika majimbo haya mawili tumeona upanuzi wa barabara wa njia nane

kutoka Kimara mpaka Mlandizi takribani shilingi bilioni 140, Mheshimiwa Magufuli amezielekeza katika ujenzi wa barabara ile na tunatambua hizi fedha ni za ndani. Ni kweli upanuzi huu umetupa taabu sana kwa ajili ya vijana wengi na wafanyabiashara machinga pembeni mwa barabara, leo wanalia sana kuanzia Kimara, Temboni, *Stopover*, Mbezi yote hata pale Kibamba CCM.

Mheshimiwa Spika, niombe sasa Mheshimiwa Waziri alleleza vizuri. Wakati tunajenga vile vituo vya daladala, vituo vya mabasi basi tutumie sehemu fulani tuanze kuwapunguza hawa wajasiriamali wakiwa wamepata mabanda mazuri kama lile banda pale Mvomero ambalo Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo wakajengewa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nijielekeze kwenye eneo moja la elimu kwa haraka. Wengi wamesema lakini hasa nipongeze sana, lile la King'ong'o ni la kwanza, lakini sasa tayari taarifa inasema yatafanyika mazuri lakini zaidi kutokana na muda niache tu nitajielekeza katika mpango unaokuja niseme vyema juu ya maji na miundombinu yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nitumie nafasi hii kukushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Orodha niliyonayo imechanganywa changanywa na wale waliochangia jana, sasa inanipa taabu kidogo. Mheshimiwa Ramadhan Abeid Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Ni Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili niwashukuru wananchi wangu wa Singida Kaskazini kwa kuniadini na kunipa fursa ya kuja kuwakilisha sauti zao katika Bunge letu hili tukufu. Nikishukuru pia Chama changu cha Mapinduzi kwa imani

yake kwangu na mimi naahidi kama nilivyowaahidi kwamba sitawaangusha, nitawatumikia kwa unyenyekevu mkubwa na kwa uaminifu wa kutosha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia mjadala, Wabunge wengi wanazungumzia jambo la *TARURA*, barabara, afya, maji na kilimo. Haya mambo ndiyo yanayogusa maisha ya Mtanzania. Naomba sana tuzingatie hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo na yenyewe ilijikita kwenye haya haya na mimi siliti hotuba, naiita yale yalikuwa ni maelekezo. Tuichukue hotuba ile tuitazame neno kwa neno, tuchukue hayo maelekezo itoshe tu kusema Mheshimiwa Rais alitupa maelekezo sisi Wabunge pamoja na Mawaziri na alisema hebu msioCOPE. Amesema fanyeni maamuzi chukueni hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu naomba ujielekeze zaidi kwenye kushauri kwa sababu mengi yamesemwa, suala la *TARURA* ni msiba, ukienda vijijini hakuna barabara ni mapalio. Sasa sisi tumechoka kupita kwenye mapalio. Wabunge hapa wanazungumza maisha halisi yaliyoko kule kwenye *field*. Tumechoka kupita kwenye mapalio, ninashauri kama hii *TARURA* haipewi fedha ifutwe! Kwa sababu hizo ni kodi za Watanzania, majengo wanayojenga kila Wilaya nchi hii hata lile jengo lao pale Wizarani hizo ni kodi za Watanzania. Hizo fedha badala ya kutumiwa kwenye mafuta, jengo na kwenye viti na mishahara, hizo fedha zichukuliwe zipelekwe zikatengeneze barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kwa uchache kwenye jimbo langu tu kwenye hili eneo la *TARURA* kilometa 800 za barabara wanapewa shilingi milioni 600, utatengeneza nini hapo? Si vichekesho hivi? Naomba hili jambo lichukuliwe, Serikali ilianganalie tuanche kurudia rudia mambo sio kila siku tunazungumza jambo hili. Kurudia rudia ina maana hawa Wabunge hawaaminiki wanapolalamika suala la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nizungumzie eneo la viwanda. Mheshimiwa Rais dhamira yake ilikuwa ni kuhakikisha tunakuwa na uchumi wa viwanda na uchumi wa viwanda hatuwezi kuuona endapo sekta ya viwanda haijawa *connected* na sekta za uzalishaji. Itakuwa ni ndoto! Tuhakikishe tunaelekeza nguvu zetu zote kwenye eneo la uzalishaji. Tuangalie kwenye kilimo, tuangalie kwenye uvuvi, tuangalie kwenye ufugaji, huko ndiko tunakuta Watanzania wengi na ndio wanaozalisha na hao ndio wanaoweza kutuletea *raw materials* zinazohitajika kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi leo natoleo mfano tu mdogo kwenye eneo la mifugo, ngozi inaoza na mimi ambaye ni mfugaji mtoto wa mkulima tunahitaji tuone yale mazao kule vijijini yanakuwa *processed*, yawaajiri Watanzania. Tunalalamika suala la ajira, tunamuajiri wapi Mtanzania kama hatujajikita kwenye eneo la viwanda? *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba haya machache niliyoyazungumza nione yakitekelezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatey Massay, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. FLATEY G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kusema jioni hii ya leo. Kwanza naomba nimshukuru Mungu kwa kutujalia na kutupatia uhai, lakini pia nikishukuru chama changu kwa kunichagua na kuniteua jina langu na kupigiwa kura na wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini. Niwashukuru sana kwa kunipa kura na kunileta humu ndani. Nikushukuru na wewe sasa kuwepo tena kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa kuchangia hizi hotuba mbili za kufunga Bunge la Kumi na Moja na kufungua la Kumi na Mbili, ukiangalia sasa jinsi ambavyo Rais wetu anavyofanya kazi mimi namuombea Mungu ampatie afya njema, aendelee kumpa nguvu ili hizi ndoto ambazo amekuwa akizungumza katika hotuba yake Mungu asaidie na sisi tumsaidie twende naye kufanya Tanzania ambayo sasa tumeingia kwenye uchumi wa kati, twende zaidi ili wananchi wetu waondokane na kero ambazo zipo katika maisha ya kawaida ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu dakika ni chache naomba niende kwenye upande huu wa kilimo. Ukiangalia ukurasa ule wa 27 kilimo chetu wananchi wanakitegemea sana, zaidi ya asilimia 75 wanategemea kilimo. Sasa naomba nishauri kwa sababu Wizara sasa ndio wana kazi ya kuhakikisha kwamba wanaangalia ile *vision* ya Mheshimiwa Rais wakati anaitoa hotuba hii. Ukiangalia leo mvua zinanyesha na mimi niishauri Wizara nayo iangalie iende katika kuwekeza kuzuia maji yanayotokana na mvua na kuchimba mabwawa, ili mabwawa yanapochimbwa basi itasaidia zaidi kufanya kilimo cha uhakika. Tukichimba mabwawa, tukaweka fedha na fedha hizi tukasaidia kuziwekeza katika mabwawa na maeneo mengi ya wafugaji na wakulima mabwawa haya yatatumika kwa mambo mawili, kwanza yatanywesha mifugo, lakini pili tutakuwa na kilimo cha uhakika wa kupata mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Mheshimiwa Rais amezungumza sana na ameahidi kwamba, katika wakati huu atahakikisha pembejeo zinafika kwa haraka. Na pia, ukiangalia sasa kwa hali ya saa hizi tusipoweza kuishauri Serikali vizuri na mimi naomba niwashauri, ukiangalia leo hii bei ya mbegu katika maeneo yetu ni kubwa zaidi kuliko debe moja. Kwa mfano, kilo moja saa hizi au mbili katika mfuko mmoja ni shilingi 13,000/= mpaka shilingi 14,000/=. Debe unapokuwa umevuna mazao linakuwa na shilingi 6,000/=; kwa hiyo, basi mimi nishauri tuone namna gani pia ya kuanzisha mashamba ya mbegu humu nchini kuliko mbegu

kutoka nje ya nchi kuja kuuzia huku. Kwa nini tusizalishe mbegu sisi tukawauzia wakulima? Na hili linawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini linguine kutokana na muda twende kwenye *TARURA*. Mimi nina kilometa 1,300 kwenye Jimbo la Mbulu Vijijini, tunapata shilingi milioni 696 haziwezi kutengeneza barabara hii. Sasa niombe wakati tunatunga sheria ya kuisaidia Serikali kutumia mfumo huu wa bei ya soko yaani *force account*, kwa kutumia miradi hii ya afya na miradi mingine ya kujenga majengo ya shule wataalam hawakukubali sana; mimi niombe Serikali ije na mpango, ione namna gani ya kusaidia hii *TARURA* maana tunaweza kuwa katika ukandarasi tunapigwa sana. Sasa ili kuona namna ya kusaidia Serikali hebu tujaribu twende kwenye *force account* pia kwenye *TARURA* naamini katika njia hiyo tunaweza kusaidika.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia barabara zetu nazo zimekuwa na halimmbaya sana, ni ngumu. Tuone namna gani mwaka 2016 tumezungumza Habari ya *TARURA*, mwaka 2017 tumezungumza hivyo, mwaka 2020 tumezungumza hivi hivi, tunaenda mwaka wa 2021 naomba sasa tufanye namna ya maamuzi makubwa tuamue ili *TARURA* ikafanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naona muda umeisha, basi kwa sababu, muda umeisha tutakutana kwenye mpango, niunge mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mtaona kwa kweli, jambo la *TARURA* linawauma Waheshimiwa Wabunge, karibu kila mtu ana-zero in hapo. Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nipate kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza nitoe shukrani kwa chama changu na Mwenyekiti wa Chama kunipa nafasi ya kuwa mgombea na mwisho wa siku kuwa Mbunge katika Bunge hili, lakini la pili vilevile nawashukuru sana wananchi



wa Njombe Mjini kwa kuniamini na kunipa nafasi ya Ubunge nasema sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa ni hotuba ambayo imetoa matumaini makubwa sana. Ni matumaini yaliyojengwa katika msingi wa mafanikio yaliyopatikana katika miaka mitano iliyopita, yameongelewa hapa kwa wingi hatuna sababu ya kuyataja yote, lakini mimi niongelee moja ambalo limenigusa na litaendelea kunigusa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais tumeshuhudia akifanya mabadiliko makubwa sana katika sekta ya madini. Mimi nasema yalikuwa ni maamuzi sahihi katika wakati sahihi. Tumeshuhudia sasa sekta hii ya madini kuwa ni sekta ambayo inaongoza kwa kuongezea nchi fedha za kigeni, lakini ni sekta inayokua kwa haraka sana. Naomba sasa Serikali iendelee kujikita na kuangalia madini mengine na hasa kwa vile utafiti katika sekta ya madini ni jambo la muhimu sana. Tunaelewa hatuwezi kutegemea wawekezaji kutoka nje kufanya utafiti, kwa hiyo, wazo langu au ushauri wangu kwamba Serikali ijikite kuiongezea *STAMICO* hela za kutosha ifanye utafiti. Na sisi tunawakaribisha kule Njombe kuna madini ya kila aina waweze kuja kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nilitaka niongelee ni suala zima la viwanda na uwekezaji. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais imejikita sana kuongelea sekta binafsi na viwanda. Ni jambo muhimu na ni jambo ambalo litatufanya sisi tuweze kufikia lengo la zile ajira milioni nane. Kule Njombe tumejikita katika uwekezaji na ukulima, lakini kwetu sisi suala la viwanda ni suala la muhimu sana na Mheshimiwa Rais anaongelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme moja kwamba wakati tunawavutia wawekezaji katika viwanda tuangalie wawekezaji waliopo katika maeneo yetu. Kule Njombe tuna zao moja la kimkakati la chai, ni zao ambalo linatakiwa lipewe umuhimu mkubwa sana. Kwa sasa zao hili linalegalega na

kuna uwezekano kama hatua za haraka hazitachukuliwa litafikia mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito, naelewa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ameongelea kuweka mazingira wezeshi ambayo yatasaidia uwekezaji uweze kufufuka katika maeneo mbalimbali. Nipende kusema kwamba bado pamoja na kwamba kuna *blue print* na tunaielewa inakuja, tumeshuhudia kwamba bado kuna tozo za kila aina ambazo zimekuwa ni kero kwa wawekezaji na kero hizo kwa vile ni suala la viwanda na kwa vile tunaongelea chai, tunaongelea mkulima wa kawaida ambaye mwisho wa siku ndiye kipato chake kitashuka.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha ukulima viwanda vya chai ambavyo viko katika maeneo sio tu ya Njombe, lakini na maeneo mengine ya jirani tozo zake ukilinganisha na viwanda vingine vya Kenya vya chai na viwanda vingine vya nchi kama Malawi unakuta wenzetu tozo ni chache sana. Kuna *study* imefanyika inaonesha tozo za viwanda vya chai peke yake zinafika karibu 19 wakati wenzetu hawana tozo, kwa hiyo, ningepomba Serikali ilitupie macho jambo hilo kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini niongelee vilevile kero nyingine ambazo zinajitokeza katika kushughulikia masuala ya wafanyabiashara, hasa wa mazao ya miti katika Jimbo la Njombe na Jimbo la Njombe ni Jimbo la Njombe Mjini, lakini lina vijiji vingi sana.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba niunge hoja mkono, lakini nipende kuisitiza iko haja ya kutatua kero za wakulima wa miti na mashamba ya mbao kule Njombe kama vile Rais alivyoahidi wakati wa kampeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Mwanyika. Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Natany, Mbunge wa Mpwapwa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili nami niweze kuchangia katika mjadala huu unaondelea. Kwanza nianze kwa kukipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa uliopatikana katika uchaguzi mkuu, lakini pia naomba nimpongeze sana Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana katika awamu hii ukilinganisha na mahali tulikotoka, lakini pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Vwawa kwa kunichagua na kunifanya kwamba niwe Mbunge kwa awamu ya pili, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachangia hotuba ya Rais na ninaona hapa kuna hotuba ziko mbili, ya mwaka 2015 na ya mwaka 2020. Na mimi naamini lengo la hotuba zote mbili ni kutupa mwelekeo kwamba tulikotoka tumetoka wapi, tumefika wapi, tunataka twende wapi.

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa aliwahi kutuambia kwamba ili nchi yoyote iweze kuendelea inahitaji vitu vine, tunahitaji ardhi, watu, siasa safi na tunahitaji uongozi bora katika hivi vitu vyote tumepata mafanikio makubwa. Cha kwanza ardhi tunayo ya kutosha, watu tunao, lakini siasa safi tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao uongozi tumekuwa na tatizo dogo kwenye uongozi na tunaona kabisa nchi yoyote inayotaka kuendelea duniani uongozi imara ni msingi mkubwa sana katika kulifanya Taifa lolote lifikie malengo yake. Na kwa hatua hiyo, ukichukua hotuba ya Rais yam waka 2015 aliyoitoa mambo aliyoyafanya na tukiona matokeo yake sasahivi, labda kwa sababu ya muda nitasema tu machache.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kwa kuonesha umahiri wa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, la kwanza jambo

lililoshindikana kwa miaka yote ya Serikali zote zilizotangulia pamoja na kwamba, kila Serikali ilifanya mambo makubwa, lakini jambo lililoshindikana la kuhamishia Serikali Dodoma limewezekana. Hiyo inapima ubora wa kiongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili alilolifanya Rais Magufuli ni kuikokota nchi kutoka kwenye nchi maskini na kuifikisha kuwa nchi ya kipato cha kati. Hili sio jambo la kubeza, ni jambo kubwa ambalo limefanyika, ni jambo kubwa ambalo viongozi wote wanastahili kupongezwa likiwemo Bunge la Kumi na Moja kwa kazi kubwa ya kuisaidia nchi kutoka tulikotoka mpaka tumeiingiza kuwa nchi ya kipato cha kati. Sasa tumekuwa ni nchi ya kipato cha kati kwenye ile *lower boundary*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa ukiisoma ile hotuba ina mambo mengi, kwa sababu ya muda siwezi kusema, lakini jambo la tatu ni miradi mikubwa aliyoweza kuitekeleza ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imetekeleza ambayo imebaki kama alama. Ukichukua mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ambao unaendelea sasa hivi, mkoloni alijenga reli ya kati, tulipopata uhuru tumejenga reli ya TAZARA, sasa tunajenga SGR kwa hela yetu. Hili ni jambo la kujipongeza na ni maendeleo makubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga bwawa la umeme, tunajenga kwa fedha zetu. Tumenunua ndege, tunajenga viwanda, barabara, kila aina ya mafanikio. Haya yote ndio yanapima utekelezaji wa hotuba aliyoitoa Rais mwaka 2015. Mwaka 2020 Rais anatuambia nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda ni *quote* ukurasa ule wa 26. Anasema, "mbali na hatua hizo kwa lengo la kukuza uchumi, kupambana na umaskini na pia kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira tunakusudia kwenye miaka mitano ijayo kuweka mkazo mkubwa katika kukuza sekta kuu za uchumi na uzalishaji, hususan, kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, madini, biashara na utalii." (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Hotuba ya Rais aliyoitoa ya awamu ya pili inatupa muelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha pili. Na hii kama kweli tukiweka nguvu tukawekeza kwenye sekta za uzalishaji za kukuza uchumi ni wazi kabisa miaka mitano itakapokwisha tutakuwa tumefikia sasa kwenda kuwa nchi ya kipato cha kati cha uwanda wa juu. Na hili linawezekana kama Bunge litaweka *targets* na malengo thabiti ya kuisimamia Serikali na kuishauri Serikali. Na ninaamini haya yanawezekana kwa uongozi wako na kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu awabariki. Ahsanteni, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Nilikutaja Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wenzangu wote kukupongeza na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Ni Mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Malima tumefurahi kwa sababu kiti ulichokikalia ndio kilekile cha Mpwapwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nilipoambiwa asubuhi nilifurahi sana. Nimeambiwa kiti hiki *Senator* alikuwa analia sana kwa ajili ya barabara, barabara ya kutoka Kongwa kwenda Mpwapwa na mimi leo nimesimama mbele ya Bunge lako kushukuru sana kwa ajili ya nafasi hii, lakini pia nishukuru Chama changu cha Mapinduzi ambacho kilinipa ridhaa ya kugombea na nilishinda kwa kishindo, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais. Kusema kweli hotuba yake ndio imebeba mustakabali wa Taifa letu. Ni wajibu wetu sisi kama Wabunge, mawaziri tumasaidie Rais kutafsiri maono yake katika njia ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wote wamesema habari ya *TARURA* na mimi ni muhanga wa *TARURA*. Kwenye jimbo langu la Mpwapwa barabara ni mbaya sana kwa sababu kwanza jioografia ya Mpwapwa ni eneo lenye vilima vingi, kwa hiyo, mvua zikinyesha maji yanaporomoka yanakata barabara, leo hali ya barabara za vijijini kule Mpwapwa ni mbaya sana na mimi nisiseme sana, ningependa tu kusema naomba sana bajeti ya *TARURA* iongezwe na niseme tu ifike hata asilimia 45 inaweza kusaidia kupunguza tatizo la barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo lingine kubwa ni la upande wa *TANROADS*. Barabara hii ya kutoka Kongwa kwenda Mpwapwa ni barabara yenye urefu mfupi sana, ni barabara yenye takribani kilometa 32, lakini barabara hii imedumaza sana uchumi wa Mji wa Mpwapwa na watu wake. Hakuna mtu angependa kwenda Mpwapwa leo kwa sababu ya ubaya wa barabara ile. Barabara hiyo *Senator* Lubeleje amelia sana miaka ya nyuma. Sasa naomba Serikali ifike wakati kilio chetu cha watu wa Mpwapwa kisikike ili barabara hii itengenezwe, ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi. Na mimi naamini Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itasaidia barabara hii kujengwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni wazo zuri la Mheshimiwa Rais kuamua kutoa elimu bure kwa watoto wetu wa kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Wazo hili ni jema sana, lakini wasiwasi wangu nimeona kwamba tusipomsaidia Rais sisi kama Serikali wazo hili mwisho wa siku tutakuwa na wanafunzi wengi wanamaliza shule darasa la saba na wengine wanamaliza kidato cha nne hawajui kusoma na kuandika kwa sababu idadi ya wanafunzi wanaoingia katika darasa la kwana na kidato cha kwanza haiendani na idadi ya walimu.

Mheshimiwa Spika, walimu hawatoshi kwa kipindi kifupi nilichokaa Jimboni nimegundua kuna upungufu mkubwa sana wa walimu karibu kila shule walimu hawatoshi

naomba sana Wizara ya Elimu ijaribu kutafuta namna ya kuongeza walimu katika shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningeweza kuzungumza ni juu ya umeme, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kazi njema sana ambayo ameifanya kuleta umeme katika nchi hii. Lakini mimi naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri ukiangalia, ukipita kwenye vijiji umeme umepita kwenye *centers* za vijiji haujapanuka nimesikia asubuhi kwamba mpango wa Serikali ni kujenga mpaka kwenye vitongoji kuweka umeme, basi wanapoenda kuweka umeme kabla ya vitongoji, lakini vile vijiji vikamilike ukienda kila kijiji bado kuna kilio watu wanataka umeme umepita katika eneo la *center* lakini maeneo mengine bado hayajafikiwa. Kwa sababu ya kazi nzuri ya Waziri naamini mpaka miaka mitano itakapofika kazi hii itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji ni tatizo ambalo pia katika Jimbo langu linaendelea na ni kubwa naomba sana Serikali ushauri wangu ni kwamba wakati mwingine tunataka kupata miradi mikubwa sana kwenye vijiji ya maji, lakini hebu nishauri badala ya kushauri miradi mikubwa ya kuweka *network* ya maji kwenye vijiji tuchimbe angalau kisima kimoja tu wakati tunasubiri upembuzi yakinifu, tunasubiri tathmini watu wawe wanakunywa maji hata kwenye kisima pale tu peke yake, halafu hayo mengine yatafuata kuweka *networking* na nini sasa hivi maeneo mengi hakuna maji vijijini watu wanaendelea ku-*suffer* na Mheshimiwa Rais amezungumza kwamba inapofika 2025 kila kijiji kitakuwa na maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja 100%.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Malima Natany George, Mbunge wa Mpwapwa na jirani yangu. Kwa kweli

barabara ya Kongwa - Mpwapwa mtihani haya. Mheshimiwa Janejelly James Ntale.

**MHE. JANEJELLY J. NTALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa jicho lako kuniona, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuwa mmojawapo wa Bunge la Kumi na Mbili. Lakini niwashukuru wakinamama wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam na Baraza Kuu la UWT Taifa na wajumbe wengine wako humu ndani ya Bunge kwa kuniadini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nishukuru Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndiyo chama pekee kinatupa nafasi watumishi wa Serikali ndani ya Bunge hili, ahsanteni sana. Lakini nimesoma risala zote mbili, Mheshimiwa Rais anaongelea maboresho ya watumishi na maslahi ya watumishi, tunashukuru sana alivyohamishia Serikali Dodoma ametekeleza kilio cha watumishi wa Serikali na vyama vyao ambavyo tulikuwa kila siku tukishauri hilo, tunamshukuru sana.

Lakini tumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alisimamia zoezi hilo aliposema kila mtumishi kuondoka Dar es Salaam ahakikishe akaunti yake imesoma, tunakushukuru sana. Lakini tunampongeza Rais kwa jinsi alivyojenga mji wa Kiserikali Mtumba, mji huo umeleta mahusiano kazini kwa kufanya Wizara kati ya mtumishi na mtumishi kufahamiana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwenye risala yake anasema ataboresha maslahi ya watumishi, lakini niombe kushauri ili maslahi ya watumishi yaboreshwe turudi kwanza tuangalie sheria za kiutumishi, kuna baadhi ya sheria yatafanya zoezi hili liwe gumu. Kuna sheria moja inaitwa sheria ya *re-categorization*...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ntale ukae chini upokee taarifa, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sababu ya muda nitaenda kwa kifupi sana.



Mheshimiwa Ntale ningependa kukupa taarifa kwamba umesema Chama cha Mapinduzi ndiyo cha pekee kutoa fursa kwa watumishi wa umma, ujue kwamba tulikuwa tuna Mbunge anaitwa Dkt. Sware Semesi alikuwa ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu, alikuwa ni Mbunge wa CHADEMA, alikuwepo mama Lyimo alikuwa ni *Chancellor* wa Chuo Kikuu pale alikuwa ni Mbunge wa CHADEMA, mimi peke yangu nilikuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Mbunge, kwa hiyo usipotoshe, na wengine wengi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejerry James Ntale unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JANEJELLY J. NTALE:** Mheshimiwa Spika, naomba nisiipokee hiyo taarifa kwenye Chama cha Mapinduzi kimetenga nafasi mbili kabisa kwamba ni nafasi za watumishi wa Serikali kutoka kwenye vyama vya wafanyakazi na humu ndani tuko wawili mimi na Dkt. Alice, sipokei hiyo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naongelea sheria ya *re-categorization*. Sheria hii kama haijaumiza mtumishi yeyote aliyehumu itakuwa imeumiza mtoto wako au mpiga kura, ile sheria mtumishi akijiendeleza, akiomba kufanyiwa *re-categorization* anashushwa mshahara na kwenda kuanzia kwenye cheo kile cha wale wengine waliopo.

Mheshimiwa Spika, binafsi sisi hatupingi mtu kwenda kuanzia pale wanapoanzia wataalam wale, lakini aachwe na mshahara wake. Kwa sababu nimefanyakazi Wizara ya Fedha kila mtumishi ana *budget line* yake ya mshahara huyu mtumishi hakuna anapoongeza bajeti, mshahara wake unakuwa ni ule ule, alichobadilisha ni kada, niombe hiyo sheria, Menejimenti ya Utumishi wa Umma mkaiangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista ni shahidi tumekuwa tukikulilia kilio hiki cha sheria hiyo inaumiza sana watumishi. Lakini kuna na miundo ambayo siyo rafiki tena kwa watumishi, leo hii Mheshimiwa Rais tunamshukuru ameunda Wizara ya TEHAMA.

Lakini kwenye muundo wa ma-*executive assistant* ambao ndiyo wasaidizi wenu bado wamekamatwa na hati mkato.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. JANEJELLY J. NTALE:** Mheshimiwa Spika, naona muda umeniishia lakini nitalileta kama swali naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

**SPIKA:** huyo ni Janejelly James Ntale, Mheshimiwa Esther Matiko alifikiria atajaribu maji haya maji marefu. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kuwa sehemu ya Bunge hili la Kumi na Mbili. Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Biharamulo walioniamini na kunichagua kwa kura nyingi za kishindo niwe muwakilishi wao katika Bunge hili, lakini bila kumsahau mke wangu mpenzi *Engineer* Ebzenia kwa *support* kubwa ambayo amenipa na watoto wangu wawili Isack na Ebenezer. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka mimi ningependa kuchangia kwasababu ya muda nimekuwa katika viwanda kwa muda mrefu kidogo takriban miaka 14 nimekuwa nafanyakazi katika viwanda kama *engineer*, kwahiyo ningependa nijikite hapa zaidi. Nimejaribu kuangalia tumetengeneza ajira takribani 480,000 katika viwanda 8,447 ambavyo tumevitalisha katika muda huu wa miaka mitano. Sasa nikijaribu kuangalia *average* ni sawasawa na kila kiwanda kimetengeneza ajira 56, sasa najaribu kuangalia tuna-*target* ya kutengeneza ajira milioni nane na tukisikiliza au kupitia hotuba ya Rais aliyoitoe hapa *focus* kubwa tuna *target* kuangalia *integration* ya mazao ya kilimo yaweze ku-*integrate* na viwanda ili tuone sasa mambo ambayo tunayachakata hapa katika kilimo, mifugo na uvuvi ambao

umeajiri Watanzania wengi ndiyo viweze kuwa vyanzo vikubwa vya ku-*integrate* ajira hizi katika viwanda.

Sasa nilikuwa najaribu kupiga hesabu *let's say* tunataka ku-*create* ajira milioni mbili tu kutoka katika viwanda maana yake tunahitaji tutengeneze viwanda takribani 33,000 tukienda na mwendo huu viwanda vile vya kawaida. Sasa ninachojaribu kukichangia hapa ni nini au maoni yangu ambayo ninayo ni nini? Tujaribu kujikita zaidi katika kuwezesha watu wenye viwanda ambao wanaviwanda tayari.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano *Breweries* wana-*import* ngano hapa na tumeangalia hotuba ya Rais inasema tunaingiza ngano takriban tani 800,000 kwa mwaka. Sasa tukiongea na *Breweries* tukajipanga tukawapa mashamba wao kwanza wawe ndiyo watu wa kwanza wa kulima kama wanavyofanya watu wa miwa na watu wengine yeye mwenyewe azalishe *raw material* kwa ajili ya ku-*feed* viwanda vyake huyo atatutengenezea ajira, ataajiri vijana wetu ambao wanasoma katika vyuo kwa mfano *SUA* na sehemu nyingine hiyo tu ni ajira tosha kwanza itazuia *importation* ya ngano, lakini vilevile itatengeneza ajira kwaajili ya vijana.

Mimi nimekuwa katika viwanda vya sukari nimekuwa naona kwa mfano kiwanda kimoja unakuta kimeajiri takribani Watanzania 10,000 wanaofanyakazi katika kiwanda cha Kagera au Mtibwa, ni watu wengi sana hawa ambao wamekuwa wameajiriwa huko. Kwa hiyo nikawa nasema *same applies* kwenye alizeti, niko katika Kamati ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Waziri uliongelea suala la Kiwanda cha Singida kwamba kina-*operate* katika 35% of *installed capacity* sasa kiwanda ambacho kinafanyakazi katika 35% of *installed capacity*, kama tungekiwezesha kwanza kiwanda chenyewe tukakipa eneo la kulima kama kiwanda, kikalima alizeti yake yenyewe maana yake kiwanda kile kingejajiri Watanzania katika mashamba yake ya alizeti watu wengine pia wangeweza kulima na kuuza katika kiwanda kile maana yake kiwanda tungeweza ku-*boost production* yake ikapanda zaidi kwa sababu *raw material* ipo na kiwanda

hakifanyi kazi katika *installed capacity* kwa sababu malighafi ya ku-*supply* katika kiwanda kile huenda ina *scarcity* yake pia. *Same applies* kwenye sehemu kama za kwetu...

**SPIKA:** *Engineer* Ezra mbegu ya alizeti hakuna, mbegu ya alizeti iko wapi? Endelea tu.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, najua mbegu ya alizeti hakuna ndiyo tunapohitaji sasa Wizara ya Kilimo ijikite katika hili kwa sababu kama tunategemea ajira ya Watanzania wengi iko katika kilimo tukasema mbegu ya alizeti hamna, halikadhalika tutasema na mbegu ya michikichi Kigoma hamna na bado tunaagiza mafuta *it's a shame* kwa nchi kama hii juzi meli ya mafuta inakuja hapa Waziri anashangilia anasema meli ya mafuta imekuja hapa wakati wale watu kule bado tunaweza tukaongea nao hata wao wenyewe wanachokifanya kule tukaweza kuki-*copy* hapa tulete wawekezaji kule wanaozalisha mafuta ya mchikichi tuwaleta Kigoma pale, tuwaambie na sisi tuna michikichi hapa hebu waweke kiwanda Kigoma halafu tuwahimize watu wao wenyewe wenye kiwanda kwanza watalima mashamba yao, wataajiri jirani zangu wa Kigoma, halikadhalika walio na mashamba ya michikichi pale wataweza kuuza kwenye kiwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata mimi nina maeneo makubwa, Biharamulo tuna mapori ambayo yamekuwa yanateka Watanzania wanaumia kwa muda mrefu tunaweza kulima alizeti pale au tukaweka mwekezaji akalima alizeti ndugu zangu wa Biharamulo pale wakaweza kuajiriwa. (*Makofi*)

Lakini ajira tunapoipata ile maana yake tunabeba wakulima watu wa chini kabisa ambao wanashida ni wakulima hata mimi mtu atalima heka moja, atalima heka mbili, kwa sababu anajua kiwanda kiko pale ataweza kuuza kwenye kiwanda.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, naona muda hautoshi naomba kuunga hoja 100% nadhani nitaongea kwenye mipango pia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru *Engineer* Chiwelesa ni mawazo mazuri sana, yaani ni kweli mimi Jimbo langu wanalima sana alizeti, lakini mbegu zinazolimwa yaani ni za wananchi za kuokota okota hizi. Unakwenda unakuta mtu kalima heka 30, 40 lakini vializeti kwa sababu nimbegu ambazo zimerudiwa rudiwa vijijini mle hakuna mbegu na ukipata mbegu kiasi kidogo ni *very expensive*. Kwa hiyo eneo hili la mbegu Wizara ya Kilimo iwe ya mahindi, iwe ya alizeti mbegu mbegu ziko wapi? Hapa Dodoma hebu mtu anipeleke kwenye duka la mbegu liko wapi, sisi hatuwezi kusema tu wakati lazima *something has to be done somewhere* wale ASA wale maneno tu wale ASA, sisi wakulima tunajua hilo.

Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako tukufu na mimi kwa nafasi ya pekee naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Mwenyezi Mungu, nitoe shukrani nyingi sana kwa chama changu Chama cha Mapinduzi kikiongozwa na Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli. Lakini pia niishukuru familia yangu mke wangu watoto wangu lakini kwa nafasi ya pekee pia wapiga kura wa Jimbo la Nkenge ambao walitupatia kura pacha 91% pamoja na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba za Mheshimiwa Rais ambazo kwa kweli zinatia faraja, zinatia matumaini zinatoa muelekeo na kuonyesha kwamba Rais yuko kwenye mstari wa kupeleka nchi yetu katika uchumi ambao ni wa juu zaidi kuliko ambavyo tumefikia sasa hivi kwa kazi nzuri iliyofanyika katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, tunaona faraja kubwa inatoka wapi katika nchi yetu, kwanza ni kusimamia tunu za Taifa; amani, mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Muungano na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ndiyo inatoa fursa kwa watu

walioko nje ya Tanzania kuweza kuona ni fursa nzuri ya kuweza kuwekeza katika nchi ya Tanzania na hii ni ushahidi mwingi kweli tumeona mikataba mikubwa ya madini ikirejewa tumeona mikataba ikiendelea kusainiwa mipya lakini tunaona mapinduzi makubwa ya kiuchumi na hii siyo peke yake ni kwa sababu ya Mheshimiwa Rais akiwa na wasaidizi wake mahiri kuanzia Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri alio wateua.

Mheshimiwa Spika, tunaona kutokana na taarifa ya *IMF* ya mwaka 2019 uchumi wa nchi yetu unaendelea kupaa na Tanzania inakuwa miongoni mwa nchi kumi bora katika Bara la Afrika. Naamini kwa hotuba hii aliyowasilisha katika kipindi hiki basi tutaenda kuwa nchi ya kwanza kati ya hizo kumi katika Bara la Afrika na kuzidi nchi nyingine za Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na nia ya dhati ya kuona Rais anataka kutuvusha katika miaka mitano mingine ijayo niombe kuchangia kidogo katika maeneo mengine. Niseme kwamba hotuba ile imeshamaliza kila kitu, hapa tupo tunaboresha na kuweka kachumbari ili mambo yaende, lakini muelekeo wa nchi umesheheni katika hotuba ya Mheshimiwa Rais na hivyo hatuna budi sisi kama washauri, kama wasimamizi, kama watendaji kuhakikisha sasa tunayaishi haya ambayo Mheshimiwa Rais ametuambia kwenye hotuba yake ili aweze kutufikisha pale ambapo anaona inafaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nishauri kidogo kwenye eneo la viwanda, tunaona nchi yetu ambavyo imeendelea kupambana kuhakikisha kwamba inakuwa na viwanda vya kutosha ili tuendeleo kupata mchango mkubwa kutoka kwenye viwanda na tunaona viwanda vingi takribani 8,477 ambavyo vimeweza kuanzishwa katika awamu ya kwanza ya Mheshimiwa Rais. Lakini tunaona mchango wa Pato la Taifa kutoka kwenye viwanda ni zaidi ya 8.5%.

Mheshimiwa Spika, tunaona ajira zaidi ya 480,000 kutoka kwenye viwanda. Niseme kwa kaka yangu

Mheshimiwa Waziri wa Viwanda tunapokuwa tunaona kiwanda chochote kinaguswa lazima tuamke tuweze kuona ni jinsi gani ya kukilinda na Wizara zetu niombe ziongee lugha moja ambayo inaweza kuinua Wizara nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikupe mfano wa kiwanda kimoja kiko katika Jimbo langu la Nkenge, Wilaya ya Misenyi. Kiwanda hicho ni cha Oram kilikuwa ninachakata na ku-*grade* kahawa ukiangalia *capital investment* iliyowekwa kwenye kiwanda hicho, sasa hivi kimebaki ni magofu kwasababu ya mabadiliko kidogo ya kisera. Najua nchi yetu inao utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba mambo yanaenda sawa, lakini mambo mengine lazima tuwe *flexible* kidogo kuona ni kitu gani ambacho tunaweza kufanya ili mambo yote yaweze kwenda. Kuna mabadiliko kidogo ya sheria katika kilimo kwamba kahawa zote zinunuliwe na *AMCOS*. Kwa hiyo, maana yake viwanda ambavyo vilikuwa vinaendeshwa vyote vika *paralyse*.

Mheshimiwa Spika, wananchi sasa hivi wanalia, kahawa wanazipeleka kule, zinabaki muda mrefu bila malipo kiwanda hicho kilikuwa kinatoa bei nzuri na wananchi wanalipwa kwa wakati, inachangia Pato la Taifa kinaajiri zaidi ya watu 2000 katika Wilaya ya Misenyi. Sasa hivi vijana wote wamerudi mtaani wapo wanamililia Mbunge wao sijui nitawapeleka wapi. Kaka yangu Mwambe, kaka yangu Bashe najua nyie mko *smart*, naomba mkae pamoja mu-*harmonize* muweze kuhakikisha kwamba kiwanda hicho cha Oram kirudi kufanya kazi ili uchumi wa nchi, lakini na uchumi wa Misenyi uweze kukomboka.

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa muda ulionipa naomba kuunga hoja hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsanteni. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Misenyi, Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Chemba atafatiwa na Mheshimiwa Rose Busiga, kama Mheshimiwa Monni hayupo Mheshimiwa Rose Busiga.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ni kwa mara yangu ya kwanza kuchangia kwenye Bunge lako tukufu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuingia kwenye Bunge hili tukufu, ni kwa mara yangu ya kwanza na ninamshukuru Mungu na nawashukuru pia na watumishi wa Mungu walikeshwa kuomba usiku na mchana ili mimi niweze kuingia kwenye Bunge tukufu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru baba yangu mzazi na familia yangu nzima na mume wangu kwa kunipa ruhusa hii kuja kutumikia Bunge hili tukufu maana si kawaida kwa wanaume kumruhusu mwanamke kuja kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote...

**SPIKA:** Jamani mmesikia Waheshimiwa karuhusiwa huyo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nina furaha kubwa sana na nilikuwa natamani nipate nafasi hii ikiwezekana naomba uniongeze dakika mbili tu kwa ajili ya kusema haya. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kuongoza vizuri Chama chetu cha Mapinduzi kwa kuipatia heshima kubwa iliyotukuka katika Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais huyu niwa kuigwa, hajawahitokea toka Tanzania iumbwe, napenda kulisema mbele ya Bunge lako tukufu hili 2015 mara tu baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kupata nafasi ya kuwa Rais ninaamini kabisa kwa watu ambao wanamtegemea Mungu, Rais huyu aliamua kuichukua Tanzania na kumkabidhi Mungu aliye hai na ndio maana watu wengine wanaweza wakasema uchaguzi ulikuwa hauna haki, lakini kwa mtu ambaye anamtegemea Mungu, Rais aliamua kuichukua Tanzania na kuipeleka kwa Mungu kwa malengo tu, ukimtumikia Mungu utapata hekima, utakuwa na maarifa,



utakuwa na busara. Ndio maana leo hii Tanzania sisi ni matajiri.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais nikiamini hata yaliyobakia kwa miaka mitano hii yote yanakwenda kukamilika. Jamani naomba nizungumze hili mwaka 2020 ninaamini kabisa Watendaji wa Kata nchi nzima na mimi nikiwemo nililingia kule Ikulu kwa mara yangu ya kwanza na Bunge hili mimi ni Mtendaji wa Kata na kila Mheshimiwa Mbunge namwambia mimi ni Mtendaji wa Kata najivuna kwa kazi niliyokuwa nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asingekuwa huyu Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli wa wanyonge, mimi ningeingia humu? Jamani lazima tujiulize, na ndio maana jina langu lilipita kwa kila Kamati jina langu lilikuwemo mimi mnyonge na leo hii naunga mkono kwa asilimia mia moja miaka iliyobakia yote ambayo hatujafanikiwa Rais kuyafikia yote yatafika na zaidi nasema nawaunga mkono Mawaziri, baba yangu hapo Waziri Mkuu usiogope, Mungu amekuteua wewe, lakini pia na Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote chapeni kazi mtangulizeni Mungu mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumejaliwa kuwa na Rais simba, akiunguruma baba watu ameunguruma na mimi naidhihirisha Tanzania nitamuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano asilimia mia moja, na sitaona haya kusema mazuri yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana nikakwambia naomba dakika mbili ninayo mazuri mengi, una daraja la Busisi kule Geita.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose ngoja, hebu ongezeni dakika mbili hapo. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tulivyoenda kule Ikulu, nilipofika Dar es Salaam, nikajua ni Dar es Salaam ya sasa ni kama Marekani kumbe ni

Tanzania. Mheshimiwa Rais kwa upendeleo kabisa akatupa na *pocket money* tukatembee tembee, nani kama Dkt. Magufuli jamani?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nazungumza haya kutoka kwenye vilindi vya moyo, nataka niwaambie watanzania mnaweza mkasema wakati tunatafuta kura za Chama cha Mapinduzi, kwa wanawake wa Geita, kwanza ninawashukuru sana wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Geita kwa kuniamini kama Mbunge wao na sitawaangusha, wanawake wote yaani ukishataja tu tunaomba kura za Mheshimiwa Rais tulikuwa tunapita wote na Wabunge, na ndio maana hakuna kura iliyoibiwa, hakuna kura iliyoibiwa kwa Tanzania nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jamani tunaangalia kule Mwanza, daraja la Busisi, tunategemea sisi Wasukuma tutakuwa tunapita pale huku tuna baskeli tumepakiza tunakula na muwa, ilikuwa haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nitazidi kuongea kwa kumuunga mkono amefanya mengi, anatumpenda Watanzania naombeni tumuelewe, naombeni tumtie moyo pamoja na Serikali yake na Waziri. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Huyu ni Mtendaji Mheshimiwa Rose Busiga, Mbunge wa Viti Maalum - Geita na alikuwa mtendaji kata katika Mkoa huu huu wa Dodoma. Kwa hiyo, ni kweli. kwa hiyo, tunaye Gavana hapa wa Kata anaweza akawaweka ndani saa 24, ahsante sana Mheshimiwa Rose. Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato atafuatiwa na Mheshimiwa Kirumbe Nenga

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia. Napenda kumshukuru Mungu sana kwasababu ni mara yangu ya kwanza kuwa katika Bunge hili na kuchangia

hotuba ya Rais. Hotuba ya Rais hii nimeipitia yote na ni hotuba yenye maono mazuri sana, yenye mwelekeo mzuri, iliyosheheni kila aina ya maendeleo ambao wananchi wowote wangehitaji kuwa nayo katika nchi yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli amejipambanua katika Afrika kuwa Rais ambaye ni wa peke sana, vyombo vya habari vimekuwa vikimsema sana kwa muda mfupi na haijawahi kutokea kwa Rais kama yeye kusemwa na nchi mbalimbali. Hiyo ni dalili tosha kwamba ameleta mabadiliko ya kutosha na tumeona katika miaka hii mitano akiwa anashughulikia nyanja mbalimbali japokuwa yeye kama alivyokwisha kusema mtu mmoja ni msomi katika eneo moja. Lakini amekuwa mtaalam katika maeneo yote karibu ya nchi yetu hii. Kwa hiyo, pongezi nyingi sana nazitoa kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa safari hii pia napenda kumshukuru sana kwa sababu ukiangalia hata baraza lake la Mawaziri wengi tulitegemea, wakati bahasha inaletwa Waziri Mkuu nilijua atarudi yuleyule. Kwa sababu kwa kazi aliyofanya Mheshimiwa Kassim Majaliwa nilitegemea tu angerudi, na wengine nilijua watarudi na wamerudi kweli. Kwa hiyo, ninamuona kabisa kwamba Rais amewaamini na hata wale ambao wengine wamefanya kazi pamoja naye amewaamini sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie suala la elimu. Elimu imetolewa sasa ni bure kuanzia darasa la kwanza mpaka *form four* na hii imesaidia sana katika kupunguza mambo mengi. Kwa mfano tulikuwa na wasichana wengi waliokuwa wanamaliza darasa la saba, uwezo wa wazazi wao ulikuwa ni wa chini ndio walikuwa wanategemewa kuwa *ma-house girl* katika sehemu mbalimbali na kwa kweli hawa walikuwa wananyanyasika sana, *ma-house girl* wengine walikuwa wanapata mishahara midogo na mwisho walikuwa wanaishia tu katika kuhangaika, lakini sasa hivi katika umri huo wa utoto wengi watakuwa shule, kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata upatikanaji wa mimba kwa watoto wa kike utashuka sana kwa sababu umri huo wa watoto wa chini ya miaka 18 watakuwa mashuleni, kwa hiyo, hii elimu bure itakuwa na faida kubwa sana. Lakini vilevile hata vijana wa kiume ambao wengi walikuwa wanajiingiza katika makundi makundi ya kuwa wezi na wadokozi, sasa nao watakuwa shule, kwa hiyo, baadae watakuwa wakubwa na watakuwa ni wa kuwajielewa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni katika upande wa afya, afya pia imeamirika sana kulikuwa kuna changamoto sana ya wananchi hasa ya kinamama kuogopa kwenda hospitali na kwenda kwa waganga wa kienyeji kwenda kupata tiba huko kwa sababu walikuwa wakifika hospitalini walikuwa wanapata changamoto. Lakini kutokana na Chama cha Mapinduzi ambacho kimeongeza hospitali nyingi hadi kufikia katika vijiji sasa imebaki kazi moja kuwahamasisha wananchi wote kuzitumia hizi huduma afya na kubadilisha mtizamo ule wa kuamini maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo pia ninaweza labda nikaiona je, Serikali sasa iweze kujikita katika kuwasaidia wananchi katika kubadilisha mtazamo, kubadilisha mtazamo ni jambo ambalo ni gumu kitu mtu anachokiamini tangu amezaliwa ni ngumu hospitali inaweza ikawepo, dawa zikawepo, wahudumu wakawepo lakini bado mtu asiende kule kwasababu zake binafsi labda alihaminishwa kwamba hospitali sio sehemu sahihi ya kwenda ukienda kwa mtu fulani ndiyo atakayekuhudumia au hasa katika wazazi unakuta mama mjamzito haendi kwenda kujifungua hospitalini au anakwenda hospitalini baada ya hatua imeshafikia mbaya na mwisho wake ndio vile vifo vichache ambavyo tunavisema wakati ambapo huyu mama kama angeweza kwenda mapema angeweza kupata huduma ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa ni kazi yetu sisi kuweza kuhamasisha wananchi wetu kuanzia chini kabisa kubadili tabia zao ili kuweza kuepuka magonjwa yale ambayo yanaweza kuzuilika na kuzitumia huduma zetu za

afya ili waweze kupata afya njema na kuweza kupona magonjwa ambayo yanazuilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, mwakilishi wa vyuo vikuu, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga na wenzangu wote....

**SPIKA:** Kwa wale wengine wasiomfahamu huyu ndio Mbunge wa Kigoma Mjini eeeh! Si mnaelewa.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu waliotangulia kuutambua utukufu wa Mungu katika kutuweka hapa, naungana pia na wenzangu kukishukuru Chama cha Mapinduzi na wapiga kura wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala unaohusu hotuba ya Rais wetu ni mjadala wenye kusudio kubwa moja la kutafsiri dira hii aliyoitoa Rais wetu katika utekelezaji wa kazi za Serikali na Taifa kwa ujumla. Kama ulivyosikia wazungumzaji waliotangulia na wengine hakuna anayekosoa wala kupinga, maana yake wote tunaikubali kwamba hii ni dira ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati kuanza kazi za uongozi wa siasa toka kipindi cha mwisho cha Mwalimu alipokuwa anamalizia nafasi yake ya uongozi.

Kwa hiyo, nimepata nafasi ya kujifunza kutoka kwa Mwalimu, kwa Mzee Mwinyi, Hayati Mzee Mkapa na Mzee wetu Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, wazee wote hawa kwa kweli walikuwa na vipawa mbalimbali ambavyo vimelifikisha Taifa letu mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme juu ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, huyu mtu amepewa uthubutu wa aina yake haogopi, hakuna mtu alifikiri kwamba unaweza ukawa Rais usiende nje kupiga magoti kwa wakubwa hawa halafu ukaongoza nchi vizuri, lakini ametufikisha hapo na sasa tunaamini unaweza ukaongoza Taifa la Tanzania bila kwenda kupiga magoti huko nje na shughuli zikaenda. Ni Rais ambaye amekuwa na uwezo mkubwa wa kutafsiri nadharia katika vitendo katika muda mfupi, anaamua jambo hili lifanyike na muda mfupi wananchi wanaona jambo limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuna jambo kubwa katika haya tunayozungumza zaidi ya kuonesha kwamba hotuba yake ni dira kwa Taifa letu. Katika kipindi cha miaka ya 1990, Chama chetu cha Mapinduzi kilijikita katika sera ya kutaka kulitoa Taifa letu kuwa Taifa lenye uchumi tegemezi na kulileta kwenye uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Tumekwenda hivyo katika kipindi chote, lakini sasa tunauona mwanga, mwanga huu tunauona hapa tulipofikia kwenye hatua ya kuwa kwenye uchumi wa kati kwenye kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokusudia kusema hapa ni kwamba sekta ya viwanda ambayo sasa imetupiga *tafu* (imesaidia) kubwa ni lazima tuiongezee kasi na katika kuiongezea kasi ni kuiongezea kasi katika kuiongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji, wenzangu wengi wameshahieleza. Lakini niseme kwa upande wa Mkoa wetu wa Kigoma, sisi tunaweza tukasaidia sana Taifa letu kuondokana na fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta ya kula kutoka nje na Serikali imeanza na Waziri Mkuu huyu Mheshimiwa Kassim Majaliwa amekuwa ndio askari wa mstari wa mbele wa kuhakikisha zao la michikichi linalimwa, linakuzwa na ikiwezekana linavunwa na kusaidia kuondokana na tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto tuliyonayo, kulima ni mchakato mrefu, na mabenki yetu mengi si rafiki kwa mkulima, miaka mitatu ya kutunza mchikichi mpaka uanze kuzaa ni changamoto kwa wakulima wetu. Kwa hiyo, Serikali

iangalie uwezekano wa kutumia fedha, mfuko sijui wa kilimo kwanza kuwapa kama ruzuku wale wakulima ili waweze kusaidia kulima na tuweze kuondokana na tatizo la kuagiza mafuta kutoka nje. Mafuta ambayo siyo tu ni gharama, lakini ni hatari kwa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niliseme ni lile ambalo Mheshimiwa Rais amelisema katika ukurasa wa 27 wa hotuba yake nalo linahusu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele naunga mkono hoja mengine tutachangia katika mpango ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge wa Igunga Mheshimiwa Nicholas Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na nchi, kwa kupata fursa ya kuwa sehemu ya Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa ridhaa ya kuwa mpeperusha bendera wa Jimbo la Igunga na hatimaye nikaibuka na ushindi na kuwa Mbunge wa Igunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa umuhimu mkubwa niwashukuru sana baadhi ya viongozi ambao kwa wakati mmoja mlipita maeneo mbalimbali mkitunadi na mkituombea kura, naamini ushindi wetu umechangiwa na uwepo wenu katika maeneo yetu na hapa nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowataja majina kwa uchache; kwanza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, mama Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, wewe mwenyewe binafsi Mheshimiwa Spika, Job Ndugai, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dkt. Bashiru

Ally Kakulwa, Wajumbe wote wa Kamati na Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi, akiwepo Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Humphrey Polepole tunawashukuru kwa kuja kwenye maeneo yetu kutupigia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa umuhimu mkubwa niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Igunga ambao walifanya nipate ushindi wa kishindo na hatimaye leo nimeweza kuingia kwenye Bunge hili, ahadi yangu kwao nitawatumikia kwa moyo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa nina muda mchache kwanza nijikite katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, maeneo ambayo ningependa kuchangia jioni hii ni upande wa huduma za kijamii na miundombinu ya kiuchumi. Kwenye huduma za kijamii, Mheshimiwa tunaanza na suala la elimu, katika upande wa elimu Mheshimiwa amesema tutaendelea kutoa elimu bure ya bila malipo, lakini pia na kuboresha miundombinu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, niwashauri Wizara ya Elimu ambao wanamsaidia Rais na Wizara ya TAMISEMI, waje na mipango madhubuti watakatayohakikisha tunapata miundombinu ya uhakika na siyo inapofikia mwezi wa kumi na mbili na mwezi wa kumi na moja tunaanza kusumbuana kuhusu madawati, madarasa na upungufu wa vifaa vya kufundishia mashuleni, naamini kwenye mpango utakaokuja watakuja hatua madhubuti kwa ajili ya kuliona hili.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwenye suala la maji, nashukuru sisi Mkoa wa Tabora tumepata Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, changamoto kubwa imebaki kwenye usambazaji na hususani kwenye suala la viwango vya bei, naomba Wizara ya Maji waliangalie hili waje na viwango vipya ambavyo vitaweza kuwasaidia wananchi wengi wa maisha ya chini na hili napenda kutolea mfano kwa mfano kwenye suala la umeme, umeme walikuja na ile programu ya REA wanatoa umeme kwa 27,000 vijijini kwa hiyo na Wizara ya Maji tunawashauri waje na programu itakayoweza



wananchi wengi kuunganishiwa maji ili waweze kutatua tatizo la ukame kwenye majibo yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ni upande wa afya katika upande wa afya pia kuna changamoto kubwa upatikanaji wa madawa na vifaatiba, lakini pia kuna upungufu wa wahuguzi wa madaktari tunaomba pia Wizara ya Afya na TAMISEMI ambao mnasimamia hutowaji wa hizi huduma na sera muweze kuziangalia pia tuweze kutatua changamoto kubwa hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia jioni hii ni suala la kilimo kwenye kilimo sisi ukanda wetu sisi tunalima sana pamba, changamoto ambayo tumekuwa tukikabiliana ni suala la wakulima kuchelewa kulipwa na ninaishukuru mwisho wa mwaka tulipokuwa tunaelekea kwenye uchaguzi kulikuwa kuna madeni, lakini Serikali waliweza kukamilisha hayo.

Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe, Mbunge na jirani yangu alinisaidia sana ilikuwa ni changamoto sana wakati wa uchaguzi lakini tuliwasiliana naye akatowa maelekezo bodi ya pamba wakatulipa. Tunaomba safari hii msimu wa pamba utakapofika kipindi cha mauzo Wizara ijipange vizuri tuhakikishe wakulima hawatoki na madeni.

Mheshimiwa Spika, lakini changamoto nyingine kwenye kilimo ni suala la stakabadhi ghalani na *AMCOS* tungeomba pia hili suala hususani wakulima wa choroko linawasumbua sana tunaomba wizara ijipange mapema itakapofika kipindi cha kuuza mkulima anakwenda kuuza kilo mbili kilo tatu kilo tano haitaji kusubiri mwezi moja miezi miwili aweze kupata malipo yake ili itatusaidia sana kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashukuru sana ahsante sana kwa kupata fursa hii naunga mkono hoja asilimia mia moja nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngassa kutoka kule Igunga, Mheshimiwa Aloyce Kwezi atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi naomba nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kaliua lakini pili naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na Chama changu Chama cha Mapinduzi na tatu nishukuru familia yangu kwa kusimama na mimi katika kipindi chote cha uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa ili niweze kuishukuru sana Serikali kwa michango mizuri ambayo imeweza kutusaidia. Suala la kwanza ni kama alivyotoka kuliongelea Mbunge mwenzangu hususani maji. Tabora tumepata Mradi wa Ziwa Victoria wa shilingi bilioni 617 na tunaamini kabisa kuanzia mwezi wa Tano tunatarajia kabisa maji yale yataelekea katika jimbo la Kaliua, Sikonge na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa fadhila hizo tunaishukuru sana Serikali kwa upendo wa wananchi hususani kuwatua akinamama ndoo kichwani, naomba nichukue nafasi hii kushukuru kwamba Hospitali ya Wilaya ya Kaliua kwetu tulikuwa hatujakamilika, lakini hivi karibuni tumepokea zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kukamilisha Hospitali ya Wilaya ya Kaliua. Lakini tumepokea fedha za madarasa tumepokea, fedha za maabara na tumepokea fedha za ukumbi kwa Mkurugenzi, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, na nishukuru watendaji wote wa upendo kwa niaba ya wananchi wote ambao tunaendelea kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuboresha sehemu ambayo Wabunge wenzangu wamechangia wengi wamechangia hususani suala nzima la barabara. Barabara naona changamoto kubwa kwanza ni kubadilisha *celling* ya *TARURA* lazima fedha ziongezwe *TARURA* ili wananchi waweze kunufaika na barabara za vijijini. Hivi tunavyoongea, zipo kata mpaka sasa hivi hazifikiki kata kama Usinge kwenye jimbo

langu barabara imekatika, kata kama Useni kilometa 60 barabara imekatika kwa kweli hiki kitu kinatumiza sana na mimi nilikuwa najiuliza kwa sababu nilikuwa Mtendaji kipindi cha nyuma, hivi zile fedha za *emergence* ziko wapi siku hizi? Mimi ninajua ni Mfuko wa Dharura inapotokea dharula basi una-*take cover* muda ule ule, barabara inakatika kata zaidi ya watu 60,000 inaachwa Mfuko wa Dharura tunakwenda kwa stahili gani hii.

Mheshimiwa Spika, *emergence fund* iwe kwenye *level* ya mkoa ili taarifa zinapofika ndani ya wiki moja basi tunapotoa taarifa kwamba kuna barabara imekatika kule wananchi wasibaki kisiwani, kwa hiyo nilikuwa nashauri hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lapilli ningelipenda kushauri ni suala nzima la afya. Sisi wote tuko hapa kwa sababu mama zetu walijifungua vizuri ndiyo maana tumefikia *level* hii na ninaipongeza kwa kuanza vituo vya afya vile 487 ambavyo tumeanza navyo. Mimi nina uzoefu kidogo kwenye sekta hii, *operation* kwenye kituo cha afya kimoja natoa mfano wa Kilolo kilikuwa kinaitwa Kidabaga, ndani ya miezi mitatu mama zangu waliokuwa wanajifungua walifanyiwa *operation* akinamama 158; sasa nilikuwa najiuliza hivi kwa kweli tunashindwa kwenda kama tumeweza kwenye kata, kama tumeweza kujenga shule za kata, ni kwa nini tusingeze nguvu zaidi kwenye vituo vya afya ili kila kata iwe na kituo cha afya? Kwa sababu ajali nyingi za bodaboda zinatokea, *operation* zingeweza kutusaidia *x-ray* zinakuwepo pale kwenye kituo cha afya, lakini akinamama wanaojifungua ndiyo naona ni shida kubwa sana kutoka Makao Makuu ya Wilaya mpaka ukafike kijiji cha mwisho kilometa 250 kituo hakipo. Ni lazima tuangalie hiki kitu na tukipe kipaumbele cha pekee. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la tatu ambalo mimi ningeweza kushauri Serikali nilikuwa naishauri Serikali kuhusiana na suala zima la hifadhi, nakushukuru sana Waziri Mkuu Mungu akubariki sana ulipotoa ufafanuzi kuhusiana na mipaka ni kweli kabisa ni changamoto na ningeshauri pamoja

na Waziri wa Maliasili, lakini ashirikishwe Waziri wa Ardhi kwa sababu unaweza ukakuta unasema mpaka huu hapa, wananchi wanasema mpaka wetu unahishia hapa siku zote, *professionally* watu wa ardhi watuambie kwamba huu mpaka unapita eneo fulani kwa kweli kumekuwa na changamoto sana hususani Kaliua kwenye suala nzima la hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme naunga mkono hoja nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Kwezi, nilishakutaja Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunipatia nafasi hii ya Bunge ni nafasi adimu, mimi ninaisema ni kwa neema yake Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Pia nakishukuru Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Lindi na kutokana na juhudi na kazi zilizoonekana za Dkt. John Pombe Magufuli zimetia imani kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi hata mwaka jana tumepata majimbo yote kwa Chama cha Mapinduzi ukilinganisha na mwaka 2015. Pia nashukuru familia yangu na rafiki zetu wote kwa *support* walionipatia kwa muda wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika napenda kuchangia kwa muda mchache huu hotuba ya Mheshimiwa Rais kwenye ukurasa wa 32, 33 na 34 kwa maeneo ya sekta ya afya, maji na elimu. Napongeza kwa kazi zote alizofanya na ndiyo maana zimeandikiwa kwenye taarifa hii na pia hata kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba nini tutaenda kufanya kwa miaka hii mitano mpaka mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya kwa mafanikio ni makubwa, mimi mwenyewe nina uzoefu mkubwa kwenye sekta ya afya ndio nilipokulia mpaka sasa hivi, kwa sababu zaidi ya miaka 30 nimeendelea kuudumu huko kama

mwalimu muuguzi, na mkunga kwa hiyo, ninauzoefu mkubwa sana na maendeleo yaliyotokea na mafanikio yaliyotokea kwakweli ni makubwa sana huwa ninamwangalia Dkt. Johh Pombe Magufuli huyu ni daktari, huyu ni muuguzi ama yaani ana kila kila sifa, lakini nikiangalia kumbe ni sababu wa utegemezi wake kwa Mungu aliye hai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kuchangia kwa machache tu katika huduma za afya, pamoja na mafanikio yote hayo lakini kuongezwe ajira za wafanyakazi wa Wizara ya Afya ama idara hiyo ya afya ili tupate *skilled personnel*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu ukiwa na wafanyakazi wa kutosha hata huyu mama nikitolea mfano mama mjamzito au mama anayekuja kujifungua au mtoto anayekuja kupata huduma pale watakuwa na muda mfupi wa kukaa pale kwa huduma kama ni huduma za kutwa ama hata za kulazwa hospitali lakini kutakuwa na muda mzuri wa hudumu hawa kuwaudumia hawa wagonjwa na pia hata *stress* za wafanyakazi zitapungua, kwa sababu wafanyakazi wako wengi na hata huduma atakayopata yule mgonjwa ama mama yeyote basi itakuwa ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika eneo hilo hilo afya mimi kama Mbunge kwenye mkoa wangu au popote nitakaopita na utaalumu wangu nitaendelea kuwahamasisha akinamama wajawazito na watoto hata na jamii kwa ujumla waende kupata huduma za hospitali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuchangia kwenye sekta ya afya mafanikio mengi yamepatikana lakini tumeona changamoto hata Mheshimiwa Rais aliiona wakati wa kampeni kwamba maji bado vijijini. Kwa hiyo hata vijiji mbalimbali vya Mkoa wa Lindi vile vijiji vingine bado havijapata maji, nikiangalia yule mama mjamzito bado anaenda kuhangaika kutafuta maji bado anaangaika ili na lile kuangalia familia hivyo basi ni tatizo tunaomba maji, mwanamke huyu tumtue maji angalau hata anapokuwa

mjamzito asihangaika kutafuta maji, akihangaika huku na kule bado hata uzazi wake hautakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, pia nachangia kwenye sekta ya elimu kwa haraka haraka, nashukuru kwa elimu bila malipo hata mwanafunzi hata mtoto wa Mkoa wa Lindi anapata elimu na hata Tanzania nzima kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Lakini katika hili ninashukuru pia kwa kuzingatia masomo ya sayansi. Kwa uzoefu wangu wa vyuo vya afya mara nyingi tunakosa wanafunzi wazuri kwa sababu hawakufaulu sayansi kwa hiyo hilo nalo nalipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika elimu tunaomba elimu ya juu kwa Mkoa wa Lindi hakuna Chuo Kikuu kwa hiyo naomba kuwe na compass ya Chuo Kikuu Mkoa wa Lindi ili nako tupate elimu ya hali ya juu ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, sasa namuita Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais zote mbili, lakini pia naomba nichukue nafasi hii kwanza niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini kwa kunileta Bungeni kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme na niungane na wananchi wengine ambao wanasema kwamba Rais Magufuli ni chaguo la Mungu na ni kweli Rais Magufuli ni chaguo la Mungu. *(Makofi)*

Mimi kwenye Jimbo langu eneo kubwa ni eneo la maji, lakini Mheshimiwa Rais amekubali kukarabati meli ya Mv Liemba. Hivi sasa imeanza kukarabatiwa, lakini Mheshimiwa Rais siyo hivyo tu amekubali kutengeneza meli mbili moja itabeba watu na mizigo yao, lakini moja itabeba mizigo peke yake. Jimbo langu ni wahanga wa usafiri wa

maji kwa maana hiyo wanatumia usafiri wa mitungwi ambayo inatumia mbao, kwa maana hiyo kumekuwa na ajali nyingi sana, lakini meli hizi zikitengenezwa zikikamilika tutakuwa wananchi wa Kigoma Kusini tumepata ufumbuzi na watu watasafiri kwa raha mstarehe kwa maana kutakuwa hakuna ajali lakini pia watasafirisha mizigo yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati anapita jimboni kunadi sera za Chama cha Mapinduzi kuomba kura na kuniombea kura mimi alikubali kuongeza zahanati, kuongeza Hospitali ya Wilaya nyingine kwa maana Jimbo langu ni kubwa sana katika majimbo ya Mkoa wa Kigoma, alikubali kuongeza hospitali nyingine ya Wilaya maana yake mimi nakwenda kuwa na hospitali mbili za Wilaya ni jambo la kumshukuru sana Mheshimiwa Rais katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie katika habari ya uvuvi. Katika jimbo langu wananchi wanajishughulisha na uvuvi, namshukuru Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi aliweza kuwasikiliza wananchi wangu waliotoka jimboni kuja kuzungumzia malalamiko ya suala zima ya kanuni zilizokuwa siyo rafiki na wao na Mheshimiwa Waziri alionesha kabisa kusikitishwa kwa nini hizo kanuni ziliwekwa vile, kwa hiyo, nina imani Mheshimiwa Gekul ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi hili jambo anakwenda kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo litakwenda kuleta uchumi mzuri katika Jimbo la Kigoma Kusini kwa maana ya uvuvi, lakini pia Mheshimiwa jimbo langu wananchi wanajishughulisha na kilimo cha mpunga pamoja na mahindi na mihogo. Lakini ipo changamoto moja ambayo kwa kweli naomba Serikali iweze kusaidia, ni wanyama kwa maana ya mamba katika majaruba yale ya mpunga kwa mfano Kyala yaani watu wanakufa kwa sababu ya mamba ni wengi sana, tumejaribu kuwaambia watu wa mifugo wajaribu kupunguza wale mamba yaani mamba wale wana uwezo wa kuchukua binadamu yaani mmoja kwa kila siku, sasa fikiria kwa mwaka mzima ni watu wangapi.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze Mbunge wa Kigoma Kusini. Msemaji wetu wa mwisho anatoka Mwanakwerekwe Mheshimiwa Kassim Hassan Haji.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wa rehema na kutujalia kuwa wazima wa afya njema na kutuwezesha sote kuwa pamoja siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nikushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi ya kusimama katika Bunge lako tukufu kwa mara ya kwanza, pia nikishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuwakilisha wa Jimbo la Mwanakerekwe, naishukuru familia yangu pamoja na wananchi wa Jimbo la Mwanakerekwe kwa mashirikiano makubwa wanayonipa na nina wahaidi nitawatumikia Watanzania wote pamoja na wao kwa kuleta maendeleo mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ukitizama ukurasa wa 13 ameweka kipaumbele kikubwa katika miaka mitano kuendeleza, kulinda na kudumisha tunu za Taifa letu yaani amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu, uhuru wa nchi yetu, pamoja na Muungano na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Pia kuhaidi mashirikiano na Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi, na kulisitiza kuwa hata kuwa na mzaa kwa yeyote atakayetaka kukatisha uhuru wetu Muungano wetu na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, hali ambayo imefanya mpaka sasa hivi kuunda kwa Serikali



ya Umoja wa Kitaifa katika Kisiwa chetu cha Zanzibar na kuleta maendeleo ya uchumi katika Kisiwa cha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 14 wa hotuba hii Mheshimiwa Rais ameonesha kuonesha mashirikiano makubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuendelea kuleta maendeleo ya pande zote mbili za Muungano na kuahidi kuleta meli nne katika Kisiwa cha Unguja. Hii imekwenda kufanya kugawanya usawa, usawa wa meli nne ziwepo katika Tanzania Bara na meli nne zije katika Kisiwa cha Unguja inakwenda kutimiza lengo la sera ya uchumi wa *blue*.

Mheshimiwa Spika, pia utoawaji tumeona juzi tu utoaji wa hati, utiahaji saini wa hati wa yamakubaliano ya maridhiano katika ujenzi wa bandari kuu ambayo itajengwa na mji wa kisasa katika Kijiji cha Manga Pwani kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa katika hotuba yake na mimi nimalizie katika ukurasa 36 niipongeze Serikali kwa kutunga sheria mpya kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu; hii imekwenda kutuongozea ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi kwa vijana wetu ambao watakuwa wanajishughulisha na shughuli hizi na kufanya kwenda kuongeza Pato la Taifa letu la Tanzania, na mimi niunge mkono hoja na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa mashirikiano yake makubwa ambayo ameyaonesha katika kisiwa chetu cha Zanzibar na kufanya mikataba ambayo inakwenda ili iwe haki, uhuru na sisi kufanya Kisiwa cha Zanzibar kiwe kiwe kinamabadiliko makubwa katika miaka mitano inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana sana Mheshimiwa Mbunge Mwanakwerekwe kwa mchango wako. (*Makofi*)

Waheshimiwa bado orodha yetu ni ndefu, lakini basi wale ambao hamjapata nafasi ya kuchangia kesho muweke majina yenu vizuri yasijirudie rudie tutakuwa na nafasi bado ya kuweza kuhitimisha hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu

kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kulifungua Bunge hili ambayo ni *vision* yake ya miaka tano ijayo.

Nawashukuruni sana kwa jinsi ambavyo kwa kweli tumechangia vizuri sana na tuendeleo hivyo na tuendeleo kujiandaa kwa ajili ya wiki ijayo ambapo Mheshimiwa Waziri wa Mipango atakuja kuwasilisasha hotuba yake ya Mpango wa Taifa ambayo itakuwa ndiyo msingi kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2021/2022. Kwa hiyo, tuanze kujiandaa sasa.

Ninalo tangazo moja la kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye anawatangazieni kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa tamasha kubwa la muziki lililopewa jina la *Serengeti Music Festival 2021*, linaitwa *Serengeti Music Festival 2021*. Tamasha hili litafanyika siku ya Jumamosi tarehe 6 Februari, 2021 katika uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kuanzia saa kumi jioni. Tamasha hili litashirikisha wasanii wa kizazi kipya zaidi ya 60 wakiwemo wale wa Jiji la Dodoma.

Muhimu sasa tamasha hilo la Jumamosi litatanguliwa na matukio mbalimbali ikiwemo *Serengeti Royal Pre-Part* ambayo ni maalumu kwa viongozi wakiwemo ninyi Waheshimiwa Wabunge, tamasha hilo litakalotangulia hilo la tarehe 6 litafanyika kwenye hoteli ya *Royal Village* siku ya Ijumaa kesho kuanzia saa moja usiku na wasanii bora kabisa kumi watatumbuiza. Kwa hiyo, kesho *Royal* baada ya kuahirisha Bunge tu hapa tunaombwa Waheshimiwa twende tukaserebuke kidogo. (*Makofi*)

Pia ikumbukwe kwamba tarehe 5 Februari, ambayo ni kesho kinatimiza miaka 44 kwa hiyo, wizara itawaletea burudani hizi kwenye siku hiyo muhimu ya Taifa letu katika eneo lililopangwa. Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana na taratibu za maonesho haya zinatolewa katika vyombo mbalimbali na kurudiwa mara kwa mara. Mheshimiwa Waziri kuna kiingilio kesho au ni kuingia bure kule *Royal*.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na kwa vile ndiyo mara ya kwanza kwa ruhusa yako naomba nimshukuru Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuongoza hii Wizara. *(Makofi)*

Kuhusu *Pre-Part* ya kesho kutakuwa na kiingilio kidogo kwa ajili ya kuchangia wasanii wetu shilingi 20,000 ni kwa ajili ya kuchangia wasanii ambao watakuwa wanatuburudisha. Kwa hiyo ni 20,000 tu Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo mnakaribishwa pale *Royal*/jioni sana na kesho kutwa itakuwa kule Jumamosi Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Basi kazi zote za leo zimekamilika, naomba nichukue nafasi hii kuairisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Ijumaa, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01:04 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Februari, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*